

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 31 Mei, 2017

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi za Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2017/2018 .

MWENYEKITI: Ahsante, Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

MWENYEKITI: Swali la kwanza kwa siku ya leo ni la Mheshimiwa Aisharose Ndogholi Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Mussa Sima na linaelekezwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 307

**Uhaba wa Nyumba kwa Watumishi
wa Idara ya Afya Singida**

**MHE. MUSSA R. SIMA (K.n.y. MHE. AISHAROSE N.
MATEMBE)** aliuliza:-

Watumishi wa sekta ya afya hususani madaktari wanatakiwa kuishi kwenye maeneo ya kazi ili inapotokea akahitajika inakuwa rahisi kuwahi kwenda kutoa huduma kwa wagonjwa. Hata hivyo, katika Mkoa wa Singida watumishi wengi wa sekta ya afya wanaishi mbali na eneo la kazi hivyo kuwa na changamoto kubwa na wakati mwingine kusababisha vifo vya wagonjwa wakiwemo wajawazito.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha watumishi wa sekta ya afya wanakuwa na makazi kwenye maeneo jirani ikiwa ni pamoja na kuboresha nyumba chache zilizopo pamoja na kujenga zingine mpya?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aisharose Matembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida una jumla ya nyumba za watumishi wa sekta ya afya 345 katika nyumba 1,072 zinazohitajika. Hivyo, kuna upungufu wa nyumba za watumishi wa afya 737. Serikali inaendelea na ujenzi wa nyumba za watumishi 21 katika vituo vya afya na zahanati. Aidha, shilingi milioni 280.8 zimetengwa katika mwaka 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa nyumba za watumishi wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza kutoa ruzuku ya maendeleo (*Local Government Development*

Grant) ambayo inatumika kumalizia maboma yaliyoanza kwa nguvu za wananchi katika sekta za afya, elimu na sekta nyingine. Kipaumbele cha matumizi ya fedha hizo kinapangwa na Halmashauri zenyewe kuititia Mpango wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD).

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Sima swalii la nyongeza.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri kwa majibu mazuri naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la kwanza, kwa kuwa mwaka jana tuliomba fedha kwa ajili ya ukarabati Hospitali yetu ya Rufaa takribani shilingi bilioni 1.7 na tumekwishapata shillingi bilioni moja, je, fedha iliyobaki itakuja lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swalii la pili, nimuombe Mheshimiwa Waziri aseme kama atakuwa tayari kuambatana nami kwenda kuangalia hali ya Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa na Kituo cha Afya cha Sokoine. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Majibu Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika mpango wa bajeti ilitengwa karibuni shilingi bilioni 1.7 na ndio maana kwa mujibu wa Serikali kwa sababu mipango yake ni kuhakikisha miradi hii inatekelezeka tayari tumeshapeleka shilingi bilioni moja. Nishukuru sana wakati naongea na Sekretarieti ya Mkoa mwezi mmoja uliopita walikuwa katika michakato ya kuona ni jinsi gani fedha zile ziweze kutumika vizuri zaidi kuhakikisha kwamba jengo lile linakamilika. Hata hivyo, ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba hospitali hii inakamilika. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajitahidi kadri iwezekanavyo fedha zipatikane, mpango ule wa ujenzi wa Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa wa Singida iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swalii la pili kwamba ikiwezekana tuweze kuongozana, nimwambie Mheshimiwa Mbunge tujipange ikiwezekana hata kesho mchana, tutoke hapa mara moja tukafanye kazi turudi tuendelee na kazi za Bunge kwa sababu ni lazima tuhakikishe kwamba tunawafifikia wananchi kuweza kuwashudumia kwa karibu zaidi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Munde na Mheshimiwa Nape.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora Manispaa mara mbili tulitenga pesa kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya, tulianza majengo hayo miaka mitatu iliyopita, lakini na mwaka huu wa fedha tumetenga tena bajeti hiyo ya shillingi millioni 120 kwa ajili ya kuendeleza majengo hayo.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kutupa pesa ili tuweze kumalizia Hospitali hiyo ya Wilaya ili tuweze kutatua kero kubwa inayoikabili Hospitali yetu ya Rufaa kwa *population* kubwa iliyopo Tabora Manispaa ili wananchi waanzie kwenye Hospitali yao ya Wilaya?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimhakikishie Mheshimiwa Munde kwa sababu muda mwingi sana amekuwa ukipigia kelele Mkoa wake wa Tabora na ndio maana kwa mapenzi makubwa mpaka Mheshimiwa Rais akaona amkabidhi *ambulance* kwa ajili ya wananchi wake wa Tabora katika sekta ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili, naomba nimhakikishie kwamba mwaka wa fedha bado haujaisha, japokuwa tumepeleka fedha za *Local Government Development Grants* katika Halmashauri mbalimbali waweke

vipaumbele tutaangalia kwa Tabora nini kimewekezwa. Naomba nimhakikishie kwa sababu mwaka haujaisha tutajitahidi kwa kadiri iwezekanavyo bajeti ile iweze kufika ili mpango wa bajeti wa Manispaa ya Tabora uweze kukamilika kama ulivyokusudiwa katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ritta halafu baadaye Mheshimiwa Nape.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa swali la msingi linafanana kabisa na tatizo tulilonalo katika Hospitali yetu ya Mkoa, karibu asilimia 85 ya Madaktari wa Hospitali ya Mkoa wa Iringa wanaishi nje kabisa ya hospitali ile na kusababisha wagonjwa kupata matatizo makubwa wanapokuja usiku kwa ajili ya matibabu. Tatizo kubwa liiloko katika Hospitali ya Mkoa kuna mwingiliano wa Magereza na Hospitali. Tulishauri mara nydingi kwamba Waziri wetu wa Afya pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani waweze kukaa pamoja waone kwamba lile gereza liweze kutoka ili madaktari wengi waweze kukaa karibu na Hospitali ile ya Mkoa ili kusaidia wagonjwa wanaofika hata usiku.

Je, ni lini sasa ombi hilo la Mkoa litawenza kutekelezeka ili wananchi wa Iringa waweze kupata haki ya kupata madaktari wakati wote?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Kabati kwa sababu wiki mbili zilizopita tulikuwa pale Iringa tukaenda mpaka Kilolo na miongoni mwa mambo tuliyopitia katika sekta ya afya kipindi cha nyuma tulifika mpaka Hospitali ya Frelimo kwa ajili ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma. Kwa jambo hili,

naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu Waziri wa Afya na Waziri wa Mambo ya Ndani wameshakaa tayari ku-*discuss* jambo hilo, usihofu kila kitu kitaenda vizuri lengo kubwa ni tuweze kuwapatia huduma wananchi wetu vizuri. Kwa hiyo, hilo jambo ondoa hofu kila kitu kitaenda vizuri Serikali itashughulikia.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nape.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa tatizo la nyumba hizi za kukaa wahudumu wa afya hasa maeneo ya vijiji hasa Mikoa ya Lindi na Mtwara na Jimbo la Mtama ni kubwa sana. Pamoja na kazi nzuri sana inayofanywa na Taasisi ya Benjamin Mkapa ya ujenzi wa nyumba katika maeneo mbalimbali, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuanzisha mfuko maalum kwa ajili ya kulishughulikia tatizo hilli ili kusogezza huduma za afya karibu na wananchi wetu?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mkoaa wa Lindi ni mionganii mwa maeneo ambayo yana changamoto kubwa sana ya afya. Mheshimiwa Nape ni shahidi kwamba katika jambo ambalo amekuwa akilipigia kelele sana ni hilli la sekta ya afya na nimponeze sana katika utekelezaji wa llani *last week* alienda kukabidhi ile *ambulace*, nadhani wananchi wa Mtama wana-appreciate kazi kubwa anayoifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili alilotoa ni wazo zuri kwa sababu sasa hivi tunatumia fedha za *Local Government Development Grants* kwa ajili ya kuhakikisha miradi mingi hasa viporo inakamilika hasa katika ujenzi wa majengo mbalimbali ya afya na elimu. Ndiyo maana katika mpango wa bajeti ya mwaka huu tumetenga karibuni shilingi bilioni 251.18, lengo kubwa ni kuweshera upatikanaji wa makazi kwa wataalamu wetu.

Kwa hiyo, jambo la kuanzisha mfuko, nadhani kwa sasa tutumie huu mfumo tuliokuwa nao lakini wazo ni zuri tutalifanyia kazi kama Serikali kuona nini tufanye, lengo kubwa tuweze kutatua matatizo ya afya kwa Watanzania wote kwa ujumla wetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata Na.308 na linaulizwa na Mheshimiwa Allan Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki.

Na. 308

Hitaji la Ambulance Tatu

MHE. ALLAN J. KIULA aliuliza:-

Wilaya ya Mkalama ni mpya na haina vitendea kazi kama vile magari katika katika Idara ya Afya na huduma za dharura zinapatikana makao makuu huku tarafa zikiwa zimetawanyika hivyo wananchi hasa wajawazito na watoto wamekuwa wakipoteza maisha kabla ya kufika hospitali kwa kukosa usafiri.

Je, ni lini Serikali itatoa gari la wagonjwa (*ambulance*) tatu kwa kila tarafa ikiwemo Makao Makuu ili kunusuru vifo hivyo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais –TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Allan Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ina gari moja la kuhudumia wagonjwa lenye usajili wa namba SM 4263 ambalo lipo katika Kituo cha Afya Kinyangiri. Kwa sasa Halmashauri imeandaa mpango wa kuwashirikisha wadau mbalimbali ili kupata gari la

wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Nyamburi ambacho kimewekwa katika mpango wa kufanyiwa ukarabati mkubwa kuwezesha huduma za upasuuji kutolewa.

Aidha, Serikali imepanga kuimarisha vituo vya afya na zahanati ili ziwe na uwezo wa kutoa huduma kwa wagonjwa wengi na kupunguza rufaa kwenda katika Hospitali ya Wilaya. Ofisi ya Rais, TAMISEMI itatoa ushirikiano wake pale Halmashauri hiyo itakapoweka kipaumbele katika kutenga fedha kuititia mapato ya ndani kwa ajili ya ununuzi wa gari la wagonjwa katika eneo hilo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kiula, swali la nyongeza.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza naomba niweke rekodi sawasawa. Cha kwanza, Wilaya ya Mkalama haina Hospitali ya Wilaya, pili mapato ya ndani ni kidogo ukilinganisha na mahitaji ya Wilaya mpya zote Tanzania na tatu ni kwamba gari liliopo lilirithiwa kutoka Wilaya ya Iramba na uzoefu unaonyesha mgawanyo wa mali unapofanyika Wilaya mpya zinapata yale magari mabovu mabovu, hilo gari lipo tu kwenye vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ni lini Serikali itatoa magari mapya na ya uhakika kwa Wilaya zote mpya Tanzania ikiwepo Mkalama? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali pamoja na kujenga Kituo cha Afya ina mpango gani wa kunusuru vifo hasa vya akina mama na watoto katika mazingira ya kutokuwepo na gari la wagonjwa? Mheshimiwa Naibu Waziri ameshafika Mkalama na Naibu Waziri wa Afya naye alishafika Mkalama na kuona jiografia ile, hapa nilipo wananchi wangu wanalia kila siku msiba.

MWENYEKITI: Tumekuelewa Mheshimiwa.

MHE. ALLAN J. KIULA: Sawa.

MWENYEKITI: Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi muda wetu mnauona wote.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyezekiti, ni kweli Mheshimiwa Mbunge Jimbo lake limegawanyika kutokana na lile Jimbo alilokuwa Mheshimiwa Mwigulu Mchomba. Tulivyofika pale mionganoni mwa changamoto kubwa sana katika Jimbo lake, kwanza kweli hawana Hospitali ya Wilaya lakini ndiyo maana jambo kubwa tulilolifanya kutokana na shida kubwa iliyopatikana pale, Mheshimiwa Mbunge alinipeleka pale na tukaweza kuangalia kwa pamoja tukaweka katika mpango wao wa sasa kuhakikisha kwamba tunakikarabati kile Kituo cha Afya ili waweze kuwa na *theater* kabisa ya upasuaji wa watoto na Mungu akijalia tutapeleka mradi wa takribani shilingi milioni 700.

Mheshimiwa Mwenyezekiti, katika swali la lini gari la wagonjwa litapatikana, naomba nisitoe *commitment* ni lini litapatikana. Kama nilivyo sema awali katika majibu yangu ya msingi kwamba jambo kubwa hili tuanzie katika *needs assessment* ya Halmashauri yetu. Naomba niseme kwamba Serikali imesikia kilio cha Mheshimiwa Allan na tutaangalia uwezekano wowote utakaowezekana, tukipata fursa tutatoa kipaumbele kwa Jimbo la Mkalama kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma ya kutosha.

Mheshimiwa Mwelyekiti, hata hivyo, niseme kwamba kama Serikali kwa umoja wake inajua kwamba wananchi wa Mkalama wana shida kubwa sana, tutajadiliana kwa pamoja kwa mawazo mapana zaidi. Kwa sababu licha ya kutokuwa na vituo vya afya...

MWENYEKITI: Ahsante sana Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Hata miundombinu ya barabara kuwasaidia wagonjwa kufika hospitalini ni shida tutalifanyia kazi.

MWENYEKITI: Mbunge wa Ukerewe, Mheshimiwa Mkundi na Mheshimiwa Bura, wanatosha muda haupo.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa kuwa Ukerewe inaundwa na visiwa na kwa kuwa yanapotokea matatizo ya dharura kiafya inakuwa kazi ngumu sana kuwawahisha wagonjwa kupata huduma ya ziada.

Je, sasa Serikali haioni umuhimu wa kutoa *ambulance boat* kuweza kusaidia kuokoa maisha ya wananchi wa Ukerewe?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshiniwa Mwenyekiti, najua kwamba tulipeleka *ambulance* kule ya kawaida katika kipindi cha kati, lakini na mahitaji ya kwamba watu wa Ukerewe wapate *ambulance boat*, naomba Serikali tuchukue kwa mawazo yenu mapana. Kama Mbunge anavyofahamu tuliongea naye *private* kwamba tutafika Ukerewe baada ya Bunge hili, tukifika kule tutajadiliana kwa mapana na pamoja nini tutawasaidia wananchi wa Ukerewe. Pia jambo hili tutaangalia jinsi gani tuliweke katika kipaumbele kama Serikali kwa kuweka mawazo ya pamoja kwa upana wake.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Bura.

MHE. FELISTER A. BURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Chemba ni kati ya Wilaya mpya katika Mkoa wetu wa Dodoma. Ukitoka Kondo cha Chemba ni zaidi ya kilomita 50 na ukitoka Dodoma Mjini kwenda Chemba ni zaidi ya kilomita 100 lakini Kituo cha Afya kilichopo pale hakikidhi mahitaji na Kituo cha Bahi ambacho kinahesabika kama Hospitali ya Wilaya bado

kina upungufu makubwa. Je, lini Serikali itaungana na wananchi wa Chemba kuhakikisha kwamba Makao Makuu ya Wilaya inapata hospitali ya Wilaya?

MWENYEKITI: Ahsante, mjibu tu ni lini Mheshimiwa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyeekiti, ni lini ni kwamba mpango wa Serikali wa mwaka huu imetengwa shilingi milioni 23 ambayo ni kwa ajili ya kuhakikisha tunafanya maandalizi ya awali lakini tumeshaingiza katika mpango mwingine na vilevile wenzetu wa Chemba wako katika mchakato wa kushirikisha *National Health Insurance Fund* katika jambo hilo. Kwa hiyo, naomba tuseme kwamba mipango hii yote itaenda kwa pamoja kusaidia Chemba iweze kupata kituo cha afya. Hata hivyo, ndiyo maana tunaamua kufanya ukarabati mkubwa katika Kituo kimoja cha Afya cha Chemba na Bahi tupunguze *referral system* ili kusaidia wananchi kupata huduma za upasuaji wakiwa katika maeneo yao.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swalini namba 309 linaulizwa na Mheshimiwa Kemirembe Julius Lwota, Mbunge wa Viti Maalum

Na. 309

Ujenzi wa Duka la Dawa la MSD - Hospitali Teule ya Sengerema

MHE. KEMIREMBE J. LWOTA aliuliza:-

Je ni lini Serikali itaanza ujenzi wa duka la dawa la *MSD* kwenye Hospitali Teule ya Sengerema?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kwa niaba ya Waziri Wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba

kujibu swali la Mheshimiwa Kemirembe Julius Lwota, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba katika hospitali za umma, Serikali iliagiza maduka ya dawa yafunguliwe kwenye hospitali za umma. Kama sehemu ya utekelezaji wa agizo hilo, bohari ya dawa imeshafungua maduka katika hospitali za Muhimbili, *Mount Meru*, Ruangwa, Sekou Toure, Mbeya, Katavi na Chato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu wa kuanzisha duka la dawa katika hospitali una faida kubwa ambazo ni pamoja na kuunga mkono dhamira ya kuleta dawa na vifaa tiba karibu na wananchi; kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa bei nafuu na kwa ubora kwa Watanzania; kuunga mkono kwa vitendo juhudzi za Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na TAMISEMI katika kudhibiti kuongezeka kwa gharama za huduma za afya; kuondoa utegemezi wa fedha kutoka Serikali Kuu na kuhakikisha upatikanaji endelevu wa dawa na vifaa tiba kwa wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza agizo hilo kwa Tanzania nzima, inaonekana itahitajika rasilimali watu na rasilimali fedha nydingi sana ambapo bohari ya dawa ilikubaliana na TAMISEMI kuwa hospitali zilizo chini yake zifungue maduka yao zenyewe na *MSD* itatoa ushauri wa kitaalamu pamoja na kuzuzia dawa na vifaa tiba.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kemirembe, maswali la nyongeza.

MHE. KEMIREMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha dhahiri kabisa kwamba Serikali inabagua maeneo ambayo hayana Hospitali za Wilaya. Kwa mfano,

Wilaya ya Sengerema kuna hospitali moja ya *mission* inahudumia wananchi wote wa Wilaya ya Sengerema na kuna ombi ambalo limetolewa na wilaya yetu miaka minne iliyopita la kujenga Hospitali ya Wilaya Sengerema ya Serikali.

Je, ni lini Serikali itatekeleza ombi hili na kujenga Hospitali ya Wilaya ili kuweza kuweka huduma ya vifaa tiba na dawa katika Wilaya yetu ya Sengerema? Nashukuru. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishe tu kwamba Serikali haibagui Wilaya yoyote ile dhidi ya Wilaya nyingine kwa sababu Wilaya zote hizi mwisho wa siku ndio zinaunda nchi yetu Tanzania. Kwa hivyo, tunatoa huduma sawa kwa maeneo yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu hospitali ya Sengerema, nimefika kwenye hospitali ile na nimeshuhudia maendeleo makubwa yanayofanywa kwa ushirikiano baina ya *mission*, Mheshimiwa Mbunge, rafiki yangu na Mwenyekiti wangu wa *Bunge Sports Club* Mheshimiwa Ngeleja pamoja na Halmashauri yake na wadau mbalimbali wakiwemo *Vodacom Foundation* na kuna miradi mizuri inayoendelea katika Wilaya ya Sengerema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kujenga Hospitali ya Wilaya nimshauri Mheshimiwa Mbunge akishirikiana na Mheshimiwa Ngeleja kwa pamoja kwenye vikao vyao vya Halmashauri waweke kipaumbele cha kuanzisha mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Nina uhakika Mheshimiwa Jafo anasikiliza vizuri hapa atashirikiana nao kuwapa ufundi na sisi tutawapa ufundi, lakini pia ikibidi kama kuna rasilimali fedha tutawasaidia. Hata hivyo, uamuzi wa kwanza uwe ni wao wenywewe kuweka kipaumbele cha kuanzisha Hospitali ya Wilaya, lakini kwa sasa inaonyesha wameridhika na huduma zinazotolewa na Hospitali ya *Mission*.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ngeleja, Mheshimiwa Kapufi na Mheshimiwa Selasini.

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naishukuru sana Serikali kwa ufanuzi wa swali ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Kemirembé lakini nilitaka tu kupata *commitment* ya Serikali kwa sababu kwa kuwa ombi letu la Halmashauri ya Sengerema la huo mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Serikali lipo Serikalini kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

Je, ni lini Serikali itaunganisha nguvu na Halmashauri ya Sengerema kutekeleza mradi huu kwa sababu ombi letu lipo pale na Serikali inafahamu? Nachotaka kujua sasa hivi ni lini Serikali itatuwezesha kupitia kasma ambayo tumeiomba ukijumlisha na kasma ambayo tumeitenga sisi Sengerema ili tutekeleze mradi huo? Ahsante sana. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jafo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itafanya jambo hilo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ndiyo maana nimesema katika *commitment* yetu katika bajeti inayokuja tumetenga shilingi bilioni 251.18 ambapo katika fedha hizo miongoni mwa mambo tunayoenda kufanya ni suala zima la ujenzi wa vituo vya afya na hospitali katika maeneo mbalimbali. Nina uhakika Sengerema waliweka jambo hili kama *priority* yao katika mpango wa Halmashauri basi halina shaka tutashirikiana na ofisi yetu ya TAMISEMI lengo kubwa ikiwa ni wananchi kupata huduma ya afya.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kapufi.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba niishukuru Serikali kule Katavi tuliweza kupatiwa kituo hiki cha *MSD* kwa msaada wa Mheshimiwa

Waziri Mkuu, lakini mita chache kutoka kilipojengwa kituo hicho kipo Chuo cha Matabibu.

MWENYEKITI: Swali sasa.

MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, ni lini Serikali itatusaidia kuhakikisha chuo hicho kimeanza kazi kwa sababu ukarabati ushafanyika kwa asilimia 99?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni lini, sina hakika sana lini tunaweza tukawa tumekamilisha lakini chuo hiki ni katika vyuo vinne ambavyo tumevipa kipaumbele cha kufanyiwa ukarabati na kufanyiwa maboresho ili kuweza kutusaidia katika mpango wetu wa kuendeleza na kuzalisha rasilimali watu kwenye sekta ya afya. Kwa msingi huo, ndiyo maana yeye mwenywewe anasema kimekamilika kwa asilimia 99; kwa hivyo kwa sasa hivi sina taarifa sahihi kwamba lini tutakifungua rasmi lakini naomba nifuatilie na baada ya hapo naweza nikamshirikisha kwenye uvumbuzi wa majibu nitakayokuwa nimeyapata kutoka kwa watendaji wa Wizara yetu.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Selasini.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niipongeze Serikali kwa mkakati wake wa kusambaza maduka ya dawa sehemu mbalimbali za nchi na nimpongeze Waziri wa Afya na Naibu wake kwa kazi nzuri ya kusimamia maduka haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu, kumekuwa na kauli ya kuwatia matumaini wazee kwamba wataendelea kupata tiba bure, lakini wazee wengi katika nchi hii hasa wazee wa Jimbo langu la Rombo bado kero ya matibabu ni kubwa sana kwao.

Ni lini Serikali basi itamaliza kero hii ili wazee waliotumikia nchi hii kwa shida sana waweze walau kumaliza maisha yao hapa duniani wakiwa na matumaini kwamba wanapendwa na Serikali pamoja na wananchi ambao wamekuwa wakiwahudumia miaka yao yote?

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa amekuelewa. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi tu nimshukuru Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo kwa swali lake kuhusu wazee na nimhakikishie tu kwamba Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa mara ya kwanza inaweka *commitment* kubwa sana kwenye masuala yote yanayohusu mambo ya wazee na ndio maana katika ngazi ya kitaifa Mheshimiwa Rais mwenyewe ametengeneza Wizara ndani yake ameweka mahsus *portfolio* inayohusu mambo ya wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo la wazee tuna vipaumbele sana sana cha kwanza ikiwa ni kwenye eneo hili la afya ambapo tunashukuru kwamba Sera ya Afya ya mwaka 2007 inatoa msamaha wa matibabu kwa wazee wote wenye miaka 60 (ambao hawana uwezo). Ili kutekeleza hilo, nakubali kumekuwa na changamoto kadhaa lakini kwa sasa tumeweka utaratibu wa kuzitaka Halmashauri zote ziweze kuwakatia kadi ya *CHF* wazee kuanzia mwezi wa 12. Kwa hiyo, Halmashauri zimeanza *ku-respond* na nikuombe na wewe kwenye Halmashauri yako uhamasishe wenzako kwenye Baraza lenu muweze kuwakatia kadi za *CHF* wazee ili waondokane na adha hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mkakati huo, tumesema mzee kwanza na wazee wenyewe wanafurahi sana, juzi nimetoka kwenye mkutano wa wazee wanafurahi sana kwamba Serikali hii inawapa kipaumbele na kweli hospitali zote nchi zimeweka kibao kwamba mzee apite kabla ya mtu mwingine na hilo linatekelezeka. Kwa hiyo, tuendelee tu kwa pamoja kutekeleza mikakati hii.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na swali Na.310 linaulizwa na Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu.

Na. 310

Kushuka kwa Bei ya Zao la Mbaazi

MHE. QAMBALO W. QULWI aliuliza:-

Miaka ya karibuni zao la mbaazi limechangia kipato kwa wakulima baada ya kupata bei nzuri katika masoko. Katika msimu wa 2016/2017 bei ya zao hili ilishuka hadi kufikia shilingi 900 kwa kilo moja ukilinganisha na bei ya shilingi 2,800 kwa kilo moja kwa msimu wa 2015/2016.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaunganisha wakulima wa zao hilo na masoko yaliyoko ndani na nje ya nchi ili waweze kupata bei nzuri?

(b) Wapo wanunuzi wa zao hilo, mathalani Kampuni ya *Kilimo Market* wanachukua mazao ya wananchi na kuchelewa kuwalipa fedha zao. Je, ni nini kauli ya Serikali dhidi ya makampuni ya namna hiyo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Qambalo Willy Qulwi, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mbaazi iliporomoka katika msimu wa 2016/2017 katika maeneo mbalimbali nchini kutokana na ongezeko la uzalishaji wa zao hilo katika nchi za China, Brazil, Myanmar, Canada, Msumbiji na Sudan kuliko mahitaji ukilinganishwa na msimu wa mwaka 2015/2016. Ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata soko la uhakika la mbaazi, Serikali kuititia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko iliandaa Mkataba wa

Makubaliano (*Memorandum of Understanding – MOU*) na Serikali ya India ambao ndiyo wanunuzi wakubwa wa mazao ya jamii ya mikunde hapa nchini ili kuweka mfumo rasmi wa soko la mazao ya jamii ya mikunde hapa nchini. Mkataba huo ulipelekwa India ambako kwa mujibu wa Ubalozi wa India nchini bado wanaufanya kazi kabla ya kusainiwa na pande zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hatua zinazochukuliwa za kuuza mbaazi nchini India, Serikali inaangalia uwezekano wa kuanzisha mfumo wa Stakabadhi Ghalani ambao umeleta matokeo mazuri kwa zao la korosho ili pia utumike kwa zao la mbaazi. Ili mfumo ho utumike ipasavyo na kwa ufanisi, Serikali itawahamasisha wakulima kujiunga katika vyama vyaya ushirika kwenye maeneo yao na pia kuwa na utaratibu wa kupanga bei elekezi yenye kuzingatia gharama zote za uzalishaji kama ilivyo kwa zao la korosho.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la wanunuzi kuchukua mazao ya wananchi na kuchelewa kuwalipa fedha zao, Serikali itaendelea kutoa maelekezo na kuhakikisha kuwa wanunuzi wote wa mazao nchini wanawalipa wananchi fedha zao mapema iwezakanavyo mara tu wanamuapo mazao hayo. Hata hivyo, mfumo rasmi wa soko la mazao ya jamii ya kunde ambao utakuwa chini ya usimamizi wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko utaziba mianya ya wanunuzi holela hivyo kupusha udanganyifu wakati wa kununua mazao ya jamii ya kunde ikiwa ni pamoa na mbaazi kutoka kwa wakulima.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Qulwi, swali la nyongeza.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, mbaazi inayolimwa Tanzania bado ina uwezo wa kuingia katika soko

lililoko India kutohana na viwango vya ubora ambayo inayo. Nashukuru kwamba Serikali imesema imeandaa makubaliano na mkataba umesainiwa wa kuwasaidia wananchi wetu waendelee kupata bei nzuri.

Je, Serikali iko tayari sasa kusukuma majadiliano hayo ili wananchi wetu waweze kunufaika kuanzia msimu wa kilimo ambao unaendelea sasa hivi baada ya kuvuna?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa biashara ya kuuza mbaazi nje ndiyo hiyo ambayo sasa haitabiliiki. Je, Wizara hii iko tayari sasa kuanza mazungumzo na Wizara ya Viwanda na Biashara ili kupata viwanda vya kusindika zao hilo tuweze kuuza nje bidhaa iliyosindikwa ili kuongeza thamani na pia kutoa ajira kwa watu wetu? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kufuatilia mkataba na Serikali ya India ili utekelezaji wake uweze kuanza kazi mapema iwezekanavyo ili wakulima wetu waendelee kunufaika bila kuchelewa.

Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunalisukuma, lakini wanaochelewesha kwa sasa siyo sisi ni upande wa India, wao wanaangalia mazingira ya hapa kwetu kwa sababu wameongea na nchi zingine za Kenya na Msumbiji, kimsingi wanajaribu kuangalia *options* mbalimbali, lakini sisi tutaendelea kuongea nao ili kufanikisha huo mkataba ili uanze mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli kabisa kati ya mikakati tuliyonayo ya kuweza kutafuta soko zuri la mbaazi na mazao mengine ya jamii ya mikunde ni kuwa na viwanda vya kuchakata hapa ndani ili tuweze kushindana katika soko la Kimataifa. India yenyewe ambayo ndiyo

mnunuzi wa asilimia 27 ya mbaazi na mazao ya mikunde duniani wanauzu katika nchi zingine baada ya kuchakata. Kwa hiyo, nasi tukiwa na viwanda itatusaidia sana tuweze kupata masoko mengine ikiwepo na masoko mazuri kama ya Marekani na Ulaya. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari hiyo ni moja katи ya mikakati ambayo tunafikiria kama Serikali.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Mheshimiwa Gekul.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kwenye taarifa ya habari *ITV* kulla kuwa kuna kauli kwamba kuna uingizaji wa mbegu *fake* nchini. Kama kauli hii ina ukweli ni hatari sana kwani inamdhulumu mkulima ananunua mbegu akidhani ni mbegu yenye ubora lakini mbegu hii inakuwa ni feki matokeo yake anapanda havuni anachokitegemea.

Je, ni nini kauli ya Serikali kuhusu kauli hii ambayo ilitoka *ITV* jana usiku kwenye taarifa ya habari? Nashukuru.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. Tizeba, majibu.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, hata mimi nimeiona hiyo kauli au *statement* iliyotolewa na kituo cha televisheni cha *ITV* kwamba nilikiri nchini hapa mbegu inayotumika kwa wakulima ni mbegu *fake*. Naomba nitoe ufanuzi wa hilo jambo kwamba sikusema hivyo na jambo hilo lilitangazwa halina ukweli wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokisema ni kwamba wakulima wengi nchini bado wanatumia mbegu hafifu na kwa hivyo uzalishaji wao bado uko duni kwa sababu ya matumizi ya mbegu hizo na si kusema kwamba wanatumia

mbegu feki. Kwa hivyo, niwaombe tu wenzetu wa kituo hicho cha televisheni wafanye hayo marekebisho ya kauli yangu. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kusema kwamba Serikali inachokisema ni kwamba bado yako matumizi ya mbegu hafifu kwa wingi hapa nchini na hiyo inatusababishia uzalishaji hafifu na si vingineyo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Gekul.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mko wa Manyara kwa ujumla wake unazalisha sana zao la mbaazi hususan katika Jimbo langu kata ya Singe, kata nzima na mnapita barabarani pale kama mnaenda Arusha ni mbaazi na imestawi. Hata hivyo, kwa kuwa hakuna viwanda vinavyochakata zao hili na Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri na kwa kuwa bei hii imekuwa ikishuka kila mwaka, wananchi wetu wamekuwa wakipata hasara.

Je, Serikali haioni kwamba ni vizuri wakanunua zao hili wao kama wanavyofanya kwa zao la mahindi kwa *NFRA* ili wao watafute soko badala ya wananchi wetu kuendelea kupata hasara maana hata viwanda havijaanza sasa kutekeleza?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kwa sasa bado hatuna viwanda vyta kuchakata siyo zao la mbaazi tu lakini mazao mengi yakiwepo mazao mengine ya jamii ya mikunde kama njegele, dengu, choroko na lentili na hiyo inaleta changamoto katika upatikanaji wa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwa sasa Serikali haina mpango wa kununua zao hilo kutoka kwa wakulima, lakini tunachofanya ni kujaribu kwenda kule kwenye soko lenyewe India na ndiyo maana tayari tumeshaingia mkataba wa awali ili wananchi wetu waweze kuuza kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, soko la India kwa sasa hata kama tukifanikiwa kupata tatizo litakuwa ni sisi kuweza kuzalisha kiwango ambacho wanahitaji. India kimsingi wana mahitaji makubwa na ndiyo maana tunafikiri njia sahihi na njia ambayo itawakomboa wakulima ni kutafuta hilo soko pamoja na kwamba kama tulivyosema tutaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vyta kuchakata mazao mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niseme kwamba changamoto nydingine iliyopo katika uuzaaji wa mbaazi na mazao mengine ni mfumo wetu wa soko. Nimshauri Mheshimia Mbunge pamoja na Wabunge wengine wahamasishe wakulima waanzishe vyama vyta ushirika kwa sababu ni mfumo ambao utawasaidia kuuza kwa pamoja na kwa urahisi zaidi.

MWENYEKITI: Waheshimiwa, naomba majibu yawe mafupi tu, Mheshimiwa Zuberi.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo kwenye matatizo ya mazao ya mbaazi vivyo hivyo kuna tatizo la zao la ufuta, lakini tatizo kubwa la mazao haya ni Bodi ya Mazao Mchanganyiko. Ni nini kauli ya Serikali katika kuiboresha hii Bodi ya Mazao Mchanganyiko iwe na mipango endelevu ya kuendeleza haya mazao ili wananchi wetu waweze kupata soko la uhakika?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini mtaiboresha hiyo Bodi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wizara na Serikali inaendelea na mikakati ya kuiboresha Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Changamoto iliyopo kwa sasa ni namna gani tunaweza tukaanzisha utaratibu wa kusimamia mazao mengi

ambayo hayana mfumo wa kuyasimamiwa. Kwa hiyo, kwa sasa Bodi inaendelea na mchakato wa kuangalia namna gani ya kuweza kusimamia kila zao kwa utaratibu wake kama ilivyo kwenye mazao mengine ya biashara. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali inafahamu hilo na linafanyiwa kazi, Bodi inajitayarisha kuangalia namna ya kusimamia siyo zao la ufuta tu lakini vilevile mazao mengine.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Swalii Na.311 linaulizwa na Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge wa Pangani.

Na. 311

Mitaji na Vitendea kazi kwa Wavuvi wa Pangani

MHE. JUMAA H. AWESO aliuliza:-

Licha ya Wilaya ya Pangani kubarikiwa kuwa na Bahari ya Hindi lakini wavuvi wa Pangani hawajanufaika ipasavyo na bahari hiyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wavuvi wa Pangani mitaji na vitendea kazi?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa sekta ya uvuvi nchini kwa kutekeleza mikakati yenyeh lengo la kuendeleza uvuvi nchini wakiwemo wavuvi wa Wilaya ya Pangani ili waweze kupata ajira, lishe, kipato na kuchangia katika pato la Taifa. Miiongoni mwa mikakati hiyo, ni pamoja na kuondoa kodi katika zana za malighafi za uvuvi zikiwemo injini za kupachika, nyuzi za

kushonea nyavu (*twines*) na vifungashio. Kodi hizo zimeondolewa kuititia Sheria ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 2014. Vilevile kuititia *East Africa Publication on Common External Tariff*, injini za uvuvi na malighafi zinazotumika kutengeneza zana mbalimbali za uvuvi na viambata vyake zimepewa punguzo la kodi ili kuwezesha wavuvi kumudu bei za vifaa hivyo. Pia Serikali inatoa ruzuku kwenye zana za uvuvi ambapo mvuvi anatakiwa kuchangia asilimia 60 na Serikali asilimia 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pangani ni eneo la kimkakati katika masuala ya uvuvi na hasa uvuvi wa dagaa katika vijiji vya Kipumbwi na Pangani Mashariki na uvuvi wa pweza katika kijiji cha Ushongo. Serikali imewawezesha wavuvi wa Pangani kwa kuwapatia mafunzo ya kuongeza thamani na uvuvi endelevu wa pweza. Katika mwaka 2017/2018 kuititia Halmashauri ya Wilaya ya Pangani, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 20 kwa ajili ya ujenzi wa soko la samaki ambapo fedha imeshapelekwa katika akaunti ya Kata ya Pangani Mashariki ili ujenzi uanze mara moja. Kukamilika kwa ujenzi wa soko hilo kutawanufaisha wavuvi wa Pangani na hivyo kupata mtaji na vitendea kazi katika shughuli za uvuvi. Natoa wito kwa Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Madiwani wa Pangani kufuatilia na kusimamia ipasavyo matumizi ya fedha hizi ili lengo la Serikali la kuwawezesha wavuvi wa Pangani liweze kutimia. Vilevile Mheshimiwa Mbunge aendelee kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani na wananchi kupiga vita vitendo vya uvuvi haramu wa kutumia mabomu na hivyo kuhatarisha uendelevu wa rasilimali hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuititia Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (*SWIOFish*) imeendelea kutoa mafunzo ya uvuvi endelevu kwa wavuvi ambapo katika Halmashauri ya Pangani, *BMUs* tatu za Pangani Mashariki, Pangani Magharibi na Boza zimenufaika na mafunzo hayo. Katika mwaka 2017/2018 Serikali itaendelea kutoa mafunzo kwa *BMUs* zilizobaki za Bweni, Ushongo Sahabu, Kipumbwi, Sange, Mikocheni, Mkwaja na Buyuni ambazo ziko ng'ambo ya Mto

Pangani. Pia, Halmashauri ya Pangani imetoa uwakala kwa BMUs nne kati ya 11 za Wilaya ya Pangani kukusanya mapato ya uvuvi ambapo asilimia 10 ya mapato hayo wanapewa BMUs. Fedha hiyo ikitumika vizuri inaweza kuwapatia wavuvi wa Pangani mitaji na vitendea kazi.

MWENYEKITI: Jibu lenyewe refu sana, Mheshimiwa Aweso.

MHE. JUMAA H. AWESO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru Serikali kwa kuondoa kodi katika zana hizi za uvuvi. Kitu ambacho nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri pamoja na kuondoa kodi na kuleta tozo kwa asilimia 40 kwa wavuvi wa Pangani lakini Serikali haikuwa wazi ni namna gani au utaratibu gani ambao unatakiwa uflatwe na vifaa hivi vinapatikana wapi ili wavuvi hawa hususani wa dagaa waweze kupata zana hizo kwa ukaribu na rahisi?.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, nataka nimuulize Mheshimiwa Waziri Serikali ina mkakati gani wa kujenga bandari ya uvuvi hususani katika ukanda huu wa Pwani ya Mkao wa Tanga kwa mantiki ya meli kubwa zinazovua bahari kuu kwa maana ya kuhaulisha, kuuza na kutoa takwimu sahihi kuhusu suala zima la uvuvi? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na utaratibu unaotakiwa kufuatwa ili wavuvi waweze kupata punguzo katika zana za uvuvi, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kimsingi wavuvi wake wanaotaka kupata ruzuku ya vyombo vya uvuvi wanatakiwa wajunge katika vikundi, lakini vilevile wachangishane fedha, wakishakuwa na fedha ya kununua kwa mfano injini ya boti wanawasilisha maombi yao Halmashauri ambao watawaelekeza namna ya kupata zile zana halafu Serikali itachukua asilimia 40 ya gharama ya chombo ambacho wanataka kununua. Mheshimiwa Aweso kwa sababu ni Mbunge kijana ambaye amekuwa

akihangaikia sana wananchi wake kwa muda mrefu sana, nimuahidi tu kwamba kama anataka kupata ufanuzi mzuri zaidi hata leo mchana anaweza akaja ofisini kwangu tukaongea ili wananchi wake wasiendelee kuchelewa kupata huduma hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bandari ya uvuvi, wakati tunawasilisha bajeti yetu tulitoa maelezo marefu sana kuhusiana na mikakati mbalimbali ambayo kama Serikali tumeweka ili kuendelea kuboresha namna ya nchi kunufaika na uvuvi katika bahari kuu. Moja ya mikakati hiyo ambayo tulisema ni pamoja na kuanza na mchakato wa kujenga bandari ya uvuvi. Katika bajeti ya mwaka unaokuja, Wizara imetenga fedha za kufanya upembezi yakinifu ili tuweze kujua ni mahali gani hasa ambapo panafaa kuweka bandari ya uvuvi. Bandari ya uvuvi yenyewe gharama za awali ambazo tumekadiria tunafikiri inaweza ikagharimu zaldi ya...

MWENYEKITI: Imetosha Mheshimiwa. Mheshimiwa Mlinga, Mheshimiwa Catherine Ruge, niangalie na Muungano Mheshimiwa mtaalam wa misitu na Mheshimiwa Mbarouk. Tunaanza na Mheshimiwa Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jimbo langu la Ulanga tumebahatika kuwa na mto mkubwa sana, Mto wa Kilombero lakini wananchi wanaoisha maeneo yale hawajawahi kunufaika na chochote kile kuhusu uvuvi.

Je, sasa Wizara iko tayari kutoa ushauri wa kitaalam na vifaa ili wananchi wanaoishi karibu na mto ule wanufaiki na shughuli za uvuvi na Serikali ipate mapato? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara na Serikali iko tayari kuwasaidia wananchi wake waweze kuvua katika Mto Kilombero. Nimhakikishie tu kwamba huduma hii inapatikana

katika Halmashauri ambapo yeye mwenyewe ni Diwani na vilevile niwashauri Waheshimiwa Wabunge wote kwamba huduma za namna ya kuwasaidia wananchi katika sekta ya uvuvi na sekta zote za Wizara yangu yaani kilimo na mifugo, sehemu nzuri ya kuanzia ni kwenye Halmashauri na sisi wenyewe tunashiriki lakini kama nilivyosema kwa Mheshimiwa Aweso, hata Mheshimiwa Mlinga anaweza akaja nikamuelekeza zaidi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Catherine Ruge.

MHE. CATHERINE N. RUGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la uvuvi haramu kwa kutumia nyavu zenye matundu madogo na baruti limekuwa la muda mrefu kwenye Ziwa Victoria, lakini pia maziwa mengine hapa nchini. Ni nini mpango wa Serikali kuwekeza kwenye vizimba (*fish cadge*) njia ambayo ni salama na yenye ufanisi ili kuwawezesha vijana wa Kanda ya Ziwa kuendelea kujajiri katika sekta ya uvuvi? Ahsante. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba katika Ziwa Victoria hakuna uvuvi wa mabomu, uvuvi uliopo ni uvuvi wa kutumia zana ambazo hazijaruhusiwa kutumia makokoro na zana zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi Serikali inaendelea kutoa elimu kwa wavuvi ili waachane kabisa na uvuvi ambao sio endelevu na katika hili tunahakikisha kwamba tunashirikiana na Halmashauri na vilevile Mheshimiwa Mbunge tunaomba na yeye atusaidie ili kuendelea kuhamasisha wavuvi wa kule anakotoka ile wafanye uvuvi ambao unaendana na taratibu za sheria.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mbarouk.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na Serikali kuondoa baadhi ya kodi katika sekta ya uvuvi na villevile kujenga Soko la Kisasa la Samaki Pangani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuuliza Mheshimiwa Waziri, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha Uvuvi katika Mkoa wa Tanga kama kile kilichopo Mwanza?

MWENYEKITI: Ahsante. Lini mtajenga chuo hicho kama kile cha Mwanza?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa chuo anachosema, Serikali itafikiria ombi lake kulingana na uwezo wa kibajeti lakini kwa sasa tunaendelea kuimarisha vyuo viliwyopo vya VETA ili kuweza kuendelea kutoa huduma hata wakati huko mbele tunafikiria kujenga vyuo vingine kadri uwezo utakavyoruhusu.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Swali Na. 312 linaulizwa na Mheshimiwa Zitto Zuberi Ruyagwa Kabwe, Mbunge wa Kigoma MJINI na linaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Bilago.

Na. 312

SUMATRA Kutoa Vibali vya Usafiri kwa Wavuvi – Ziwa Tanganyika

MHE. KASUKU S. BILAGO (K.n.y. MHE. ZITTO Z. R. KABWE)
aliuliza:-

Mamlaka ya Usimamizi wa Usafirishaji wa Ardhini na Majini (*SUMATRA*) hutoa vibali vya usafiri kwa wavuvi wa Ziwa Tanganyika.

(a) Je, ni kifungu gani cha sheria kinaipa mamlaka *SUMATRA* kutoza ushuru kwa wavuvi na wakati huo huo haifanyi hivyo kwa matrekta kwenye kilimo?

(b) Je, Serikali haioni kuwa inadidimiza wavuvi kwa kuwarundikia tozo nyingi na kuwafanya waendelee kuwa maskini?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zitto Zuberi Ruyagwa Kabwe, Mbunge wa Kigoma Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (*SUMATRA*) haitoi vibali wala haitozi ushuru kwa vyombo vya usafiri majini nchini ikiwa ni pamoja na wavuvi wa Ziwa Tanganyika, ila kwa mujibu wa Sehemu ya III, Kanuni ya 18 ya Kanuni za Sheria, zinazoitwa: *The Merchant Shipping (Small Ships, Local Cargo Ship Safety, Small Ships Safety, Survey and Inspection for Vessels engaged on Local and Coastal Voyages Inland Waters) Regulations 2006, GN. 106, SUMATRA* inalo jukumu la kukagua ubora wa vyombo vya usafiri majini kwa pamoja na vya uvuvi na kutoa Cheti cha Ubora (*Seaworthiness Certificate*) na usajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu ya msingi ya *SUMATRA* katika vyombo vya usafiri majini na vya uvuvi ni kuhakikisha kuwa vyombo hivyo ni salama kabla havijaanza kutoa huduma au kufanya shughuli za majini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, *SUMATRA* inapokagua vyombo vya usafiri majini kwa mujibu wa Sehemu ya II, Kanuni ya 9 ya Kanuni za Sheria, zinazoitwa: (*The Merchant Shipping (Fees) Regulations, 2005*), wenyewe vyombo vya usafiri majini ikiwa ni pamoja na vya uvuvi hutakiwa kulipa ada ya ukaguzi kwa *SUMATRA* kwa ajili ya ukaguzi uliofanyika. Hivyo, Serikali haikusudii kudidimiza wavuvi wala haijawarundikia tozo nyingi ambazo zitawafanya wawe masikini bali inawahakikishia wavuvi hao mazingira salama kwa ajili ya kufanya shughuli zao za uvuvi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bilago.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu aliyotoa kwa swali hili, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, wavuvi wa Ziwa Tanganyika katika Manispaa ya Kigoma Ujiji maisha yao yote yanategemea uvuvi na vyombo vile kama mitumbwi inatumika kwa ajili ya uvuvi siyo kusafirisha abiria. Sasa ni lini Serikali itaondoa tozo hii ili kuondoa manyanyaso kwa wavuvi wa Kigoma Ujiji?

Swali la pili, sambamba na vyombo vya majini, bodaboda walioko Wilaya ya Kakonko na Wilaya zingine hapa nchini nao wanatozwa *SUMATRA*. *SUMATRA* ya bodaboda ni shilingi 22,000 sawa na kiti kimoja mwenye basi angelipa kwa kiti basi lenye abiria...

MWENYEKITI: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti ndio nakuja. Basi lenye abiria 60 lingelipa shilingi 1,320,000. Ni lini sasa Serikali itaondoa tozo ya *SUMATRA* kwa bodaboda katika Wilaya ya Kakonko na Wilaya zingine nchini? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Dkt. Ngonyani majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali yote mawili kwa pamoja kwamba kimsingi hatutozi tozo kama ambavyo nilisema katika jibu la msingi, kinachotozwa na *SUMATRA* ni ada ya ukaguzi. *SUMATRA* wanahitajika kukagua iwe hizo meli au hizo boti zinazotumika kwenye uvuvi au pikipiki zote hizi zinatakiwa zikaguliwe ili tuwe na uhakika zinapotoa huduma au zinapofanya shughuli za uvuvi zipo salama. Sasa kazi hiyo inayofanywa na *SUMATRA* inahitaji kulipiwa ada kidogo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Msabaha.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika Ziwa Tanganyika kumekuwa na tatizo la wavuvi wengi kuvamiwa hasa kutoka nchi za jirani kama Congo, wale wavuvi wamekuwa wakipata shida sana. Je, Serikali imejipangaje kuhakikisha hawa wavuvi wanaotoka upande wa Kigoma nao angalau wanaridhika na rasilimali zao na kutokunyanyaswa na raia ambao wanatoka Congo na nchi jirani za Burundi? (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu mojawapo ya kufanya ukaguzi ni pamoja na kuvisajili vyombo hivyo ili vipate uraia kwa sababu mara nyingi vyombo hivi vinapotumika kwenye maji siyo rahisi kujua hapa umevuka mpaka au hapa uko ndani ya nchi yako. Kwa hiyo, usajili wa vyombo hivi ni muhimu sana na vikishasajiliwa vinatambulika kwamba hiki ni chombo cha Tanzania, hiki chombo cha Burundi, hiki chombo cha DRC tunapokutana katika maeneo yale ya Ziwa Tanganyika. Hiyo ndiyo silaha pekee ya kuiwezesha nchi yetu, kwanza wale maadui kutambua kwamba wanamgusa raia wa Tanzania na hivyo Serikali ya Tanzania inaweza kuwa tayari kumtetea mtu huyo. Kwa hiyo, njia mojawapo ya utetezi ni hiyo ya kuvisajili vyombo hivyo na tukiishavisajili tunafanya shughuli za doria mara kwa mara katika ziwa lile na nadhani Mheshimiwa Mbunge atakuwa amewahi kuona matokeo mazuri ya doria zinazofanywa katika Ziwa Tangayika katika kuhakikisha kwamba wavuvi wa Tanzania wanakuwa salama.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaedelea na Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, swali namba 313.

Na. 313

Hitaji la Kisheria la Uraia wa Nchi Mbili

MHE. KHATIB SAID HAJI aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiwataka Watanzania waliopo nje ya nchi kuwekeza katika miradi ya maendeleo nchini ili kusaidia kukuza uchumi wetu na hatimaye kuongeza ajira kwa Watanzania.

Je, kwa nini Serikali inashindwa kuweka Sheria ya Uraia wa Nchi Mbili ili iwe rahisi kwa Watanzania hao kuitikia wito huo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kupitia Idara ya Diaspora na Balozi zetu nje ya nchi zina utaratibu wa kuwatambua na kuwahamasisha diaspora wenye ujuzi wa taaluma mbalimbali kuja kuwekeza kwa wingi nchini kupitia sekta ya kiuchumi, kuleta ujuzi, elimu na utaalamu wanaoupata huko ughabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya uraia wa Tanzania yanasmamiwa na Sheria ya Uraia Namba 6 ya mwaka 1995 ambayo imebainisha kuwa uraia wa Tanzania upo katika makundi matatu, uraia wa kuzaliwa, uraia wa kurithi na uraia wa tajinisi. Aidha, sheria hii kupitia kifungu cha 7(4)(a)(b) kimeeleza bayana kuwa raia wa Tanzania anaacha kuwa raia kwa kigezo cha kuchukua uraia wa nchi nyingine. Hivyo basi, kutokana na sheria hii na sera ya Tanzania kuhusu uraia ambayo hairuhusu wala kutambua uraia wa

nchi mbili, Serikali haiwezi kuweka sheria ya uraia pacha kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili lilijadiliwa pia wakati wa mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, Bunge Maalum la Katiba ambalo lilijadili pendekezo hili liliono Tanzania bado haipo tayari kwa sasa na Bunge hilo Maalum likatoa pendekezo kwamba; "Mtu yejote mwenye asili au nasaba ya Tanzania na ambaye ameacha kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupata uraia wa nchi nyiningine atakapokuwa katika Jamhuri ya Muungano atakuwa na hadhi maalum kama itakavyoainishwa katika sheria za nchi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nukuu hii imebainishwa katika Sura ya 6, Ibara ya 72 ya Katiba Inayopendekezwa ya Oktoba, 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mchakato wa kupata Katiba Mpya bado haujakamilika, namuomba sana Mheshimiwa Mbunge avute subira ili mchakato huo uishe.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Haji.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kwanza Mheshimiwa Waziri anaposema kwamba mchakato wa Katiba Mpya haujakamilika anakwenda kinyume na dhana ya Mheshimiwa Rais ambapo amesema Katiba Mpya siyo kipaumbele chake.

MWENYEKITI: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza swali sasa. Swali la kwanza, kwa kuwa Tanzania siyo kisiwa na tumeona nchi nyiningi zimefaidika kwa kuwatumia raia wake walioko nje kwa kuwapatia hadhi ya kuwa na uraia wa nchi mbili.

Je, Serikali haioni kwamba tunapoteza fursa muhimu ambazo tunazipigania kwa raia wetu walioko nje ya nchi kuwa na uraia wa nchi yao ili waweze kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa Taifa hili? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Waziri amenijibu akisema kwamba Watanzania wenyenye nasaba watapewa hadhi maalum itakayowatambua lakini hivi karibuni zimetolewa kauli tata na Serikali za kuwavunja moyo na kuwatisha Watanzania walioko nje ya nchi kuhusu umiliki wa mali katika nchi yao ya Tanzania ikiwemo tishio la kuwanyang'anya ardhi na nyumba zao.

Je, Serikali haioni kwamba iko haja ya kuwatoa hofu na wasiwasi huu uliotokana na kauli iliyotolewa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi? Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi tu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kusema kwamba hatuzioni faida zinazoletwa na Diaspora wetu kama tutabdalilisha na kuwapa uraia wa nchi mbili, sisi tunasema kwamba hawa watu kwanza hawapotezi haki yoyote. Kama tu watu ambao siyo raia wa Tanzania wanaruhusiwa kuwekeza Tanzania na kwa vile pia kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi sheria hairuhusu lakini bado watu hawa wanawekeza na ndiyo maana sisi kama Wizara tunawahamasisha na tutaendelea kuwahamasisha na kuwajulisha fursa mbalimbali tulizonazo katika nchi hii ili watumie fursa hizo kwa faida yao na familia zao hapa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba hivi karibuni Serikali au Tanzania imewavunja moyo wale Diaspora walioko nje kwa kuwanyang'anya ardhi, nafikiri nimeshasema na sheria zinasema wazi mwenye kuweza kumiliki ardhi Tanzania ni Mtanzania, ni raia wa Tanzania kwa

sheria zilizoko hapa nchini lakini hawanyang'anywi ardhi kama wao ni raia wa Tanzania. Wako raia wa Tanzania ambao wanaishi nje ya nchi hii wanamiliki ardhi na wanaruhusiwa kuwekeza kama raia wengine wowote.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Swali Na.314 linaulizwa na Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa.

Na. 314

Miradi ya Makaa ya Mawe - Mchuchuma na Liganga

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA aliuliza:-

Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Liganga imekuwa ikiwекwa katika mipango ya Serikali katika Awamu karibu zote nne zilizopita, hata Awamu hii ya Tano bado miradi hii imewekwa.

(a) Je, ni lini wananchi walioachia maeneo yao ili kupisha miradi hii watalipwa fidia yao?

(b) Je, ni lini miradi hii itaanza kazi?

(c) Je, ni kweli Serikali imejipanga kuhakikisha miradi hii inaanza?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Mchuchuma na Liganga umeainishwa katika Dira ya Taifa 2025; Mkakati wa Fungamanisho la Maendeleo ya Viwanda 2015; Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016-2021) na Ilani ya Chama

cha Mapinduzi ya 2015 - 2020. Ni majukumu na wajibu wa Serikali kutekeleza maamuzi na maelekezo yaliyorejewa hapo juu. Ni kweli, Serikali imejipanga kuhakikisha miradi hii inaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naelewa tatizo la Mheshimiwa Mbunge ni kuchelewa kuanza kwa mradi na hasa malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha mradi. Kuchelewa kuanza kwa mradi kumetokana na nia nzuri ya Serikali ya kutaka kuhakikisha miradi inatekelezwa na wakati huo huo Taifa linapata manufaa stahiki kutokana na uwekezaji huo. Timu ya wataalamu imekamilisha kazi ya kupitia vipengele vyote vya vivutio na kuwasilisha taarifa yao Kamati ya Kitifa ya Uwekezaji (*NISC*). Kamati hiyo imetoa maelekezo kwa timu ya wataalam kujadiliana na mwekezaji maeneo yenye mvutano. Ni imani yangu kuwa baada ya makubaliano kwenye maeneo hayo machache yaliyobaki, vikao husika vitatoa baraka za mwisho na mradi utaanza mara moja ikiwemo kulipa fidia kwa watu waliopisha mradi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Deo Ngalawa, maswali ya nyongeza.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, tarehe 19 Aprili, 2016 niliuliza swali hili hili katika Bunge hili hili. Bunge lilielezwa kwamba fidia ingeweza kulipwa Juni, 2016 na mradi kuanza Machi, 2017. Je, tushike kauli ipi kati ya haya majibu mawili? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa mwekezaji tayari anayo hela, yuko tayari kulipa, kwa nini Serikali isichukue jukumu la kulipa fidia ili wale wananchi wale waendelee na shughuli zao nyingine za kiuchumi halafu mwisho Serikali itakapokuwa tayari ije ichukue kwa mwekezaji hiyo hela ambayo tayari anayo sasa hivi?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji majibu, anasema majibu ya uhakika sasa.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ametaka kujua achukue kauli ipi ya Serikali kati ya jibu nililompa tarehe 19 Aprili na hili ninalompa leo. Katika jibu langu nimeeleza kwamba Serikali imechukua hatua ya kupitia makubaliano na mwekezaji ili kuhakikisha kwamba uwekezaji unaowekezwa unakuwa na manufaa kwa Watanzania na kwa mwekezaji. Mheshimiwa Ngalawa huo ndiyo mchezo wa siku hizi, Serikali itahakiki kuhakikisha uwekezaji unaowekezwa unaleta tija kwa mwekezaji na kwa Watanzania. Naogopa usije ukadirudia mwaka 2030 nikiwa Mbunge niko hapa Waziri ukaniuliza mbona mmeacha mashimo Ludewa, nitashindwa kukujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kulipa fidia Serikali, nina imani hii timu yangu inayofanya kazi, nayoisimamia mimi mwenyewe, hatuondoki hapa Bungeni bila kukubaliana. Wawekezaji wako Dodoma, watendaji wangu wote wako Dodoma, mimi nawasimamia mwenyewe lazima tukubaliane Mchuchuma na Liganga ianze.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Swalii Namba 315 linaulizwa na Mheshimiwa Mwanne Ismail Mcchemba, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 315

Serikali kupeleka wawekezaji Mkao wa Tabora

MHE. MWANNE I. MCHEMBA aliuliza:-

Mkao wa Tabora upo tayari kwa ajili ya uwekezaji wa EPZ uliotengewa eneo katika Wilaya ya Uyui.

Je, ni lini Serikali italeta wawekezaji katika Mkao wa Tabora?

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kutenga eneo la uwekezaji Mkoa wa Tabora kwa ajili ya EPZA ulianza mwaka 2010 baada ya Wizara yangu kuelekeza uongozi wa Mkoa kutenga eneo lisilopungua ukubwa wa hekta 2000. Uongozi wa Mkoa ulipendekeza eneo ulipokuwa Mgodi wa Resolute lenye ukubwa wa hekta 866. Baada ya ukaguzi wa eneo hilo ilibainika kuwa sehemu kubwa ni mashimo yaliyofunikwa hivyo kutofaa kwa ajili ya miradi ya EPZA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa ushauri kwa Mkoa wa Tabora na kwa Mikoa mingine waendelee kubaini na kutenga maeneo ya uwekezaji. Watenge maeneo kwa malengo ya *Special Economic Zone - SEZ* au *Export Processing Zone - EPZ* kulingana na ushauri utakaotolewa na wataalamu wangu, lakini pia watenge maeneo kwa ajili ya uwekezaji usiokuwa wa *SEZ* wala wa *EPZA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelekezo ya hapojuu, Wizara yangu inakamilisha uandaaji wa mwongozo utakaosaidia Mamlaka za Mikoa na Wilaya kutenga maeneo ya uwekezaji na namna ya kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuleta wawekezaji Tabora, nitoe taarifa kuwa hivi sasa Mamlaka ya Biashara Tanzania (*Tan Trade*) kwa kushirkiana na Mkuu wa Mkoa wa Tabara wanaandaa kongamano la kutangaza vivutio vya Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Tabora kuwa Wizara na mimi mwenyewe tutaendelea kuitangaza Tabora kwa lengo la kuvutia wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwanne Mchemba.

MHE. MWANNE I. MCHEMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niulize maswali madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa Wilaya ya Uyui tayari ina eneo kubwa ambalo wawekezaji wanaweza wakalitumia. Je, Serikali iko tayari sasa kuwapeleka wataalam kuhakikisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa wawekezaji wengi hapa nchini hukiuka maandiko au mikataba wanayoingia na Serikali. Je, Serikali iko tayari sasa kuipitia upya ile mikataba na kuivunja kabisa mikataba ambayo wameingia hapa nchini kwa mfano Kiwanda cha Manonga na Kiwanda cha Nyuzi? Je, Serikali inasema nini? Je, Waziri yuko tayari sasa kwenda kuviona viwanda hivyo jinsi walivyoviharibu? Naomba majibu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi tu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Uyui, kwenye kongamano nililolisema ambalo analisimamia Mkuu wa Mkoa na Meneja wa *Tan Trade* na mimi nitakuwepo. Kwa hiyo, nitakwenda Uyui na wataalam tutaangalia hali itakavyokuwa na tutaweza kuwashauri namna ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si wawekezaji wote wanakiuka, mmoja anayekiuka umlete tutamshughulikia, ni *case by case*. Wawekezaji si wabaya, wawekezaji ni wazuri lakini yule anayekiuka tutamshughulikia kulingana na tukio lenyewe.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Khadija Nassir na Mheshimiwa Kubenea.

MHE. KADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa *T/C* ndiyo lango kuu la uwekezaji

nchini, je, *TIC* inaisaidiaje *EPZ* kwenye kutekeleza majukumu yake vizuri? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi zote hizi mbili ziko chini yangu, kwa Kiswahili cha kawaida *TIC ni receptionist, EPZ* ndiyo anaandaa kama ni ubwabwa kwenye meza. Kwa hiyo wote wanashirikiana, ni mkono na mdomo. *TIC ni receptionist*, ni mpiga *sound anakaribisha* watu, *EPZA* anaweza kuwatendea inavyobidi. (*Kicheko/Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika majibu yake ameeleza kwamba uwekezaji ni lazima uende pamoja na manufaa kwa wananchi waliopo katika eneo ambalo uwekezaji umefanyika. Katika Jimbo la Ubungo kuna maeneo ya *EPZ* yaliyopo eneo la *Ubungo External* na kuna Kiwanda cha Urafiki ambacho Serikali imekibinafsisha kwa mwekezaji wa nje. Maeneo hayo mawili hayana manufaa yoyote kwa wananchi wa Ubungo na eneo la *EPZ* lina migogoro mikubwa, wafanyakazi wanalipwa mishahara midogo...

MWENYEKITI: Mheshimiwa inaelewaka, ni swali moja tu.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itatatua matatizo ya *EPZ* yaliyoko katika Jimbo la Ubungo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msemo kwetu unasema mwenye shibe hamjui mwenye njaa. EPZA kuna viwanda vinaajiri vijana zaidi 3,000, mimi naomba kama kiwanda hicho kingehamia kwetu nikaajiri vijana 3,000. Urafiki inatoa ajira, inaweza kuwa na upungufu yale *specific* uyalete kwangu niyashughulikie. Wawekezaji wote ni wazuri yule aliye mbaya mumlete kwangu, lakini hao 1,800 na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu upande wa Ajira wanaajiri vijana 400 kila baada ya miezi minne. Narudia tena na sifichi ningeomba hao watu wangekuwa kwenye Jimbo langu naajiri vijana wangu 400 kila mwezi, usikufuru Mheshimiwa Kubenea.

MWENYEKITI: Ahsante tunaendelea na swali namba 316 linaulizwa na Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu, linaulizwa kwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

Na. 316

Tatizo la Maji Jimbo la Ulyankulu

MHE. JOHN P. KADUTU aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itaunganisha Jimbo la Ulyankulu katika miradi ya maji toka Ziwa Victoria na maji toka Mto Malagarasi?

(b) Je, Serikali iko tayari kuyakinga maji ya Mto Igombe ili kuwa na bwawa kubwa ambalo litapunguza shida ya maji?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Injinia Isack Kwamwelwe.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Peter Kadutu, Mbunge wa Ulyankulu, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshaanza utekelezaji wa mradi kutoa maji kutoka Mto Malagarasi kwa ajili ya kuleta maji katika Miji ya Urambo, Kaliua, Nguruka na Usoke. Mradi huu pia utahudumia baadhi ya vijiji vilivyopo Wilayani Uvinza na maeneo mengine ya Wilaya ya Uyui, Manispaa ya Tabora na vijiji vitakavyokuwa umbali wa kilometra 12 kandokando ya bomba kuu. Mradi huu utasaidia kutoa huduma ya maji safi na salama kwa wakazi wengi zaidi kwa kuwa Mto Malagarasi unayo maji mengi yanayotiririka wakati wote wa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jimbo la Ulyankulu, Serikali imemuagiza Mhandisi Mshauri katika usanifu unoaoendelea kuweka matoleo kwa ajili ya upanuzi wa mradi kwa awamu zitakazofuata ili wananchi wengi zaidi wakiwemo wa Ulyankulu waweze kufaidika na mradi huo. Usanifu wa mradi unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Juni, 2017.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo la kukinga maji ya Mto Igombe kwa ajili ya kujenga bwawa kubwa linahitaji kufanyiwa utafiti na usanifu wa kina ii kulinganisha gharama za uwekezaji na manufaa ya mradi huo. Mipango ya Serikali katika kuendeleza hifadhi ya vyanzo vya maji ni pamoja na kutekeleza miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa mabwawa makubwa. Aidha, kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji Serikali imetoa wito katika Halmashauri zote nchini kuanza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa madogo ambayo yatasaidia kutatua shida ya maji kwa wananchi, mifugo pamoja na umwagiliaji. Kwa sasa Ulyankulu inapata maji kutoka kwenye visima virefu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kadutu.

MHE. JOHN P. KADUTU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, nataka kujua kwa nini hasa Jimbo la Ulyankulu lilitengwa kwa miradi hii mikubwa kwa sababu kutoka Tabora Mjini kwenda

Ulyankulu centre ni kilometa 90, kutoka Kaliua kwenda Ulyankulu ni kilometa 90, kutoka Kahama kwenda Ulyankulu ni kilometa 90...

MWENYEKITI: Mheshimiwa uliza swalii.

MHE. JOHN P. KADUTU: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini Serikali isi-plan kuhakikisha mradi mmojawapo unapeleka maji Ulyankulu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la pili, je, Naibu Waziri yuko tayari sasa kuambatana na mimi baada ya Bunge hili akaone mwenyewe vyanzo vya maji badala ya kusubiri taarifa za maandishi za wataalam wake ambao mimi naamini kabisa taarifa wanazoleta siyo sahihi?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Injinia Kamwelwe majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa Mheshimiwa Mbunge niseme Jimbo la Ulyankulu halijatengwa, ni jimbo jipya, limetangazwa juzi juzi. Nafahamu Ulyankulu ina miradi ya maji ambayo kidogo haina hali nzuri, inatakiwa tuifanyie ukarabati kwa sababu kuna mabwawa ambayo muda mrefu yanatumika na mabomba yapo. Kwa hiyo, tutayafanya kazi ili kuhakikisha yanaimarika na wananchi wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tutafanya utafiti na kufanya ulinganisho ama kutoa maji Kahama au kutoa maji upande wa bomba hili litakalotoka Malagarasi sehemu ya Kaliua. Pale patakapokuwa pako *cost effective*, tutahakikisha kwamba maji yanatoka ama Ziwa Victoria au kutoka Malagarasi na kuhakikisha wananchi wanapata maji yenyehu kuhakikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii lake la pili ameomba kufuatana na mimi. Mheshimiwa Mbunge niko tayari tukimaliza Bunge tufuatane ili na mimi niende nikajionee huko na tushauriane pamoja na Halmashauri ili kuhakikisha

kwamba wananchi wanapata maji safi na salama kwa haraka.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda, naelewa maana ya maji, Mheshimiwa Ester Mahawe, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Saul, Mheshimiwa Phillipo Mulugo na Mheshimiwa Haonga, basi.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika maeneo ya Mkoa wa Manyara hasa Wilaya ya Kiteto na Simanjiro katika Kata za Makame, Ndredo, Lolera kwa upande wa Kiteto na Kitwai, Naberera na vijiji vya Namalulu hali ni mbaya, ule ukanda ni wa wafugaji.

Naomba tu kumuuliza Mheshimiwa Waziri ni lini sasa watu hawa wataweza kupata huduma hii ya mabwawa kwa ajili yao wenyewe pamoja na wanyama?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Waziri kwa kifupi, maji ni shida, nyumba yote imesimama. Waziri mwenyewe wa Maji na Umwagiliaji.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba tuelewane, suala la vijiji anavyovisema na hayo mabwawa anayoyasema tumetoa mwongozo. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge tushiriki katika kuweka vipaumbele katika wilaya zetu kulingana na bajeti ambazo tunaziweka kwamba mwaka huu tunapeleka maji katika vijiji kadhaa na mwaka unaofuata vijiji kadhaa. Pia tumesema kwamba kila Halmashauri iweke katika mapato ya ndani mipango ya kujenga mabwawa.

Kwa hiyo, mambo yote haya yanaibuliwa kwenye Wilaya na Halmashauri husika, ukiniuliza swali la nyongeza hapa nitakujibu kiujumla. Kwa hiyo, mimi nilifikiri ni vizuri sana tukashiriki kuibua miradi kwenye Wilaya ili hivyo vijiji anavyovisema viweze kuwekwa kwenye mipango.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Shally Raymond swali la nyongeza.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ya tambarare ya Kilimanjaro yana shida ya maji safi na salama. Ni lini sasa Serikali itatumia *Lake Chala* ili kuyapatia maeneo ya tambarare maji vikiwemo vijiji vya Mahida, Malawa, Ngoyoni, Ngareni, Holili na kwingineko?

MWENYEKITI: Ahsante, umeelewaka. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iko tayari na inatekeleza miradi mingi ya maji na mipango kemkem ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutoa maji kutoka *Lake Chala*, naomba tushirikiane na Halmashauri yako ambayo hilo bwawa liko katika hiyo Halmashauri ili tuone jinsi gani tunaweza tukafanya utafiti na kuweka fedha kuhakikisha vijiji vinavyozunguka sehemu hiyo vinapata maji.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Saul Amon.

MHE. SAUL H. AMON: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Rungwe ni moja kati ya Wilaya ambazo zimebarikiwa sana kuwa na vyanzo vingi vya maji. Hata hivyo, kuna baadhi ya maeneo maji yamefungwa yasiendelee kutiririka kwa sababu ya uhaba wa maji, hakuna matenki, miundombinu ni ya kizamani mno na watu wameongezeka.

Je, Serikali ina mpango gani na Wilaya ya Rungwe ili kuisambazia maji ambayo hayana taabu ni maji ya kutega? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Maji yanatiririka, ni ya kutege tu, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji Injinia Kamwelwe.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kweli kabisa kwamba Wilaya ya Rungwe kuna maji ya mtiririko/mserereko. Ndilo maana tumehakikisha kwamba kila Halmashauri inapatiwa fedha na Wizara ya Maji na Umwagiliaji ili sasa hilo suala la miundombinu, matenki na watu wameongezeka, kwa sababu maji yapo tuhakikishe kwamba tunaiboresha na wananchi wanawenza kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshauri Mheshimiwa Mbunge kama anaona wataalam wake kidogo wana upungufu, Wizara ya Maji na Umwagiliaji tuko tayari kusaidiana kutoa wataalam ili kwenda kukamilisha hiyo miradi kwa sababu fedha ipo.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Phillipo Mulugo.

MHE. PHILLIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Jimboni kwangu Kata ya Mbangala nina Kampuni inaitwa *Shanta Gold Mining*. Kampuni hiyo imefunga Mto Lwika na kusababisha wananchi wa Mbangala kutopata maji. Miezi miwili iliyopita kulitokea vurugu kubwa sana kati ya Polisi na vijana wa pale Mbangala lakini Serikali ipo na wanaona kabisa bwawa limefungwa na mto hautiririki kwenda hata vijiji vya Maleza. Je, Serikali inaniambia nini juu ya Ashanti wafungue ili na sisi kijiji cha Mbangala tuweze kupata maji?

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kampuni ya Shanti kufunga

bwawa Mbangala, Mheshimiwa Mbunge ndio anatoa taarifa sasa hivi. Naomba tuwasiliane ili tuhakikishe tunatatua hili tatizo kwa haraka sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa mji mdogo wa Mlowo uliopo Jimbo la Mbozi ambao una idadi ya watu karibu 60,000 tangu uhuru hawajawahi kupata maji safi na salama ya kunywa licha ya kwamba Marais wote wanaopita huwa wanaahidi kutatua tatizo hili la maji.

Je, ni lini Serikali itatatua tatizo hili la maji katika Mji Mdogo wa Mlowo ambapo mwaka jana wametangaza tenda lakini hadi sasa hakuna kinachoendelea katika Mji ule wa Mlowo? Ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri mwenyewe, nimemuona Waziri, Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji Injinia Lwenge.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza si kweli kwamba wananchi wale hawajawahi kupata maji toka uhuru. Sema maji yaliyopo pale Mlowo hayatoshelezi kwa wingi wake lakini wanapata maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nikupe taarifa kwamba sasa hivi Serikali imeamua kuanzisha huu Mkoa wa Songwe na tutakuwa na mamlaka moja. Kwa hiyo, Mlowo na Mbozi tutaunganisha mamlaka moja ya maji na tutaipa uwezo zaidi wa kuweza kusambaza maji ya kutosha. Sasa hivi tayari *tender* imeshatangazwa katika kuboresha upatikanaji wa maji Mlowo pamoja na Mbozi.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha sana, lakini nimewavumilia tu kwa sababu ya hali yenyewe, sasa tunaendelea na matangazo.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, wageni waliopo kwenye jukwaa la Spika ni wageni wawili wa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango ambaao ni Profesa Beno Ndulu - Gavana wa Benki Kuu na Dkt. Ngunangwa Balele - Meneja Uchumi wa Benki Kuu. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tuna wageni watatu wa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson pamoja na Umoja wa Wanawake Wabunge Tanzania (*TWPG*) kutoka *Hanns Seidel Foundation* wakiongozwa na Dkt. Susanne Luther, Mkuu wa Uhusiano wa Kimataifa kutoka nchini Ujerumani. Karibuni sana. *We are glad to have you with us here.* (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 34 wa Mheshimiwa Mashimba Ndaki ambaao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango kilichopo hapa Mkoani Dodoma. Wanafunzi wa Mipango mko wapi, simameni. Ahsanteni, karibuni sana. (*Makofi*)

Tuna wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambaao ni wanafunzi 35 na mwalimu mmoja kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*) kilichopo Mkoani Dodoma. Wanafunzi wa *CBE*, haya karibuni sana, masomo ya biashara, m jitahidi. (*Makofi*)

Wageni walitembelea Bunge kwa ajili ya maonyesho ni wageni 22 kutoka Muungano wa Vikundi vya *VICOBA* Tanzania (*VIGUTA*) ambaao wamekuja Bungeni kuwaonesha Waheshimiwa Wabunge nyumba za gharama nafuu kabisa kwa wananchi wetu. Mnakaribishwa mkaone maonesho hayo ya nyumba za gharama nafuu.

Tangazo kutoka Mheshimiwa Joseph Selasini, Mwenyekiti wa Jumuiya ya St. Thomas Moore hapa Bungeni anawatangazia Wabunge Wakristo Wakatoliki, leo Jumatano tarehe 31 Mei, 2017 kutakuwa na ibada ya misa mara tu baada ya shughuli za Bunge kusitishwa saa saba mchana katika kanisa dogo lilitopo ghorofa ya pili, ukumbi

wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kushiriki katika Ibada hiyo Takatifu.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo niliyonayo.

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako, Mheshimiwa Bilago, Mheshimiwa Frank Mwakajoka na Mheshimiwa Kubenea. Tunaanza na Mheshimiwa Kubenea.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuomba Mwongozo. Nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) isomwe pamoja na Kanuni ya 46(1).

MWENYEKITI: Kanuni ya 46(1) inasema nini?

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 46(1) inasema kwamba Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nauliza swali la nyongeza juu ya uwekezaji unaofanywa na wawekezaji wa nje, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara alilijibu swali hilo kwa msingi wa kunigombanisha na wananchi wangu wa Ubungo. Alisema kwamba viwanda vile vinatoa ajira kubwa sana na kwamba angeomba viwanda vilivyopo Ubungo vingehamia kwenye jimbo lake na akasema kwamba tuache kebehi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya msingi illikuwa ni matatizo yaliyopo katika uwekezaji kwenye viwanda vilivyopo Jimbo la Ubungo. Sikukataa kwamba hakuna viwanda, nilisema viwanda viwo lakini kuna matatizo ya msingi ya wananchi wa pale ambapo Waziri badala ya kusema kwamba tukae pamoja tuyajadili matatizo yale anakuja kunitupia mzigo kwamba mimi sitaki uwekezaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa...

MWENYEKITI: Ahsante, umeeleweka.

MHE. SAED A. KUBNEA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako kama Waziri anaruhusiwa kufanya uchochezi ndani ya Bunge wakati ambapo ndani ya Jimbo la Ubungo wapo wapiga kura wa Jimbo la Muleba Kaskazini ambao wanafanya kazi za vibarua.

MWENYEKITI: Mheshimiwa ahsante. Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuomba mwongozo kwa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tishio kubwa la ugonjwa wa Ebola nchini ambalo limetolewa na Mheshimiwa Waziri wa Afya hata leo katika vyombo vya habari, sijaona ni mkakati gani ambao umewekwa kwa ajili ya kuwapa elimu wananchi wa mpakani Tunduma kwa sababu kumekuwa na hofu kubwa sana kwenye mpaka wetu wa Mji wa Tunduma kwa sababu mpaka ule ni mpaka mkubwa kwenye nchi hii na unatumiwa na wananchi wengi kutoka Congo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kujua Serikali imeweka mikakati gani ya dhati kabisa kwenye mipaka yote katika nchi hii na hasa mpaka wa Tunduma na pia kutoa elimu kwa wananchi. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwalimu Bilago.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba Mwongozo kwa Kanuni ya 68(7) ikisomwa pamoa na 46(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nauliza swali la Mheshimiwa Zitto, swali namba 313 majibu yalijotolewa

hayakuwa yamekamilika kwa sababu Mheshimiwa Zitto alitaka kujua ni kwa nini vyombo vya uvuvi kama mitumbwi inatozwa *SUMATRA*, wakati siyo chombo cha usafirishaji sambamba na ambavyo magari yasiyo ya usafirishaji ambayo hayatozwi *SUMATRA* kwa mfano matrekta hayatozwi *SUMATRA*. Kwa hiyo, mtumbwi wa uvuvi ni sawa na trekta la mkulima. Kwa hiyo, majibu aliyotoa imeonesha kama vile chombo cha uvuvi kile kinasafirisha wakati hakifanyi usafirishaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, wakati nauliza swalii la nyongeza kuhusiana na bodaboda zinazotozwa *SUMATRA* alieleza kwamba ni kwa sababu ya kukagua. Mimi nikawa nimezungumzia bei inayotumika, sikatai ukaguzi, lakini angalia kitikimoja kinatozwa shilingi 22,000; mwenye basi la abiria 80 atatozwa bei gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Na mimi naomba mwongozo wako kwa Kanuni ya 68(7) ikinsomwa pamoja na Kanuni ya 46.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri wa Maji anajibu swalii kuhusu kutoa maji Malagarasi kwenda Ulyankulu alisema kwamba maji ya Malagarasi yanatosha. Taarifa niliyonayo ambayo ni kweli na ya sasa hivi, taarifa hizo zake ni za zamani, Mto Malagarasi uko kwenye tishio kubwa la kukauka baada ya kuvamiwa na ng'ombe zaidi ya laki nane kwenye *wetland* ya Malagarasi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilitaka tu kupitia kwako Waziri ajue kwamba hiyo Malagarasi anayoisemea taarifa alizonazo na walizojibia swalii ni taarifa za zamani na haya maji hayataendelea kuwepo kama hali hii itaendelea.

Kwa sababu amesema wanaanza kwenda kufanya upembuzi yakinifu mwezi Julai, nimshauri Waziri kabla ya kufanya chochote wakajiridhishe na bajeti ya maji ya Mto Malagarasi vinginevyo Malagarasi itakuwa haipo na hiyo miradi ya kwenda Kaliua na Ulyankulu itakuwa ni hadithi ambayo haipo. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Nianze kwa mtiririko huo huo kama niliviyowatambua waomba Mwongozo.

Mheshimiwa Kubenea ametumia Kanuni ya 68(7) pamoja na Kanuni ya 46(1), niseme moja kwanza, muuliza swali la msingi Mheshimiwa Mwanne Mcemba, akajibiwa jibu la msingi na baadaye amesimama aauliza maswali mawili ya nyongeza na akajibiwa na Serikali akaridhika. Wabunge mna haki au mna fursa na ninyi wasiozidi wawili au watatu kuuliza maswali ya nyongeza, lakini kwa Mwongozo ambao umeshatolewa siku za nyuma kuhusiana na suala kama hili, Mbunge mwagine ambaye siyo muuliza swali la msingi hawezi akadai kwamba swali alilouliza yeye halikujibiwa kikamilifu. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, sababu ipo wazi tu, mwenye swali la msingi aliyeuliza alikuwa na shabaha fulani na Serikali imemjibu kwa maandishi, amesimama baada ya jibu hilo kutolewa aauliza maswali ya nyongeza akaona kwamba kule alikotaka kufika kwa jibu la Serikali hakufikishwa, yeye ana haki ya kusema sasa nasimama kutaka swali langu lijibiwe kikamilifu, lakini kwa wengine ambao tunaingia kama tishali huwezi ukajibiwa kwa sababu ni swali la papo kwa papo. Mara nyingi mnaona Waziri *unless* amejipanga vizuri sana atatoa majibu ya juu juu tu. Ndiyo maana Mwongozo huu ambao na mimi ninausitiza sasa ni kwamba Mheshimiwa Kubenea kama unataka wewe kuja kwa *gear* hiyo ombo na wewe uulize swali la msingi ili sasa Serikali ikujibu.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndiyo Mwongozo wangu lakini huwezi ukalalamika kuititia majibu ya swali lako la nyongeza.

Mheshimiwa Frank Mwakajoka, Mbunge wetu Tunduma kuhusu tishio la Ebola, kikanuni nadhani tu umetaka kusikika kwa wananchi wako maana ni tukio ambalo halijatokea humu Bungeni leo na mimi nasimama kwenye Kanuni hizi. Kwa *aspect* hiyo Mwongozo wangu ni kwamba sina ombi sahihi la Mwongozo kwa hilo. Hata hivyo, kwa vile inahusu hali ya usalama wa afya za wananchi wetu hasa kwenye mipaka, Serikali imesikia na ipo Bungeni wakiona kwamba kuna haja ya kulitolea tamko watasema wenyewe. Kwa hiyo, mwongozo wangu ni kwamba halijakaa vizuri kwa mujibu wa Kanuni ya 68 (7). (*Makofii*)

Mheshimiwa Bilago umeuliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Zitto ambaye ameuliza swali la msingi, wewe upo sawa pale kwa sababu umeuliza kwa niaba ya mwenye swali na umejibowi na Serikali, lakini unaamini kwamba majibu ambayo yametolewa na Serikali kuhusiana na hayo maeneo mawili mitumbwi na bodaboda kwamba halijakaa vizuri. Kwa sasa hivi Mwongozo wangu kwa swali lako acha tukasome vizuri majibu hayo na hasa yale ya nyongeza tujiridhishe kama swali lako au maswali yako ya nyongeza yamejibowi na Serikali. Pia unasema hata swali lenyewe jibu la msingi bado una wasiwasi kwamba halijajibowi kikamilifu na Serikali. Naahirisha kutoa mwongozo kwa hilo mpaka tupate hiyo fursa ya kupata majibu vizuri.

Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, swali la Mheshimiwa Kadutu limejibowi na kauliza maswali ya nyongeza akaridhika na wewe unaangukia kwa yale niliyosema kwa Mheshimiwa Kubenea. Hata hivyo, kwa vile Serikali ipo na wewe unasema hali ya maji ya Mto Malagarasi kama unavyofahamu wewe jibu hili wametumia taarifa za zamani, ndio hoja yako.

Sasa kwa vile wanaenda kufanya upembuzi yakinifu wa mradi huo haya ndiyo mionganoni mwa masuala ambayo watakumbana nayo, yawezekana taarifa zao ni za juzi lakini watakapoenda *site* ndiyo wataona hali halisi ya hoja hiyo. Nawe ulikuwa unaangukia kwa mwongozo wangu. Wewe unasema limetokea humu asubuhi kwa sababu ni majibu ya

Serikali, ndiyo hoja yako nimekuelewa lakini majibu ni hayo maana umeuliza la nyongeza mwenye swalii la msingi alikuwa ameridhika na majibu hayo lakini mimi naamini Serikali imesikia.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo kiporo cha Mwongozo ni hili la Mheshimiwa Bilago kuhusiana na bodaboda na vyombo vyajini (mitumbwi).

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema haya, nadhani tuko vizuri, Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Fedha na Mipango

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tuna orodha zetu kwa uwiano ule ule, nitajitahidi muda ndiyo huo tumeula sana leo, tuanze na Mheshimiwa Khatib Haji.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nichukue fursa hii adhimu kuwataki kheri na baraka Waislamu wenzangu katika Mfungo huu Mtukufu wa Mwezi wa Ramadhani. *(Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nianze na utangulizi ufuataao. Tarehe 25 Oktoba, 2015, Watanzania walifanya maamuzi ya kumchangua Rais, John Pombe Magufuli kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunakubaliana hilo halina hoja wala dawa, ni jambo lilitokea na sisi tunakubali.

Hata hivyo, Watanzania hao hao sambamba na kumchangua Rais waliwachagua Wabunge hawa kuwa ndiyo kioo cha kuisimamia, kuielekeza na kuishauri Serikali yetu. Kwa

hivyo, tulichaguliwa pamoja naye Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, ana wajibu mkubwa sana kutusikiliza vizuri sana na kuititia Waziri Mkuu mimi ningependa tu mpelekee salamu moja Mheshimiwa Rais ya upendo, kwamba tulichaguliwa pamoja naye kwa hivyo ayape uzito sana tunayoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchaguzi ule kuna wenzetu wengine walitukimbia hapa, waliondoka wakati mbaya sana, kuna wengine walikwenda Rwanda kuona dada wenye shingo refu kule, lakini leo wamerudi hapa Mheshimiwa Rais ndiyo anawafanya watu wa karibu sana kuwaalika ikulu kila linapotokea jambo, hawafai hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule wa mapambano ilikuwa tukae pamoja kuivusha nchi yetu katika uchaguzi ule wapo tuliokuwa naye na hatutamuacha, aendelee kushirikiana na sisii, aachane na wale wengine wababaishaji, hawatamsaidia. Mheshimiwa mpe hiyo salamu, ahsante sana. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie habari ya wafanyabiashara, inaonekana Waziri Mkuu hukunifahamu lakini nitakuwa kwenye meza yako nikupe vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara si maadui, wafanyabiashara wa Tanzania ni watu tunaowategemea sana katika kuleta pato la nchi hii. Katika nyendo tunazokwenda nazo hivi sasa kauli zetu, kauli za viongozi haziashirii wema kujenga ukaribu na wafanyabiashara badala yake tunajenga uhasama na chuki na wafanyabiashara jambo ambalo halitatuletea tija. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaka kuvuna maziwa mengi katika ng'ombe lazima tumlishe vizuri, usitegemee ng'ombe usiyemlisha utapata mavuno mazuri, hutapata maziwa yanayostahiki. Kwa hiyo, tunatakiwa tuangalie, hivi sasa tunakuwa na tabia hasa Mawaziri wetu mnakuwa na ile kitu kuona mseme yale yanayompendeza Mheshimiwa lakini hamtaki kumwambia hali halisi tuliyonayo katika nchi. Sasa hivi Kariakoo mlango wa biashara ulikuwa unatoa

kilemba mpaka shilingi milioni 30 kuupata kabla ya kulipa kodi lakini sasa hivi wafanyabiashara wenyewe majumba wamekosa kabisa wafanyabiashara wa kukodisha fremu za milango. Hiyo ni ashirio moja kwamba biashara inakokwenda sio kuzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna wajibu wa kukaa nao wafanyabiashara tukaona ni kipi kinachowakwaza. Jana alisema mwenzangu mmoja hapa hamtangazi tena mapato ya kila mwezi lakini iko sababu kwa nini hamtangazi. Tuliwaambia mwanzo mnachokusanya ni *arrearszinazotokana* na malimbikizo ya nyuma zikimalizika hizi makusanyo hayo tunayojidai nayo yatakuwa hayapo tena na ndicho kinachotokea sasa. Likija suala la mapato Taifa linakuangalia wewe Waziri nakushauri hebu tukae na wafanyabiashara tuangalie yanayowakwaza ili tupate njia ya kutokeea. Sasa hivi tumekwama na tunapoelekea ni kubaya zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nataka niseme habari ya kodi wanayotozwa watu wenyewe magari mabovu, jana mwenzangu mmoja alizungumzia na mimi nataka kulirudia. Elimu ni kitu muhimu, Watanzania unapokuja mfumo mpya wa kodi au jambo jipya ni lazima kwanza waelekezwe. Mfano mtu alikuwa na gari amenunua limekufa miaka 10 nyuma lakini leo akinunua kigari chake kingine akienda *TRA* anaambiwa gari hii ullipie kodi zote za miaka 10, hii kweli ni haki? Haya mambo yapo na sasa hivi imekuwa ni shida kubwa sana kwa watu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napendekeza Mheshimiwa Waziri, ili gari litembee lazima lipate mafuta, tuhamishie hayo mengine hata kama ni *percent* ndogo iwekwe kwenye mafuta kwa sababu gari linalotembea litakuwa linatozwa pale gari linapotumika, gari likifa itakuwa hakuna tena kesi baina ya raia na Serikali. Sasa inakuwa tunajenga uadui, wananchi wanaona *TRA* kama maadui wakubwa na siyo hivyo, nchi za wenzetu wafanyabiashara ni marafiki wakubwa na vyombo vinavyokusanya kodi, kwa nini sisi tunakuwa mahasimu wakubwa? Ni kwa sababu

mnakuwa na sheria za mwendo kasi, halichachi, ni pale mnapoamka mkaamua kufanya mnafanya, haiwezekani. Lazima tuwaandae watu wetu linapotokea badiliko la kisheria ili watu wajandae na hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie misaada ya nje ya nchi ya wahisani. Hakuna asiyejua kwamba nchi yetu misaada tuliyokuwa tukipata toka *Millennium Challenge Account* mekatika na haikukatika kwa bahati mbaya wameacha kutusaidia kwa sababu walizozia inisha mapema. Waliainisha mambo mawili wakisema wao hawatakuwa tayari kuendelea na ufadhilli kwamba mambo haya ndani ya nchi hayakushughulikiwa nayo ni suala la uchaguzi wa Zanzibar na suala la Sheria ya Mitandao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo mawili wahisani walitueleza wazi na bahati nzuri sana Waziri wa Mambo ya Nje nilimsikia kwa masikio yangu akisema kwamba; "haya ni mambo madogo, tutayashughulikia haraka na ufumbuzi utapatikana" yaah, ndiyo alivyozungumza. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea kwa kauli ile murua, mwanana, *burudaa wal asilla*, jambo hili litapatiwa kweli ufumbuzi. Niwaulize wenzangu mmeshindwa nini? Utawala wa JK tulikuwa na changamoto za kiuchaguzi lakini watu walizungumza wakafikia makubaliano na nchi ikaenda, nchi haikuzuiliwa misaada, tatizo nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu sisi lilitokuwa kubwa lipi ambalo halizungumziki. Watanzania ni wamoja, linakuja jambo, msaada ule wa *Millennium Challenge* ulikuwa ukisaidia sana umeme vijiji, leo sababu ya Wazanzibar milioni moja na nusu na Watanzania milioni 50 wanakosa msaada ule muhimu kwa upande wa Tanzania Bara, kwa jambo ambalo tungeweza kukaa kuzungumza kwani kubwa lipi sisi tunatoa moto kwenye midomo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno asali tunatoa midomoni mwetu, kwa nini nyie msitoe maziwa tukawa karibu, tatizo nini? Msaada ule bado ni muhimu, kweli kuomba ni aibu, lakini ukiwa huna omba kuliko kuiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nasema bado tuna haja na Waheshimiwa Wabunge nawasikia kila siku hapa likija suala la umeme vijiji kila mmoja ananyanyuka *REA*, *REA*, hakuna *REA* ile pesa haiko, mimi nawaambia, tusidanganyane. Ile pesa kubwa iliyokuwa ikitupa kiburi kuendeleza miradi ya *REA* ya umeme vijiji imematika kwa sababu ya mambo mawili tu, Sheria ya Mtandao na Uchaguzi wa Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumza uchaguzi wa Zanzibar wengine mnakasirika na huu Mwezi wa Ramadhanii sipaswi kumkwaza mtu, nasema kwa lugha nyepesi sana kwa lugha ya maziwa na asali tukaeni tujadili tuone umuhimu wa kuzishawishi nchi za *European Union* kurudisha...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, muda wako ndio huo, una Kiswahili kizuri cha Pemba. Tunaendelea, dakika tano, tano hawa, Mheshimiwa Riziki Lulida na Mheshimiwa Ally Saleh. Tutaanza na Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia mambo mawili tu, la kwanza ni suala la *investor confidence* ambalo jana Mheshimiwa Lema alilizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo kubwa Tanzania la *investor confidence* kwa sababu ya kauli nydingi ambazo zinatolewa na Serikali, matendo mengi ambayo yanatendwa na Serikali ambayo katika nchi nyingine athari yake inaonekana moja kwa moja, lakini hapa kwa kuwa athari yake hatuioni moja kwa moja kwa sababu *stock*

exchange yetu haifanyi kazi kama vile ambavyo ingetakiwa tunadharau.

Kwa hiyo, napenda niishauri Serikali na Mheshimiwa Waziri kwamba wakae na Serikali na wajaribu kutengeneza namna ambayo *shock* ya kibashara, *shock* ya uwekezaji inaweza kupata nafasi kidogo kwa kuzuia kauli au matendo ambayo yanapoteza *investor confidence*, hilo moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa MNwenyekiti, lakini lingine nitalizungumzia kwa undani kidogo ni suala la Mfuko wa Pamoja wa Fedha ambapo leo hii halitochacha mpaka nipate majibu, kwa sababu hili lipo Kikatiba, miaka *almost* 40 hivi sasa halijafanyiwa kazi, kwa nini linashindwa kufanyiwa kazi? Kama vile ambavyo Mahakama ya Katiba ambayo nchi hii imesema iundwe mpaka leo haijaundwa badala yake tunatatua matatizo yetu ya Katiba kwa kuitia kwa Tume ya Pamoja au *whatever*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko huu wa Pamoja wa Fedha tokea kuasiwi hivi sasa tumeshapoteza mamilioni katika kuiendesha na kujaribu kufanya kazi, mabilioni yote ambayo yametumika yamekwenda bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Pamoja ni *white elephant* haujaundwa, haujatumika na kwa hivyo bado matatizo ambayo yameundiwa kwayo yako pale pale kwamba Zanzibar inalaumika haichangii katika Muungano, lakini Zanzibar inasema itachangiaje katika Muungano wakati hajui matumizi yapo viyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Bara hayawezi kuwa sawasawa na matumizi ya Zanzibar kwa sababu Zanzibar ni ndogo kama inataka askari, inataka askari kidogo kuliko Tanzania Bara, kama inataka kulinda mipaka Tanzania Bara inapakana na nchi tisa wakati Zanzibar inapakana na Kenya peke yake. Kwa hiyo, kuna mambo mengi ambayo hatuwezi kwenda sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi kulikuwa na ripoti nyingi zimefanywa, moja ni ripoti ya *black*, nyingine ni ripoti ambayo imetengenezwa na *Coopers and Lybrand*, ikionesa namna gani kunawenza kuwa na *formula* kwa sababu inaonekana *formula* ya 4.5 ambayo tunagawana hivi sasa imepitwa na wakati. Kwa hivyo, mfuko huo siyo tu utaonesha Zanzibar ichangie kiasi gani na Tanzania Bara ichangie kiasi gani, kuondoa lawama kwamba Zanzibar inabebwa au Zanzibar inapata bure kila kitu, pia utaonesha namna ambavyo fedha za Muungano, zilizo halali za Muungano hazitumiki kwa Serikali ya Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusikatae ukweli, hapa tuna mamlaka tatu, tuna mamlaka ya Zanzibar, tuna mamlaka ya Muungano na tuna mamlaka ya Tanganyika, Tanganyika ipo, haijawahi kuondoka, kwa sababu mfanyakazi wa kilimo wa Tandahimba ni mfanyakazi wa Tanganyika siyo mfanyakazi wa Muungano. Mfanyakazi wa Mbeya, Nachingwea wa Wizara ya Afya ni mfanyakazi wa Tanganyika siyo mfanyakazi wa Muungano, tunajidanganya siku zote. Kwa hiyo, mamlaka ya Tanganyika ipo, imekuwa inatumia fedha za Muungano kwa ajili ya Tanganyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiwepo Mfuko wa Pamoja na hizi ripoti zimeonesha ni kiasi gani fedha za Muungano zinakusanywa na hizo fedha za Muungano zinatosha kuendesha Mamlaka Tatu, Mamlaka ya Tanganyika, Mamlaka ya Zanzibar na Mamlaka ya Muungano. Kwa hiyo, mpaka leo mfuko hauundwi kwa sababu watu walioko Tanganyika wana hofu ya ku-expose hiyo, kwamba kuna fedha za Muungano zinatumika kwa Tanganyika, wana hofu ya kuonesha kwamba Zanzibar inaweza kuchangia iwapo kungekuwa na usawa kwa maana ya kwamba Zanzibar itashirikiana kitu gani na Muungano itashirikiana kitu gani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri leo hii natangaza kabisa, najua mtashinda kwa wingi... (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa muda wetu ndio huo, Mheshimiwa Riziki Lulida dakika tano.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru nami kwa kupata nafasi hii. Niungane na Mheshimiwa Ally Saleh kuhusu *investment confidence* haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikuwa katika mkutano wa malaria ambao uliandaliwa na *USAID* na wao wameingia katika uwekezaji katika malaria, ambacho ni kiwanda kimojawapo nataka nikitolee mfano cha *A to Z*. Kile kiwanda kina wafanyakazi 8,000 kinalipa kodi bilioni 17, kinalipia *TANESCO* bilioni moja, lakini cha kusikitisha kwa vile hakuna *health policy*, narudia tena hakuna *health policy* inayomfanya yule mwekezaji awe na *confidence* na uwekezaji wake. Kwa mfano, ye ye ana kiwanda cha kutengeneza chandarua ambazo zina dawa na zimehakikiwa kimataifa na ndani, lakini leo wanaingiza vyandarua feki kutoka nchi za nje ambazo yule mfanyabiashara analipa kodi, yule anaambiwa kwa vile chandarua tunagawa bure anaingiza bidhaa zile bure. Tunajiliza, tuko tayari kusimamia viwanda vyetu au bado tunakutana na kipingamizi kikubwa kwa vile hatuna sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza hapa kuwa nchi hii bado hatujaingia katika sera ya viwanda na tunakwenda katika viwanda, sera iko wapi? Matokeo yake huyu anaingiza hiki, huyu anaingiza hiki, matokeo yake kiwanda kitakuwa, watu 8,000 Watanzania waliopata ajira, zitakuwa zimepotea. Ushuru mkubwa anayepeleka *tax* ya bilioni 18, huyu anaingiza bidhaa kutoka nje, *even price control* inakuwa haipo. Tunataka tufanye kazi tukijua tuna idadi ya kiasi gani? *Quantity, quality, price* na *time delivery* inatakiwa ijulikane. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama tunakwenda katika uwekezaji wa kiholela bado viwanda vyetu vitakuwa vinasuasua, wanaleta wawekezaji wa nje, ndani watafunga hivi viwanda na tutakuwa hatuna kodi, wala kutakuwa hakuna ajira. Tuwe wa kweli, tusimamie sera, wailete Bungeni

tufanyie kazi, lakini wakiendelea viwanda, wakati hakuna sera, kutakuwa hakuna biashara wala hakuna maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mdau natoka Lindi, Selous ni mbuga kubwa nazungumzia huu ni zaidi ya mwaka wa kumi, lakini jiulize kama *TANAPA*, Serengeti ni ndogo inaingiza bilioni 100, Selous hamna kitu ni ubabaishaji, kuna nini hapa? Kwa nini kuna kigugumizi ndani ya Selous? Korido ya Seleous ambayo ina tembo inafanyiwa *promotion* gani? Hakuna. Wanakwenda kuwakamata akinamama wauza maandazi, wanaouza mitumba mikononi, lakini wanaacha mabilioni ambayo yako katika Selous. Ili nchi hii iendelee tunahitaji uongozi, siasa safi na watu. Sasa kama vitu hivi havisimamiwi kwa pamoja itakuwa hatufanyi kazi ambayo imetuleta hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kuhusu suala la mjusi. Mjusi ukiingia ndani ya *exhibition* unalipa *Euro* 24 kwa mtu mzima, kwa watoto wanaingiza kwa *Euro* 12, lakini kwa mwaka wanaingiza *Euro* milioni 600. Uki-convert into Tanzanian *shillings* unapata *trillions* of *trillions*. Sisi tunapata nini? Jamani hata tukitaka *revenue* au kukaa chini tukatengeneza mrabaha, nchi ikajipatia hata angalau bilioni 200 haiwezekani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafumba macho wanaangalia vitu vidogovidogo pombe, soda, jamani mbona wana mabilioni ya pesa wanayaacha, hawaoni kama wana uchumi mkubwa wanauacha? Wanatuweka Tanzania katika hali ngumu, lakini kumbe hali ya kupata uchumi ipo. Tujiulize, kwani wataalam wanafanya kazi gani? Uchumi huu wanaoukalia wanafanya nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike mahali basi tuambiane ukweli kama tumeefeli tuseme tumeefeli; kama hatujafeli mambo matatu nataka yatekelezwe. Suala la pato la mjusi, suala la Selous na suala la wawekezaji wa ndani kupewa kipaumbele ikiwemo *A to Z* ya Arusha. Wameweke Mwekezaji, amekuwa *frustrated* hata kufunga kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengine nakushukuru sana dakika tano zimenitosha. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa kutunza muda. Tunaendelea na Mheshimiwa Omary Mgumba atafuatiwa na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Martha Umbulla ajiandae.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Fedha. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya na uzima tumekutana siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mchango wangu nitajielekeza kwenye milioni 50 za kila kijiji. Mheshimiwa Waziri wa Fedha mwaka jana wakati alipokuja hapa alikuja na mpango mzuri na Bunge lako hili lilitenga zaidi ya shilingi milioni 59 kwa ajili ya kutekeleza azma hii ya kupeleka milioni 50 kila kijiji. Hata hivyo, mpaka muda huu tunaongea kutokana na ripoti ya Kamati na hali halisi hata kule kwenye vijiji vyangu, hakuna kijiji chochote ambacho kimeshapata milioni 50. Moja ya changamoto kubwa ambayo tunakutana nayo sasa hivi tukienda kwenye Majimbo swalii la kwanza utaulizwa milioni 50 zitakuja lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna shida kubwa sana kule vijijini kwa sababu, niwapongeze sana UWT upande wa akinamama walifanya kazi kubwa sana pamoja na Wabunge kuhamasisha vikundi vingi sana vimeanzishwa kwa matarajio kwamba kuna milioni 50 zitakuja, kwa sababu tuliwaambia kwamba tutapitishia kwenye vikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali wakati inakuja kufunga mjadala huu ni vizuri ikaja na kauli thabiti ya Serikali kwamba hizi fedha zitatoka au zimebadlishwa mpango mwingine ili tuwe na jibu la Serikali na Wabunge kuwapelekea wananchi wote tuwe na msimamo mmoja badala ya sasa hivi wananchi hawatuelewi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nikikumbuka ile bajeti

ya mwaka jana Mheshimiwa Waziri alisema tumetenga milioni 59, mwaka huu tungepeleka labda milioni 50, mwakani 50 mpaka miaka mitano vijiji vyote tungevimaliza. Sasa mwaka jana hatukupeleka hata senti tano, lakini bajeti ya mwaka huu inakuja na milioni 60. Nilitegemea kwa sababu hatukupeleka mwaka jana bajeti ya mwaka huu ingekuja na mia au zaidi ya mia ili twende na mipango ambayo Serikali ilipanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nijielekeze kwenye mapato. Tatizo kubwa la nchi yetu hasa nchi hizi za dunia tatu ikiwemo na Tanzania tuna mahitaji makubwa sana lakini mapato yetu ni madogo. Katika hili niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Tano, watu wengi walikuwa wanalaumu kwa nini tumepokea mpaka sasa asilimia 34 ya fedha za miradi ya maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza kwa sababu kabla haijaingia madarakani Serikali ya Awamu ya Tano zaidi ya miaka miwili, Serikali Kuu ilishindwa kupeleka hela za maendeleo katika Halmashauri zetu. Sasa leo tumepata asilimia 34, kutoka sifuri unapata asilimia 34 ni suala la kupongeza sio kubeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema katika hili ni ukweli usiopingika, hali ya biashara sasa hivi nchini siyo nzuri, biashara nyingi zinafungwa. Maana ya biashara kufungwa ni kwamba ajira za Watanzania zinapotea, mapato ya mtu mmoja mmoja na wafanyabiashara yanapotea, mapato ya Serikali yanapungua. Huko mbele tusipochukua tahadhari ya kuongeza *tax base* ya walipa kodi nchi hii inawezekana walipa kodi watapungua na mapato ya Serikali yatabungua sana. Baadaye hata haya tuliyofikia sasa yatakuwa yanapungua, kwa sababu athari nyingine itakuja, tutawakandamiza wale wachache walipa kodi, tuwaongezee viwango badala ya kuisambaza hii kodi kwa watu wengi zaidi ili waweze kulipa kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika hili, nimeona katika ukurasa wa 77 wa kitabu cha Mheshimiwa

Waziri amesema kwamba, miongoni mwa mikakati yao ni pamoja na kurasimisha biashara nyingi zisizokuwa katika mfumo rasmi kuja kwenye mfumo rasmi wa kodi. Leo hii tuna tatizo katika nchi yetu, Mtanzania mfanyabiashara akisikia biashara yake imetembelewa na Polisi au imetembelewa na *TRA* anapumua zaidi ikitembelewa na Polisi kuliko *TRA*. Anajua leo sijui kuna shida gani? Au leo umaskini sasa umeshaingia kwenye biashara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika hili, niombe kama kweli tunataka kuwarasimisha na kupanua *tax base* katika hili, tupate walipa kodi wengi katika nyanja hizi, basi Serikali inapaswa itoe elimu ya kutosha kwa walipa kodi na Watanzania kwa ujumla, umuhimu wa kulipa kodi, manufaa kwa nchi na kwenye hii biashara yenyewe, watu waelewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kutoa *incentive* maalum kwa wajasiriamali wa ndani. Kuwaambia mtu ye yote yuko huru kurasimisha biashara yake kuingia kwenye mfumo wa kodi, tutaanza kudai kodi hapo alipoanza kurasimisha kwenda mbele. Tatizo sasa hivi zinafungwa biashara nyingi, sio kwamba hawapati faida, wakati mwininge mtu anaona anakuwa salama zaidi kufunga biashara aachane na Serikali kuliko aje ajitangaze kurasimisha anapewa madeni kuanzia miaka ilipoanza hiyo biashara, akija kuangalia uwezo wa kulipa hana, matokeo yake biashara inakuwa hohehahe na anafilisiwa kabisa. Sasa kwa nini mtu aje ajirasimishe kwa nini asifunge tu aachane nayo atafungua biashara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali kama kweli tuna dhamira ya kuwasaidia wajasiriamali na kweli tuna dhamira ya Watanzania walipe kodi bila kushurutishwa basi ni vizuri tutoe *incentive*. Tuseme miezi sita au mwaka mtu ye yote tutaanza kulipa kodi pale unapoanza kurasimisha biashara yako kwenda mbele. Nilishawahi kusema humu ndani tuchukue mfumo kama wa Wizara ya Ardhi inavyofanya, leo nikipima ardhi yangu mimi naanza kulipa leo, huwezi kusema kwamba miaka yote unatumia ardhi hii lazima ulipe, hakuna mtu atakuwa na huo uwezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwenye matumizi. Ni kweli mwenzangu mmoja alizungumza huku, sisi tuna tatizo kubwa sana la mapato ni madogo lakini hata hayo mapato yenyewe madogo, Serikali inajibana, *TRA* wanajibana yakifika kwenye Halmashauri zetu au taasisi zetu hayatumiki kwa makusudio ya Serikali iliyopanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa mfano kwenye Halmashauri yangu ya Morogoro, kuna miradi kwa mfano miradi ya maji pale Kiroka na Tuluwakongo, hela zimekuja tangu 2015 milioni 700 mpaka zimeanza kutumika leo kwa mbinde kwelikweli, kwa sababu zile pesa zinatakiwa Mkandarasi zisimamiwe kule vijijini, sasa watu wa halmashauri hawana maslahi binafsi ya asilimia 10, kwa hiyo hawaoni umuhimu wowote wa kusaidia hilo jambo liende. Wako radhi wananchi wakose hiyo huduma kwa vile tu wao hawana maslahi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vizuri Serikali mkaweka mifumo sahihi ya ufuatiliaji ili mijue fedha mlizozipeleka kule zinatumika? Kwa sababu sisi Madiwani tunadanyanya sana na hawa wataalam na wao wanasema kila kitu tuwaachie wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapeni mfano mwingine. Kwenye hiyo hiyo Halmashauri juzi tu tumetoka kwenye Kamati ya Fedha, walileta pale pesa walizoleta zaidi ya milioni 360 kwa ajili ya miradi ya maendeleo lakini wakatuletea sisi shilingi milioni 170 wakasema zingine hamna, na *bank statement* wanakuletea kabisa unaambwiha haipo. Baada ya kubanana sana zikaja ikaletwa tena, tulizisahau milioni 190. Sasa mambo kama haya wakati mwingine kama mnavyofahamu wasimamizi wakubwa ni madiwani, lakini madiwani wenyewe hawa hawana mishahara. Sasa akirubuniwa kidogo ni rahisi sana kupitisha kwa sababu anajiangalia yeze na maslahi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba, kwa sababu Madiwani ndio wasimamizi wakubwa wa Serikali kule chini wa pesa za wananchi, ni vizuri Serikali

ikaangalia namna gani ya kuwalipa mishahara Madiwani ili waweze kusimamia pesa za umma zitumike kama zilivyopangwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Wakaguzi wa Ndani kule kwenye Halmashauri, kila akitaka kwenda kukagua miradi anaambiwa hatuna pesa Serikali haijagawa *OC*. Hizo pesa wakati mapato ya ndani yapo! Morogoro *DC* tumekusanya zaidi ya bilioni 1.6, haijawahi kufikiwa tangu uhuru ianze, tulikuwa tunaishia milioni 500, 600, lakini leo Mkaguzi wa Ndani anaambiwa kwamba hakuna *OC* huwezi kwenda kukagua ile miradi, kwa sababu wanaficha mambo yao waliyoyafanya. (*Makof*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Martha Umbulla na Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae.

MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami uniruhusu pia niwashukuru sana wenzangu kwa kunipa pole pale nilipofiya. Pamoja na hilo nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na hata leo naendelea kufunga katika kutimiza ibada ambayo anaisimamia yeye mwenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie pale ambapo ameishia mjomba wangu kutoka Morogoro katika jambo la Ofisi ya *CAG*. Ni kweli yamesemwa mengi juu ya *CAG* kwamba zile fedha kwa ajili ya ukaguzi zinachelewa na ushauri mzuri umetolewa, lakini nataka nizungumzie sana kwenye hili suala la *Internal Auditors*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Internal Auditors* hawawezi kufanya kazi bila maelekezo ya Ofisi ya Mkurugenzi, tukumbuke kwamba huyu anaenda kukaguliwa ndio huyo huyo ambaye anatoa hiyo ruksa kwa ajili ya kukagua hizo fedha. Nataka niseme, kama utaratibu huu utaendelea haya anayoyasema Mheshimiwa Mbunge hapa kwamba unakwenda kuomba *OC* kwa ajili ya kufanya ukaguzi unaambiwa *OC* hakuna basi ndivyo ambavyo itakuwa inafanyika kila muda ambapo tunataka ukaguzi ufanyike, lakini kwa nini wanafanya hivyo? Maeneo mengi yanafanyika kwa sababu ofisi za Wakurugenzi na Watendaji wengine wamekuwa wabadhirifu na kwamba wanatumia mgongo wa kutokupatikana kwa *OC* ili kuficha makosa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachopenda kupendekeza kwa Serikali yangu, sasa Ofisi ya *Internal Auditor* londolewe katika Halmashauri zetu, ziwe moja kwa moja zina mahusiano na Ofisi ya *CAG* Makao Makuu ili kiasi kwamba wanapokwenda kukagua vitabu basi wawe wanakagua kwa mujibu wa taratibu na *authority* ambayo wanakuwa nayo kutoka kwenye Ofisi Kuu ya *CAG*, lakini kuendelea kuziacha hizi ndani ya Halmashauri ni kuendelea kutwanga maji ndani ya kinu na hatuwezi kupata unga tunaoutarajia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nishukuru sana kazi kubwa inayoendelea kufanya na Serikali yangu katika kuhakikisha kwamba inaendelea kuweka fedha nyingi katika maeneo ya kilimo. Nimesoma kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri juu ya jitihada kubwa zilizofanyika kupitia Benki ya Kilimo na jinsi ambavyo wameweza kuwafikia watu wengi. Pamoja na hilo, ushauri kwa Serikali yangu ni kuendelea kuangalia maeneo ya kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika mwaka uliopita tumeshuhudia katika taarifa mbalimbali ikiwemo taarifa ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kwamba katika mazao ambayo yameiletea fedha nyingi nchi yetu ni pamoja na zao la korosho, pia zao la pamba. Kwangu katika kitabu hiki niliposoma hasa katika eneo la jinsi ambavyo Serikali

imeenda kusaidia wakulima, katika kuwapa elimu, fedha katika vikundi mbalimbali kwa ajili ya kujiendeleza, maeneo hayo mawili makubwa sijayaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atueleze juu ya mkakati wake alionao sasa wa kuangalia jinsi gani anawezesha maeneo haya au wakulima hawa waweze kufaidika. Kwa mfano tumeona wenzetu Morogoro hasa katika eneo lile la kilimo cha mpunga kule Kilombero wameweza kufaidika na mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia akumbuke tunalo Bonde kubwa sana la Ruvu ambalo lina *accommodate* chakula ambacho kinauzwa katika eneo kubwa la Dar es Salaam. Hata hivyo, leo hii tulivyo pale, wakulima wale na vikundi vile vyta wakulima havina jinsi wanavyoweza kutunisha mifugo yao. Ninachomwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuelezea kwenye eneo la kilimo basi pia aeleze na matumaini mapya ya wakulima hasa wa Bonde la Ruvu na Bonde la Wami jinsi gani wanaweza wakafaidika na fursa hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nimkumbushe Mheshimiwa Waziri jambo moja zuri. Mwaka 2009 Wananchi wa Kijiji cha Msata, Kata ya Msata, walitoa eneo lao wakawapa Chuo cha Usimamizi wa Fedha – IFM, mambo ya ajabu yakaanza hapo. Mwaka 2013 baada ya makelele mengi sana Chuo cha Usimamizi wa Fedha wakalipa fedha kwa ajili ya uendelezaji wa eneo lile, lakini toka mwaka 2013 mpaka leo, hakuna jambo lolote lilinofanyika katika eneo lile! Mji wa Msata umeendelea kukua na wananchi ambao walikuwa wamejipanga kwa ajili ya kufanya maendeleo wakipata *support* na chuo kile, wakaanza kukata tamaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiona kama Mbunge wao ndani ya Kitabu cha Hotuba ni maneno ya kwamba, sasa ndio mnajipanga katika mpango mkakati wa kuanza kuchora ramani ya eneo lile. Mheshimiwa Waziri binafsi nikwambie kuchoshwa kwa wananchi wangu kusubiri hicho,

lakini pia kuchoshwa kwa Chama cha Mapinduzi kwa ahadi ambazo zinaonekana kwamba, hazitekelezeki. Ninachomwomba Mheshimiwa Waziri kabla wananchi wale wa Msata hawajakikataa Chama chake kilichompa nafasi yeye kuwa Waziri wa Fedha, hebu aje na majibu mazuri ya kimkakati juu ya jinsi gani amejiandaa kuweka fedha kujenga majengo yale na maendeleo ya wananchi kuendelea kupatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini sio mwisho kwa umuhimu Mheshimiwa Waziri, ni ushauri juu ya mwenendo wa fedha katika Serikali yangu. Mheshimiwa Waziri tumeona katika lugha zinazosemwa kwa yeye na Serikali yangu, mara nydingi lugha inapozungumzwa ya maendeleo ni lugha ya kodi. Wameeleza wengi waliotangulia kwamba, watu sasa wamefikia sehemu wanafunga biashara wanapowaona Maafisa wa *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo mimi kwa usomi wangu mdogo natambua kwamba, ziko *means*nyingi sana za kuweza kujipatia fedha, mojawapo kuna vitu vinaitwa *Municipal Bond*, kuna vitu vinaitwa *Infrastructure Bond*, leo hii tunahangaikaje kuwaminya Watanzania maskini na wanaendelea kuumia wakati tunazo njia ambazo yeye kama msomi wa mipango anazijua vizuri na anaweza kuzisimamia vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano hatuoni sababu kwa nini miradi mikubwa kwa mfano kama hii ya Bwawa la Kidunda ambayo nategemea kwamba, ndio litatuletea maji na nguvu ya umeme katika maeneo yetu ya Dar-es-Salaam, Mkoa wa Pwani na maeneo mengine ya Tanzania, tunaendelea kukusanya hela kuititia nguvu za wanyonge wakati tunaweza kutengeneza taratibu ambazo zinaweza zikatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, katika maeneo mengi panapotoka matatizo ya kiuchumi Benki za Kimaendeleo zimekuwa ndio kimbilio. Tumeshuhudia wakifanya hivyo

Wajerumani, tumeshudia wakifanya hivyo Wajapani, lakini tumeshuhudia pia nchi mbalimbali ikiwemo Marekani jinsi ambavyo wameweza kuititia vyanzo mbalimbali na kuweza kukusanya pesa na kuweza kusaidia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo njia ambayo kiuchumi au kifedha wanaita *reveragies*, ambazo benki inaweza ika-*raise* hela mara tano ya kile kiwango ambacho kinatakiwa ili kusaidia kunyanya kiwango cha pesa kuweza ku-*finance* miradi mikubwa. Mheshimiwa Waziri ni kwa nini mpaka leo hii Wizara yake imeendelea kumshauri Rais wangu, imeendelea kuwaumiza Watanzania kuititia mianya ya kodi wakati tunazo njia kuititia *reveragies* ambazo zinaweza zikawasaidia kupata hela nyingi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri atakaposimama atuambie Watanzania, amejlipangaje kuweza kusaidia kunyanya fedha kwa ajili ya kusaidia miradi mikubwa ya Serikali, lakini pia kupunguza huu ugumu na machungu kwa wananchi wetu. Maana tunatambua tunayo Benki kama *TIB*, tunayo Benki kama *TADB*, hizi zote kama zitawezeshwa kuititia fursa hizi za ku-*raise* hela ambazo zinaweza zikasadia kupunguza makali kwa wananchi wetu nina hakika kabisa yale malengo mazuri tulioyahidi katika ilani tutaweza kuyafanikisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo Mheshimiwa Waziri nimpongeze tena yeye anavyoendelea kukamilisha na kusimamia shughuli mbalimbali za Wizara, malalamiko mengi ya wananchi yamekuwa katika kuangalia kwamba, huku Serikalini wanajidai, wanatamba kwamba, uchumi unaendelea vizuri wakati maendeleo katika mifuko ya wananchi yameendelea kuwa mabaya zaidi. Mheshimiwa Waziri namwomba sana tafsiri ya maendeleo, tafsiri ya uchumi, tafsiri ya maisha yaliyo bora kwa Watanzania ni maendeleo yanayofanana na hali halisi ya maisha wanayoishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono sana mipango hii, lakini namwomba Mheshimiwa Waziri

atambue kwamba, huko mtaani maisha ya wananchi ni magumu na malalamiko ni mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako. Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Kasuku Samsoni Bilago dakika tano ujiandae.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi. Nianze na kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia uzima na kuniwezesha kusimama hapa kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri na timu yake yote ya Watendaji kwa kazi kubwa ya kutafuta rasilimali fedha kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Ukusanyaji wa fedha ni jambo moja, lakini kutumia vizuri na kwa wakati ni jambo lingine ambalo ni muhimu zaidi katika maendeleo ya nchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo yanayotumia fedha nyingi tukiacha mishahara ya Watumishi wa Serikali, lakini asilimia zaidi ya 60 hadi 70 zinatumika katika manunuzi ya umma. Eneo hili limekuwa na changamoto kubwa sana tena kwa muda mrefu na kwa miaka mingi. Manunuzi ya umma hayaendani na thamani ya fedha ambazo zinatumika katika kununua bidhaa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni wakati sasa nilitarajia kuona katika taarifa ya Waziri pia, kwamba, tatizo hili ama changamoto hii ya muda mrefu imeweza kuangaliwa kwa kiwango gani na utatuzi wake ukoje kwa sababu ni eneo muhimu sana katika rasilimali fedha ambazo hatunazo katika nchi yetu ambazo zinatosha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Tunaiomba Serikali wakati inaanishaa iweze kutupa ni namna gani sasa inaenda kuhakikisha

kwamba, fedha zinazotolewa katika manunuzi zinakwenda sambamba na ubora wa bidhaa zinazotumika hasa katika maeneo ya ujenzi katika nyumba za Serikali zinazojengwa, na katika barabara, eneo ambalo limekuwa changamoto kwa muda mrefu sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Wizara ya Fedha. Tunaambiwa kwamba, takwimu zinasema hadi kufikia Februari, 2017 Wizara ilipokea shilingi triliioni 27.4 ambayo ni sawa na asilimia 3.5 tu ya fedha zote za maendeleo ambazo zimeidhinishwa na Bunge. Tena isitoshe katika hizo fedha triliioni 27 tuliona kwamba, triliioni 1.9 ni fedha za ndani na fedha triliioni 25.4 na zaidi kidogo ni fedha za nje. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunaona kwamba, hata Wizara ya Fedha yenye sehemu kubwa ya fedha inazotumia kwa miradi yake ni fedha za kutoka nje, hili ni suala ambalo kidogo ambalo halipendezi katika taratibu zetu za Serikali. Tunajua *uncertainty* za fedha za nje, fedha za wafadhili ambazo zinaweza zikakwama hapa na pale. Tunaiomba Serikali na kuishauri Serikali iweze kubuni mikakati mbalimbali ya kuweza *ku-raise* fedha za ndani, ili ziweze kutekeleza miradi yake ya maendeleo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima la mafungu ya Wizara ya Fedha. Katika Mafungu nane yaliyo chini ya Wizara ya Fedha, ukisoma taarifa ya Waziri ni Mafungu matatu tu yaliletewa fedha ambazo ziko zaidi ya asilimia 60, lakini asilimia 50 na kwenda chini ndio mafungu yaliyobakia, sasa hii ni hatari. Tunataka kujua pengine ni vizuri Waziri atuambie ni nini tatizo la Hazina kuchelewesha utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo ikiwemo miradi iliyo chini ya Wizara ya Fedha na hata miradi mingine ya miradi ya maendeleo katika nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imekuwa changamoto, wananchi wengi wanalamika kwamba, kwa nini Serikali na Bunge inaidhinisha fedha za kutosha, lakini hazifiki kwa

wakati na zinafika chini ya kiwangi kilichoidhinishwa na Bunge. Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 ipo sasa hivi, inaeleza kwamba ni vema fedha zilizoidhinishwa na Bunge ziweze kutolewa kwa wakati, ili miradi ya maendeleo iweze kutekelezwa kwa wakati. Hili limekuwa tatizo sugu, tunaiomba Wizara ya Fedha wakati inahitimisha ituambie ni changamoto gani ya Hazina kutotoa fedha kwa wakati, ikiwepo hata zile za kufadhili miradi ambayo iko chini ya Wizara ya Fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kupata ufumbuzi wa kuchelewesha fedha za miradi, nashauri kwamba Wizara hajafanya kazi kubwa zaidi katika ukusanyaji wa maduhuli. Ukusanyaji wa maduhuli ni jambo jema, ni jambo la muhimu sana, lakini pamoja na hilo la pili ni kuhakikisha kwamba, Deni la Taifa halipandi. Vilevile kuhakikisha kwamba, thamani ya shillingi yetu haishuki. Mambo haya matatu ambayo ni jukumu la Wizara ya Fedha ihakikishe kwamba, uchumi wa Taifa unapanda, sambamba na kuhakikisha kwamba, inasimamia maeneo haya matatu ambayo nimeyaeleza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia isimamie kikamilifu kushuka kwa thamani ya shillingi, hili nimelizungumzia na ninadhani hilo likisimamiwa vizuri tunaweza kuwa na maendeleo ya uhakika katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri, ukurasa wa 76, imeandikwa utaratibu wa mikakati ya kupunguza umaskini, inaeleza kufanya uchambuzi na tathmini ya miradi ya kuondoa umaskini ngazi ya Wilaya na vijiji. Sina hakika anamaanisha nini, lakini najua kulikuwa na MKUKUTA namba I,II na III ambazo hazikufanya vizuri sana katika nchi yetu. Pamoja na nia njema ya Serikali ya kuhakikisha kwamba inaondoa umaskini baina ya watu wake, lakini bado maeneo mengi, harakati nyingi ambazo zimeainishwa na Serikali katika kuondoa umaskini hayajafanya vizuri. Nitoe mfano mdogo tu wa asilimia 10 ambayo inatolewa na Halmashauri katika kuwapa mitaji wanawake na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa Halmashauri nyingi zinatoa hizi fedha kama kuondoa lawama, lakini ukiangalia kwa undani kabisa, ukienda kuulizia, hizi fedha hazijaonesha *impact* hata kidogo, haijulikani kapewa nani? Haijulikani riba ilikuwa shilingi ngapi? Haijulikani wamenufaika watu gani? Hata hivyo, Halmashauri zinaenda kutenga na kuzitoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali katika harakati mbalimbali za kuondoa umaskini, iweze kuangalia kwa undani, iweke utaratibu mzuri na hasa tunakoelekea kupata zile milioni 50 za kila kijiji, Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba kila mtu ananufaika na hizi fedha ili tuone umaskini unapungua katika nchi yetu kwa nia njema ya Serikali ya kuwezesha wananchi kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie njia ambayo mimi naiamini kwamba, kwa sababu suala la utoaji mikopo, naomba labda ku-*declare interest*, mimi nimetoa mikopo kwa takribani zaidi ya miaka 20 kwa watu maskini na kwa ufanisi. Hivyo, naomba pamoja na nia hiyo, lakini njia ambayo ina uhakika na endelevu ni kuwawezesha wakulima, kwa sababu mkulima anaweza akalima kwa kupata fedha kuliko mtu maskini ambaye anapata mlo mmoja kwa siku, ukamwambia chukua mtaji huu kafanye biashara, hataweza kufanya biashara, atazila hizo fedha na matokeo yake hayataonekana, lakini mkulima atachanganya shughuli yake ya kila siku, atalima na ukimhakikishia soko la uhakika kwa bidhaa zake anaweza akaondo tatizo la kipato chake, akapata mapato kwa ajili ya familia yake na hatimaye kuondoa umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo na ufugaji ndio sekta ambayo inagusa maisha ya watu wengi. Kwa hivyo, naona kwamba, Serikali ikielekeza uwezeshaji wa wakulima na wafugaji kuwapa mitaji ili waboreshe kilimo chao, si kwa namna ya mikopo yenye riba ambazo tunazona, pale ndio mahali ambapo tunaona Serikali itaweza kuondoa umaskini kwa uhakika baina ya wananchi wake, kuliko sasa hivi kuwapa mitaji ya mikopo ambayo hatuna hakika

inamlenga nani hasa, ikimlenga mtu ambaye ni maskini anayepata mlo mmoja kwa siku hatafanya kazi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Bashe, Mwalimu Kasuku Samson dakika tano na Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya dakika tano.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa. Kwanza nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha wote hai na salama, tulipata bahati ya kufika kwenye Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Mwenyezi Mungu atujalie tuweze kufunga kwa amani na utulivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze hotuba yangu na mchango wangu kwa maneno yafuatayo:-

Jukumu la msingi la Wizara ya Fedha kama Wizara ni *administrator* anayesimamia utekelezaji wa kitu kinachoitwa *Fiscal Policy*. *Fiscal Policy* ndiyo *instrument* inayotumika na Serikali kukusanya fedha na inayo-guide Serikali sehemu ya kutumia fedha hizo kwa lengo moja tu la msingi, kusaidia na kuchochaea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya tathmini yangu kwa kina. Leo tuna mwaka mmoja, nimekaa najiuliza maswali na naongea kwa polepole sana, nini dhamira ya wataalam walioko katika Wizara ya Fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamiaji na utekelezaji wa jambo hili una *vehicle* mbili tu, moja yenye dhamira ya

kupambana na mfumuko wa bei. Hapo ndipo Serikali itaweka kodi ili kupunguza *purchasing power* ya watu, lakini katika kuchochea uchumi nyingine ni Serikali kutumia Sera yake ya Kodi ili kupunguza sehemu mbalimbali wanazotoza kodi na kukuza uchumi na hasa pale ambapo biashara zinapokuwa chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamtolea mfano mlipa kodi mmoja mkubwa anaitwa *TBL*. *TBL* baada ya mabadiliko ya kodi ya mwaka jana, kodi anayolipa kwa Mwaka huu wa Fedha wa 2016/2017 tunaomaliza, imeshuka kwa bilioni 50. Huyu ni *TBL* kwa nini, kwa sababu ya *imposition of Excise Duty*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za Wizara ya Fedha zinaonesha kushuka kwa makusanyo ya kodi ya *PAYE*, taarifa ya makusanyo ya fedha ya Wizara ya Fedha inaonesha kushuka kwa *VAT on Import goods*. Taarifa ya *TPA* inaonesha kushuka kwa mapato kwa asilimia 13 ya bandari yetu, kwa nini? Kwa sababu ya *imposition* ya *VAT on transit goods*. Najiuliza swalii, wataalam wa Wizara ya Fedha wanafikiri nini? Mwalimu wangu wa uchumi yumo humu ndani, *I am not an economist*, lakini nimesoma *basics*, najiuliza wao wanatoa wapi hizi *thinking wanazo-impose?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa za Wizara ya Fedha biashara 7,700 zimefungwa nchi hii, ajira zimepotea! Najiuliza maswali, *what is the bottom line? Bottom line* ni kukuza uchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wa Wizara ya Fedha wameweka kodi maeneo mbalimbali kwa mwaka wa fedha na ukisiliza *business community* inalalamika juu ya *imposition* ya kodi nyingi zinazowekwa na Serikali na huoni dhamira ya Serikali kupunguza kodi hizi, huoni kabisa. *A large tax payer* ambaye ananunua mazao ya kilimo kutoka kwa Watanzania kama *TBL*, anaenda Serikalini anapeleka *proposal* ya kuwaambia jamani, mnavyoweka kodi hii mnapoteza fedha hizi na Serikali *at the end of the day* inapoteza kiwango hiki cha fedha! Alisema Mheshimiwa Serukamba hapa ni

Iazima Serikali ijue katika kila biashara ya kila Mtanzania Serikali ni *share holder* kwa asilimia 30, kwa sababu inachukua siku ya mwisho *corporate tax*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mifano michache, nimeitaja; *Domestic VATimeshuka, VAT on import imeshuka, domestic ya excise imeshuka, PAYE imeshuka, withholding tax imeshuka, corporate tax imeshuka! Where are they going to collect? Wapi?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba kaka yangu Mheshimiwa Mpango nilisema mwaka jana na narudia leo ndani ya Bunge hili. Naheshimu sana *his academic background, either kuna mambo mawili, kuna slow move ndani ya Wizara ya Fedha juu ya wataalam kuishauri Serikali sawasawa.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa za Wizara ya Fedha zinaonesha zimefunguliwa biashara mpya laki mbili, unajuliza swali biashara elfu saba zilizofungwa *impact* yake kwenye kodi zimeonekana. Hizi laki mbili zilizofunguliwa kwenye uchumi hazionekani, nashindwa kuelewa wapi tunataka kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niiombe Serikali kwa heshima kabisa, kuna njia mbili za kutengeneza bajeti, anao *large tax payer* wake Mheshimiwa Waziri, awaite awaambie kutoka wewe *TBL* anataka *corporate tax* ya *this amount* mwaka huu wa fedha amfanyie nini kama Serikali, atamwambia ili a-grow productivity yake atasema nipe *one, two, three, four, because the bottom line una-tap* mwisho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo vinywaji baridi wiki iliyopita *CocaCola Kwanza* imepunguza wafanyakazi 130. Jamani ninyi wataalam mliokaa huko nataka niwaambie jambo moja na niseme kwa kuwa mimi ni Mbunge wa Chama cha Mapinduzi, sitavumilia kutoka moyoni kuona *technical mistake* ambazo haziitaji *PhD*wala u-professor. *We will not allow this!* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Rais iko *very clear, ku-grow* uchumi wa nchi hii, kujenga viwanda, *ku-create ajira, hatuwezi ku-attain* namna hii. Nataka niwape mfano, ukisoma taarifa ya *Port Authority* ya Kenya mwaka 2014/2015 asilimia 1.4 ya mizigo ya Tanzania ilipita pale. Mwaka 2016/2017 asilimia 2.7 ya mizigo ya Tanzania imepita Mombasa, *ina-grow, maana yake wafanyabiashara* wanahama, wanaenda kupitishia mizigo yao kwingine, *why!* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *principal* ziko wazi, Serikali inakusanya kodi, haiwezi kukusanya kodi kwa watu maskini, haiwezi kukusanya kodi, nataka niwape mfano, Bunge liliopita Waziri wa Fedha alisema humu ndani Dkt. Mpango tutagawa *EFD machines* kwa wafanyabiashara Serikali haijagawa *to-date*, unajua kinachoendelea *site*, wafanyabiashara wameandikiwa barua waikopeshe Serikali hela.... (*Makofi*)

*(Hapa muda wa kengele ililia kuashiria muda
wa mzungumzaji kuisha)*

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako, muda wetu ndioyo huo.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Wahemishiwa Wabunge, niseme jambo moja, Serikali inaleta mapendekezo humu Bungeni ya kodi na tozo mbalimbali, Bunge ndilo linaloamua tusi-pass hiyo, Serikali inapendekeza. Tunaendelea Mheshimiwa Kasuku Samsom Bilago.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Naomba nianze kuzungumzia suala la Mkaguzi na Mdhibiti wa Fedha za Serikali (*CAG*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mdhibiti na Mkaguzi huyu amekuwa akifanya kazi ya kukagua fedha za Serikali miaka

nenda rudi, nilitaka kujua ukaguzi huu unalenga nini? Kama ukaguzi unafanyika na wanaofanya ubadhirifu wa fedha za umma hakuna hatua inayochukuliwa kuna sababu gani ya CAG kuendelea kukagua fedha. Kila mwaka tunaletewa taarifa kuna Halmashauri zenye hati chafu, sijui ripoti chafu lakini hakuna kinachofanyika. CAG ana kazi gani kama ripoti yake haiwezi kuwa na *impact*? Tunatenga fedha CAGafanye ukaguzi lakini akimaliza kukagua hatuoni madhara au hatuoni *impact* ya ukaguzi wake kwenye nchi hii. Lazima ifike hatua baada ya ukaguzi *what next*, nini kifanyike juu ya ripoti ile kwa ukaguzi mbovu uliopatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ukurasa wa 34 ambao Waziri amesema Ofisi ya Mdhibiti ya Mkaguzi Mkuu wa Fedha za Serikali ndiye yenye jukumu la kufanya ukaguzi wa fedha wa hesabu za Serikali. Sasa nataka kuuliza, nimepata taarifa kwamba CAG anakagua fedha za vyama vya wafanyakazi. CAG ameanza kukagua Chama cha Walimu Tanzania (CW) chama ambacho kimekuwepo tangu mwaka 1993 hakijawahi kukaguliwa na CAG na kule hakuna ruzuku ya Serikali, hakuna fedha ya Serikali yoyote iliyokwenda kule anakwenda kutafuta nini kule Chama cha Walimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi inanipa wakati mgumu sana. Tena vyama viko zaidi ya kumi na mbili, kumi na tatu ameendaje Chama cha Walimu kukagua ambapo vyama vya wafanyakazi vinakaguliwa kwa mujibu wa sheria, vinakaguliwa na Mkaguzi wa Vyama vya Wafanyakazi anayetambulika kwa Msajili ya Vyama vya Wafanyakazi. Huyu CAG amekwenda kufanya nini, kama siyo kuna jambo fulani mtu anafikiri limefanyika anamtuma CAG kwenda kukagua fedha ambazo zimekwisha kaguliwa na ripoti ya vyama vya wafanyakazi na fedha zote zinakaguliwa mwezi wa tatu na taarifa lazima ifike kwa Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi si zaidi ya tarehe 30 mwezi wa tatu. Leo CAG yupo Chama cha Walimu anakagua fedha. Naomba kujua hilo nipate majibu anatafuta nini kule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu Wazabuni kutolipwa. Serikali lazima ifike mahali ifahamu kwamba uzabuni ni biashara. Wazabuni ni wafanyabiashara! Kama Serikali inawakopa wazabuni, inashindwa kuwafanya waendelee ku-move na biashara zao ni makosa makubwa. Sambamba na hilo wapo watu *wali-supply* mbolea, pembejeo, waliosambaza pembejeo hapa nchini mpaka leo hajalipwa, wamefilisiwa na mabenki na wengine wamekufa kwa sababu ya kudaiwa fedha za pembejeo na benki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inakopaje watu binafsi? Nani mwenye capacity kati ya Serikali na mtu binafsi? Ifike hatua Serikali iangalie nani wa kumkopa na nani isimkope. Mnarudisha nyuma uchumi wa wananchi wanaojitolea kuitumikia hii nchi kwa *ku-supply* kabla ya kulipwa. Kwa hiyo, Serikali ifike mahali illipe wananchi hawa wanaotoa huduma Serikalini mapema iwezekanavyo wasiwarudishe nyuma. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la kuchagua tukubaliane, Serikali inataka kodi, inapenda kodi au inapenda machinga. Tumeruhusu machinga wamemwagika Kariakoo wanauzu mpaka milangoni mwa watu wanaotakiwa kutumia mashine ya *EFD*, matokeo yake bidhaa zinatoka kwenye maduka anapewa machinga anauza, mwenye duka hauzi kwa sababu tayari bidhaa zake ziko kwa machinga. Biashara inaendelea wala yule mtu wa dukani halalamiki kwa nini machinga yuko mlangoni kwake, kwa sababu anajua ye ye inamlipa. *EFD* mashine haitumiki kwa sababu ye ye hauzi. Bidhaa zake zinauzwa na machinga. Machinga halipi kodi. Ni nchi gani hii tunayokwenda? Halafu watu wamesimama tu wanaona machinga tunapenda machinga tunapoteza kodi za nchi hii, mwenye *EFD* pale Kariakoo halipi kodi, bidhaa zake dukani zinakwisha, wanapewa wamachinga.... (*Makofî*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa lkupa Alex..

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinitaja Lucy Owenya.

MWENYEKITI: Haya Mheshimiwa Lucy Owenya.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba nianze na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Mimi naomba niwaambie Mamlaka ya Mapato Tanzania ni lazima wawe marafiki wa wafanyabiashara, wao wanaona ni ufhari kwenda kuflisi wafanyabiashara, badala ya kutoa elimu unaenda kufunga akaunti ya mfanyabiashara, unaenda kufunga biashara yake, sasa ukishafunga biashara yake wale wafanyakazi hawatafanya kazi mnakosa *pay as earn* na mnakosa mapato. Naomba muwaelimishe, hata kama mnawadai wapeni muda walipe hicho mnachokitaka kwa muda lakini na biashara iendelee, mkizifunga zile biashara na ninyi pia mnakuwa mmekosa mapato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kuhakiki *TIN*sasa hivi unakuta watu wengi hawaendi kuhakiki *TIN*zao kwa sababu ukienda kuhakiki *TIN* unakutana na madeni. Haya yamezungumzwa na wengi, magari yamekaa zaidi ya miaka ishirini, wafanyabiashara unakuta unamurai mtu zaidi milioni 40 lakini mfanyabiashara anapeleka *returns* kila mwaka, hivi ni kwa nini *TRA* badala ya kukusanya hayo mapato unamwekea mtu deni mpaka linafika milioni 40 halafu ndiyo unakuja kumpa sasa hivi unamwambia aliye milioni 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu hii kodi ya *road licence* ingizwe kwenye mafuta na tozo itozwe kwenye magari ambayo yanatembea barabarani, badala ya ku- *frustrate* watu, kuna watu kule Moshi wamekufa. Utakuta mtu analetewa deni la milioni 200, kuna Mzee kweli kabisa amefariki pale Moshi hajui atalipaje hiso fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba ndugu zangu mjaribu kuwafanya wafanyabiashara wawe marafiki zetu na Waheshimiwa Wabunge muelewe kwamba hizi pikipiki mlizotoa kwa wapiga kura mna madeni mnadaiwa huko, hakikisheni mnaenda kubadilisha majina na waelimishwe watu wakiuba kifaa chake au ukimkabidhi mtu kifaa cha moto lazima abadilishe jina. Kuna siku 30 za kubadilisha lakini mtu akishauza lile gari hajui kama kuna umuhimu wa kubadilisha jina, badala yake mnakuja kumwaadhibu yule mtu aliyebadilisha jina mnawambia aliye lile deni nafikiri hii si haki na siyo sawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka naomba niulize kuhusu wale walipanda mbegu DECI, wale walikuwa ni watu waliojikusanya na kesi ilienda Mahakamani na ikaisha. Kuna zaidi ya shilingi bilioni 14 zimelela pale Benki Kuu. Nataka Mheshimiwa Waziri aje atuleze fedha zile zimeenda wapi au ndiyo mtindo wenu wa Serikali mnazitumia bila kuwaeleza, maana yake hapa tulichanga fedha za maafa Arusha tukasikia zinajenga mochueri Mount Meru. Kwa hiyo, hebu tuelezeni zile fedha ziko wako na ni lini mtawapa hawa walipanda mbegu fedha zao maana yake kuna wengine wameshafariki. Mheshimiwa Waziri akija ku-*wind up* atuambie ni lini watawalipa hawa walioewekeza fedha zao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie *EFD machines*. Sasa hivi sijui hizi *EFD machines* zinatumika wapi na wapi. Kwa mfano, Moshi mpaka wamachinga wanatumia *EFD machine* lakini hapa Dodoma maduka makubwa tu hawatumii *EFD machines* na mnajua kabisa mlisema wenyewe, Serikali ilisema itazitoa hizi *EFD machines* bure, hilo zoezi lilianza Dar es Salaam kwenye mikoa mingine ni lini mtatuletea hizo mashine ili wafanyabiashara wadogo wadogo na wao waweze kutumia hizi *EFD machine*.

Mheshimiwa Menyekiti, *EFD machine* moja inauzwa shilingi laki nane mfanyabiashara mdogo ni vigumu sana kutumia shilingi laki nane kununua hiyo mashine. Halafu zaidi ya hilo hizi mashine haziko *durable* zinaharibika haraka sana,

ukitengeneza mashine moja si chini ya laki moja mpaka laki moja na nusu. Sasa ni mfanyabiashara gani mdogo ambaye ataenda kununua mashine ambayo inaharibika kila wakati? Ukizingatia umeme wetu ndiyo huo ikiingiza *EFD machine* kwenye umeme inaweza ikaungua. Unakuta *EFD machine* zinaharibika kila wakati na inabidi ulipe hela kwa ajili ya kutengeneza hizo mashine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka njue utaratibu wenu ukoje. Ni watu gani wanaotakiwa kutumia hizi *EFD machines* na zinatumika sehemu gani Tanzania, maana yake kuwa Watanzania wanaokaguliwa kila siku na kuna Watanzania wengine wanakaa tu bila kuzitumia. Mheshimiwa Waziri wakati anakuja ku-*windup* naomba na hilo nalo atuelezee. . (Makof)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Ikupa Alex, Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Oscar Mukasa ajiandae.

MHE.STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Naomba niendelee kumshukuru Mungu kwa ajili ya muda huu, lakini pia niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais akisaidiwa na Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi ambavyo anaendelea kuitekeleza llani ya Chama chetu cha Mapinduzi. Pia naomba niendelee kumpongeza sana Waziri mwenye dhamana ya Fedha na Mipango pamoja na Naibu Waziri wake na timu nzima ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja naomba niongelee huduma kwa wastaafu. Napenda niipongeze Serikali kwa jinsi ambavyo imeboresha mfumo wa malipo ya pensheni kwa wastaafu wetu, lakini pia naungana na maoni ya Kamati kuhusiana na wastaafu ukurasa wa 21.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili nina ushauri ufuatao:-

Serikali ni kweli imeongeza kima cha chini kwa pensheni kwa wastaa fu wetu na kufikia laki moja. Kima hiki cha chini ukiangalia na uhalsia wa maisha ya sasa hivi ni kidogo sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali ama naishauri Serikali kima hiki kiendane na uhalsia wa maisha. Pia Serikali iangalie kwamba mtu anapokuwa mzee na gharama zinaongezeka. Ndiyo katika umri huu ama muda huu ambapo mtu anakuwa na magonjwa anahitaji kujitibia lakini pia anakuwa anahitaji ale hata lishe bora tofauti na mtu wa kawaida unaweza tu ukala ugali na maharage siku imepita lakini kwa Mzee anahitaji kula vizuri na anahitaji huduma za matibabu. Naomba Serikali iliangalie hili iendee kuboresha pensheni kwa hawa wastaa fu wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee pia msamaha wa kodi kwa wafanyabiashara wenyе ulemavu. Ikumbukwe kwamba watu hawa walio wengi ama walio wachache pia wameamua kujitao kwenye eneo la utegemezi na kuona kwamba wajishughulishe na biashara, aidha, wameona kwamba wasiwe omboomba. Kwa hiyo naiomba sana Serikali iondoe kodi kwenye biashara za watu wenyе ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niongelee suala la zima la kodi kwa vyombo vya moto vinavyotumiwa na watu wenyе ulemavu yakiwemo magari ama kama ni bajaji. Katika eneo hili naishukuru Serikali kwamba inatoa *exemption* kwa vyombo vile ambavyo vimefungwa vifaa maalum vinavyoonesha kwamba chombo hiki kinatumika na mtu mwenye ulemavu, ikumbukwe kwamba kuna mtu mwenye ulemavu mwingine ambaye anaendeshwa ama anasaidiwa kwa mfano ukichukulia mtu ambaye haoni, kwa vyovyote vile lazima ataendeshwa na mtu anayeona, sasa ukimfungia kifaa maalum, halafu atakitumiae hii inakuwa haiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali iangalie tu kwamba kama kifaa hiki kinatumika na mtu

mwenye ulemavu isiangalie kwamba lazima hiki chombo kiwe kimefungwa kile kifaa maalum kwa mtu mwenye ulemavu. Kwa mfano, mimi naendesha gari mwenyewe lakini gari yangu haina vife vifaa maalum ambavyo vinatumika na watu wenyewe ulemavu, kwa hiyo sasa nisinyimwe *exemption* kwa sababu tu ile gari hajafungwa vife vifaa maalum, naomba sana Serikali iondoe kodi kwenye hivi vyombo vinavyotumika na watu wenyewe ulemavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la *road licence* hata mwaka jana wakati nachangia bajeti hii nilongelea hilo pia. Serikali itoe msamaha wa *road licence* kwa watu wenyewe ulemavu. Kwa nini nasema hivyo kwa mfano mtu kama mimi natumia gari ambalo kwangu siyo *luxury* ni hitaji la lazima. Kwa hiyo Serikali inaponitoza kodi ya *road licence* kwenye gari yangu ina maana kwamba inalipisha ile miguu. Gari pale inasimama badala ya miguu ya mtu mwenye ulemavu ama inasimama badala ya hata macho kwa mtu mwenye ulemavu. Kwa hiyo, *road licence* iondolewe kwenye magari ama vyombo vinavyotumika na watu wenyewe ulemavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho na si kwa umuhimu natoa rai kwa Watanzania wenzangu, kumuunga mkono Rais wetu katika juhudzi za ulipaji wa kodi kwa kudai na kutoa risiti pale ambapo mauzo na manunuzi yanapofanyika. Kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu bado kuna wimbi kubwa la udanganyifu kwenye suala zima la kodi. Unaenda dukani ama kwenye kituo cha mafuta unadai risiti, mtu anakwambia mashine ni mbovu, ukipita tena siku nyingine anakwambia mashine ni mbovu. Hawa wafanyabiashara hizi mashine za *EFDwanazo* ila wanatumia hii ya kusema kwamba mashine ni mbovu kama ni njia ya ukwepajji wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hili, kuna wafanyabiashara wanakwepa ulipaji wa kodi kwa kudanganya kwamba mashine ni mbovu. Niwaombe sana Watanzania tuwe na uzalendo katika ulipaji wa kodi. Mambo mengi leo tunaona kwamba hayaendi kwa

sababu makusanyo yanakuwa si mazuri na ni madogo kwa sababu sisi wenyewe hatuwajibiki katika suala zima ya ulipaji wa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Oscar Mukasa na Mheshimiwa Emmanuel Papian ajiandae.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niungane na Waislam wote nchini kwa kuwataki mfungo mwema katika mwezi huu Mtukufu. Naomba mchango wangu nimtangulize Mwenyezi Mungu. Nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Makatibu wote wa Wizara pamoja na Watendaji wa Wizara kwa kutuletea hii bajeti ili tuweze kuijadili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Benki ya Wanawake. Tanzania ina mabenki mengi lakini Benki ya Wanawake ni benki pekee ambayo ina wateja karibu asilimia 74 ya wateja wote. Sisi wanawake tunao wajibu mkubwa kabisa wa kuipigania benki hii. Mwaka 2010 Serikali ilitoa ahadi ya kutoa ruzuku ya shilingi bilioni 10 kwa miaka mitano yaani itatoa bilioni mbili kila mwaka katika Benki ya Wanawake lakini toka ahadi hiyo ilipotolewa ni shilingi bilioni 5.75 tu ambayo imetolewa mpaka sasa hivi. Je, hizi bilioni 4.25 Serikali itatoa lini? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu benki hii tumeona inakuwa ikifanya kazi vizuri sana, karibu mikoa sita sasa hivi imefungua madirisha lakini bado ina kazi kubwa kuhakikisha kwamba benki hii inafungua madirisha katika mikoa yote ili wanawake wote waweze kupata haki ya kupata mitaji kama ambavyo Serikali ilitaka, kwamba

wanawake waweze kupata mitaji kupitia benki hii ya wanawake. Sasa nitaomba labda wakati Waziri anahitimisha atueleze na asipoeleza vizuri itabidi tushike shilingi ya mshahara wake ili wanawake wote nchini waone kwamba benki hii inatendewa haki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee pia kuzungumzia kuhusu *TIB* (*Tanzania Investment Bank*), naunganana mkono na wote waliosema kwamba upo umuhimu wa benki hii kupewa mtaji wa kutosha kwa sababu ndio benki pekee inayosaidia kuleta kwa haraka zaidi maendeleo ya nchi hii. Tanzania inaelekea kwenye uchumi wa viwanda lakini bila kuiwezesha benki hii tutapata shida sana, kwa sababu ndio pekee itakayosaidia kuwezesha miundombinu ya viwanda. Serikali iliahidi kuipatia mtaji shilingi bilioni 500 na tena iliahidi kutoa trillioni tatu lakini ilipatiwa shilingi bilioni 150 tu. Sasa niombe Serikali itakapokuwa inajibu itueleze nini mkakati wa kuhakikisha benki hii sasa inawezeshwa ili huu uchumi wa viwanda uweze kwenda kwa kasi zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Naipongeza sana mifuko hii kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanya katika jamii yetu kama ujenzi wa daraja la Kigamboni, ujenzi wa majengo ya *UDOM* na kadhalika. Niombe Serikali ilipe madeni ya mifuko hii ili iweze kuendelea kuisaidia jamii na Serikali pia. Kipekee naomba nichukue nafasi hii kuishukuru *LAPF*, *NSSF*, *PPF* na Shirika la Bima (*NIC*) kwa kuniunga mkono katika programu yangu ya ukarabati wa majengo kongwe kwa shule za msingi katika Mkoa wa Iringa. Niombe na mifuko mingine basi iendelee kutusaidia ili kuendelea kusaidia jamii zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alisema mifuko hii sasa hivi ianze kuwekeza katika viwanda ili isaidie pia na kuongeza ajira nchini. Pia nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama alipokuja Iringa kutembelea kinu cha *National Milling* alisema kwamba *NSSF* itatoa mtaji. Najua kwamba ikitoa mtaji katika kile kinu itasaidia pamoja pia na kupata soko kwa wakulima wetu wa Iringa vilevile kuongeza ajira katika mkoa wetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuzungumzia kuhusu madeni ya wazabuni. Naipongeza Serikali kwa kuanza kulipa madeni ya wazabuni kiasi cha shilingi bilioni 796 katil ya deni la shilingi triliuni tatu iliyokuwa inadaiwa, lakini bado wazabuni wengi sana wakimemo wa Mkoa wa Iringa wanaidai Serikali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali ingetangaza katika gazeti ili wazabuni waliohakikiwa na wale waliolipwa madeni waweze kujua, kwa sababu kuna wengi walikuwa wanaidai, lakini hawajui hatma ya madeni yao mpaka leo hii, kama yatawekwa wazi angalau hata sisi tunapokwenda kwenye mikutano maswali yanapungua, wanakuwa wanajua kabisa hatma ya madeni yao ni yapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielezee kuhusu Ofisi ya Ugaguzi (*CAG*), kwanza nipongeze kwa kazi nzuri ambayo imekuwa ikiifanya, ofisi hii inafanya kazi nzuri sana lakini changamoto kubwa ni utekelezaji wa ushauri wa mapendekezo yanayotolewa katika ripoti yake. Bado Serikali hawajaweza kuyafanya kazi yale mapendekezo ambayo yanatolewa. Vilevile wapewe fedha ya kutosha, kwa wakati na waweze kukagua mapema ili kusaidia nchi yetu panapokuwa na matatizo, tuweze kujirekebisha halafu tuendelee mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu *TRA*; *TRA* imekuwa ikifanya kazi nzuri sana tu lakini nafikiri sasa hivi wafanyabiashara wale wadogo wadogo wamekuwa wakikadirisha kodi kubwa sana hata wale wakubwa kiasi kwamba wanashindwa kufanya biashara zao vizuri. Vilevile kuna utaratibu wa kumkadiria kodi mtu anayetaka *T/N* ya biashara, anatakiwa aliye kadirio hilo kabla hata ya kuanza biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limekuwa ni tatizo sana, watu wengi wanakwepa kuomba *T/N* kwa sababu wanakuwa wana mitaji midogo, sasa akijua kwamba akienda pale atatakiwa akadiriwe ile kodi yake kabla hata

hajaanza biashara halafu baadaye tena ndio alipie anashindwa kujisajili. Sasa ningeomba Serikali iangalie kwa sababu shida yao ni kurasimisha hizi biashara ili kuweza kupata kodi kwa urahisi zaidi, lakini sasa hii itasababisha biashara nyangi kutorasimishwa, watu wanaogopa kwenda kuzirasimisha kwa sababu wanatakiwa walipe kodi hata biashara zao hawajui kwamba watazifanyaje. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna utaratibu wa kumtaka mfanyabiashara aambatanishe *invoice* ya madai kwa mtu aliyempatia huduma kabla hata yeye hajalipwa. Ukitolea tu mfano wale wazabuni wanaofanya kazi na Serikali utakuta kwamba wanapeka *invoice* lakini kuja kulipwa madeni inachukua muda mrefu sana. Sasa *TRA* wanataka uambatanishe na ile *invoice* ya risiti wakati hata bado hujalipwa. Hili pia ningeomba Serikali iliangalie na iweke utaratibu mzuri wa kumsaidia huyu mfanyabiashara ili aweze kufanya biashara yake vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lingine, utaratibu wa kutaka wafanyabiashara kununua hizi *EFDs*, nafikiri wenzangu wengi sana wamesema. Mfanyabiashara anakuwa na mtaji kidogo sana, sasa anapokwenda kununua hii *EFD* tayari mtaji wake unakuwa umeathirika. Kwa hiyo, hata hii niungane na wenzangu kwamba Serikali hebu iangalie uwezekano wa *EFDs* mashine ziweze kutolewa bure. Nakumbuka hata Mheshimiwa Rais alishawahi kutoa ushauri kwamba *TRA* wawapatie hizi *EFDs* mashine wafanyabiashara wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie tu mfano kama *TANESCO* utakuta *TANESCO* wanakufungia ile mashine yao kwa hiyo inasaidia, inapunguza hata gharama za kufuatilia. Hii ni kwa sababu tayari mtu anakuwa amefunga ile mashine na hata ile kodi inayokadiriwa sasa inasaidia, kwamba unalipa kweli kodi halali, lakini si kama wanavyokadiria kodi kubwa wakati pato unalopata sio. Kwa hiyo, naomba hizi *EFDs* ziweze kupatiwa bure kwa wafanyabiashara wote, hata Mkoa wa Iringa bado hatujapatiwa hizi mashine za *EFDs*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna lile la *tax clearance* kwa mfanyabiashara anayedaiwa kodi. Naona kama sio sahihi kwa sababu utakuta mfanyabiashara huyu, wengi sana wamefunga biashara zao sasa hivi kwa sababu ya hizi *tax clearance*. Hii ni kwa sababu wamekadiriwa kodi kubwa ambayo kwa kweli hailipiki na hawa wafanyabiashara wamekuwa wakifanya biashara bila kupata faida. Utakuta huyu mkadiriaji bado hajaangalia na bado hajamsikiliza huyu mfanyabiashara matatizo makubwa ya kibiashara anayoyapata. Sasa hivi wengi wamekopa benki na utakuta wengi wao bado wanaidai Serikali na wengi wao bado wana matatizo makubwa kwenye biashara zao. Kwa hiyo, ningeomba Serikali iangalie sana hawa wafanyabiashara kwa sababu ni sawasawa na ng'ombe... (*Makof!*)

(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kuisha)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Papiani atafuatiwa na Mheshimiwa Saul Amon na Mheshimiwa Flatei ajiandae.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinitaja Oscar Mukasa halafu umeniruka sasa hivi, ilikuwa baada ya Ritta Kabati.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mukasa, Mheshimiwa Emmanuel Papian na Mheshimiwa Saul Amon.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Awali ya yote namshukuru Mungu kwa afya. Pili nawatakia kila la kheri ndugu zetu Waislam ambaao wameanza mwezi Mtukufu. Pia nataka kuwapa pole wananchi wa Biharamulo kwa adha inayoendelea huko, sasa hivi ni vurugu tupu baina ya wafugaji na wakulima baada ya hii habari ya mifugo kutolewa hifadhini bila mpango, lakini hiyo tutaisema baadaye. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwa maana ya hotuba nataka kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu Waziri na timu nzima kwa sababu kuna kazi wamefanya ndio maana tupo hapa, vinginevyo tungakuwa hatuvezi hata kujadili, kwa hiyo nawapongeza kwa kazi, lakini tunayo mambo ya kusema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, nitakwenda haraka haraka kwa sababu ya muda nina mambo kadhaa. Ukarasa wa 73 wa hotuba Wizara inazungumzia mafanikio kwa mwaka uliopita na moja ya mafanikio hayo ni kupunguza madeni ya wazabuni na wakandarasi. Wamesema wengi sana waliotangulia, lakini nataka kuweka msisitizo hapa, tunaomba Wizara iwatazame hawa wazabuni na wakandarasi kama sehemu au kama mawakala ambao mbali na kufanya kazi zao ndio wanatusaidla kuwezesha mzunguko wa pesa huko kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, mama mmoja ambaye ndiye analisha shule zetu za sekondari karibu 20 zote pale, huyo ni mfano tu, wako wengi pale wafanyabiashara wa Biharamulo wanaodai pesa na sasa wanaelekea kafilisika. Huyu namchukulia kama mfano, analisha shule lakini hivi tunavyozungumza anaidai Serikali milioni kama 400, imefikia hatua sasa mabenki yanataka kukamata magari yake, lakini watu binafsi wengine ambao wameshamsaidia wao tayari wamekamata magari na rasilimali, amesimama kabisa, yaani ni muda siyo mrefu tunamuingiza kwenye umaskini, tunamaliza mtaji wake wakati ni mtu yeye na wenzake wanashiriki kuwa kama mawakala wa kutusaidia kuzungusha pesa pale, akilisha watu 20 kuna watu anawaajiri pale kwenye kiwanda chake, wanabeba mahindi wanapeleka kwenye mashine, wanapakia kwenye gari, wanasambaza, ni ajira zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa hatumtazami yule mfanyabiashara peke yake, tunatazama mzunguko mzima. Tunaomba mlipe uzito ili haya madeni tuyalipe hata kama hamuwezi kulipa yote angalau sasa

naomba Mheshimiwa Waziri tuone namna gani kila mmoja angalau anapunguza ule mzigo ili magari yake yaruhusiwe, mashine zake ziruhusiwe kuendelea, vinginevyo anasimama kabisa na wote waliomzunguka ambao wanapata uchumi kupitia ye ye wanasmama kabisa, hilo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimeangalia ripoti moja hapa ya Benki Kuu inazungumzia *annual growth of banks credit to major economic activities*, mengi yamesemwa pale katika chati mojawapo. *Interest* yangu iko kwenye habari ya kilimo, inaonesha mwezi wa Tatu mwaka huu *growth* ni *minus 9.2* ukilinganisha na *11.2* chanya ya mwaka jana mwezi wa Tatu mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ikanikumbusha nilkwenda siku moja Benki ya Kilimo pale, nimepekela kampuni moja ya binafsi ambayo tunataka itusaidie kushughulika na wakulima wa Biharamulo. Benki ya Kilimo wanatuambia tuna mikoa kadhaa ya kuanzia Kagera haimo, sasa nikawa nashangaa ni namna gani sasa! Hili ndio jambo ambalo linakwenda kushughulika na Watanzania asilimia 80 ambao ndiyo wakulima lakini bado tunalifanya kwa maeneo madogomadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie hapo namna gani wale ambao tuna nia ya kuleta watu watusaidie kwenye uwekezaji wa kilimo tutasaidiwa, kwa sababu benki hii wanatuambia kuna maeneo wanaanza mengine tusubiri. Tusubiri wakati hii ndio ajira ya asilimia 80 ya watu wetu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, nataka kugusia kidogo habari ya sekta binafsi, MKURABITA, Hernando De Soto alisema nafikiri ni 2003 kama sikosei mwanzoni mwa 2000 kwamba asilimia 98 ya *business transaction* kwenye nchi hii zinafanyika nje ya mfumo, kwa hiyo hazilipi kodi na asilimia 90 kama sikosei, *figure* hizo nitaangalia vizuri, za *land property* (mali ardhi) iko nje ya mfumo hailipi kodi. Hilo tulishalifanya uchambuzi kwa kusaidiana na Hernando De Soto ndio ikazaa MKURABITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, mbona hatuoni mrejesho wa kila tunavyosoma bajeti wa namna gani sasa, MKURABITA imeondoa kwa mwaka mmoja idadi kadhaa ya Watanzania waliokuwa nje ya sekta inayotambulika imewaingiza kwenye sekta, hivyo, hata Waziri wa Fedha atuambie kwa kuingiza hawa sasa tumeingiza nguvu ya kikodi ya kiwango fulani ili mtu akiweza kufuatilia kwa miaka mitano tunaona tunakwenda wapi, naomba maelezo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la nne; wenzangu wamegusia, kuna habari ya kukusanya kodi, habari ya kupeleka hela kwenye Halmashauri lakini kuna habari ya kasi ya kuzitumia. Nina mfano mahususi hapa, tuliomba pesa kwa ajili ya maji ya Biharamulo Mjini kutoka Wizara ya Maji, tunashukuru wametupa milioni 200 mwezi wa Kwanza, mpaka leo tunavyoongea mwezi wa Tano huu unakwisha mambo yanakwenda taratibu kama kinyonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza leo na *RAS* wa Kagera na mtu wa Mamlaka ya Maji Bukoba Mjini, anasema mwanzo kulikuwa na ubishani kati ya Watendaji wetu wa Halmashauri na Mkoani, kwamba Halmashauri wanataka wafanye wao, hawa wanasema haiwezekani hizi hela zitapotea. Hiyo process tu ya kubishana imetumia miezi miwili. Tunaomba Waziri aje na mfumo ambao pamoja na kuzipeleka na kuzisimamia kwa maana zimefanya nini, tuwe na mfumo wa kutazama kasi ya kuzitumia kwa sababu inachangia sana kwenye kukwamisha maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano, nimesoma hotuba ukurasa wa 76, tunasema moja ya majukumu ya Wizara; kuweka utaratibu wa mikakati ya kupunguza umaskini, kufanya tathmini ya miradi ya kuondoa umaskini ngazi ya Vijiji na Wilaya. Hii sasa naleta habari ya ng'ombe na mifugo kule kwenye hifadhi, kwenye muktadha wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza kilio cha wafugaji Kanda ya Ziwa na jana nilikuwa Biharamulo ni kwamba tunavyozungumza ng'ombe 11,000 wametaifishwa

kwa maana ya kwamba tunawaondoa kwenye hifadhi kwa sababu hawastahili kuwa kule, sina tatizo na hilo. Mimi sio mmoja wa Wabunge wanaotaka ng'ombe wakae hifadhini, lakini swali langu ni kwa nini hatuoni hii kama ni fursa ya kiuchumi? Kwa nini hatujaribu kukaa na wafugaji na wakulima tukawaonesha fursa tulizonazo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi nimewahi kusema hapa, nimesaidiwa na *UNDP* wamefanya tathmini ya uwekezaji kwenye Wilaya ya Biharamulo baada ya kutuambia kwamba sisi ni maskini wa pili. Wakasema mambo mengi lakini nitasema moja tu, asilimia 54 ya eneo letu liko kwenye hifadhi, asilimia 46 ya eneo letu ndio la uzalishaji, lakini hilo asilimia 46 asilimia kubwa ya kutosha ni *underutilized*, hatujapanga, ardhi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza na Mifuko ya Hifadhi, dada yangu Mheshimiwa Jenista hapa nataka nimshukuru sana, akatukusanya mpaka Mifuko ya Hifadhi, wakaja viongozi wa Chama cha Wafugaji, wakakaa wafugaji wako tayari, tumefanya tathmini kuna mifugo kama milioni moja kiwango cha chini. Wakasema kila kichwa kichangie elfu 50 tukaona hiyo bilioni 50, tuungane na Mifuko ya Hifadhi tutengeneze viwanda kule, tutengeneze ranchi ndogo ndogo kwa sababu ripoti zinasema tuna *underutilized* ardhi yetu, tuwaondoe kwa namna ambayo hawatakaa kwenye hifadhi lakini hawataleta vurugu kwa kuwatoa kwenye hifadhi kuleta Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza Biharamulo hatukuwa na migogoro ya wafugaji na wakulima lakini leo badala ya akili ya Mbunge na akili ya watu wengine kuwekeza kwenye kutafuta uwekezaji tunawekeza kwenye kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo haikuwepo. Nimwombe Mheshimiwa Waziri amesema kwenye ukurasa wa 41 habari ya ubia wa sekta binafsi mpaka wana Tume maalum, watusaidie sasa. Wakati maliasili na kilimo hawajalionia hilo au wanalionia, lakini wanakwenda taratibu waje wao na jicho la uwekezaji ili tukatatue mgogoro wa wafugaji, hifadhi na wakulima kwa jicho la uwekezaji

kwa sababu inawezekana, wafugaji na wakulima wapo tayari lakini sisi viongozi ndio tunawagombanisha kwa kutofanya kazi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 75, Mheshimiwa Waziri ameongelea majukumu ya Wizara ya kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera ya uchumi, ndio mambo haya. Uchumi tusiuangalie huku juu tu, twende huko Wilayani watusaidie, tunazungumzia kuondoa umaskini lakini Biharamulo leo tunaongeza umaskini. Mimi pale sasa hivi hotuba pekee ninayopaswa kutoa pale ni kuzungumzia mifugo tu, siwezi kuongelea maji, siwezi kuongelea nini, kuongelea wakulima na wafugaji. Hebu... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Emmanuel Papiani, Mheshimiwa Saul Amon na Mheshimiwa Flatei Massay.

MHE. EMMANUEL P. JOHN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze Waziri kwa hotuba yake aliyoitoa ambayo inaweza kutusogezza na ikatufikisha mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nataka kusema *TRA* imefanya kazi nzuri, sasa hivi tunaona kuna mahusiano mazuri kuliko nyuma ambako kulikuwa na maneno mengi, vurugu na wafanyabiashara, mvurugano na kukimbizana, sasa kunaonekana kuna lugha ambayo ni mahusiano mazuri yanayofanya watu kulipa kodi kwa usahihi lakini pia kwa mahusiano mazuri ya lugha na wanafanya vizuri zaidi kuliko kipindi cha nyuma ambacho kulikuwa na mivutano mikali baina ya wafanyabiashara na watoza kodi wetu. Hilo ni jambo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kuna hii Benki ya Kilimo, benki hii tunadhani sasa ndio wakati wake, Awamu ya Nne imejitahidi imeanzisha benki hii, lakini

tunaomba Serikali basi ione namna gani ya kuiongezea mtaji. Kuna fedha za nje, Nchi kama za China, leo China tunasema ni marafiki zetu wakubwa sana wa kihistoria kwa nchi yetu, kwa nini benki za China Serikali isikope kwa riba nafuu ikaletea pesa Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo ikaipa mtaji wa kutosha ikaisimamia hii benki ikaenda kwa wananchi wetu ambao ndio asilimia 80 ya Watanzania ambao wanajihuisha na shughuli za kutafuta maisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuimarisha benki hii na kuipa mtaji unasaidia watu wengi kuwa kwenye wigo mpana wa kufanya kazi na Watanzania wengi watakapofanya kazi Serikali itaweza kukusanya kodi ya kutosha. Niishauri Serikali ilitazame hili, ilifanyie kazi na ihakikishe kwamba hii benki inapata mtaji kwa kipindi kisicho kirefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hizi benki za blashara, hizi benki sasa hivi zina hali ngumu, zimekopesha watu, watu wameshindwa kurejesha mikopo kwa sababu ya kipindi kigumu, uwezo wa kushindwa kulipa kwa watu umeongezeka, lakini benki hizi zilikuwa na nia njema kwa sababu zimekopesha wakulima ambao hata mahali ambapo kilimo kimeshindikana kwa sababu ya mvua zikajaribu ku-*risk* zikakopesha hao watu, watu wame-*default*, sasa benki na zenyewe zinakwenda kuanguka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yawezekana hizi benki za biashara; *CRDB, NMB*, zina *defaulters*, mikopo mingi inachechemea. Tunaomba basi Mheshimiwa Waziri na Gavana watazame hili waone huruma mahali ambapo wamekosea, basi warudishe nyuma kidogo, wasamehe kwa sababu wanaoumia ni wengi Watanzania wetu wanaolipa kodi, basi tuone ni namna gani wanaweza kusonga mbele. Vinginevyo, wakiendelea kukandamiza sana kwa hali ilivyo sasa tutapoteza watu wengi kibiashara, tutapoteza kodi kubwa sana lakini pia na nchi itayumba *economically*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ione huruma hivi vyombo vyetu vya fedha mahali vilipokosea basi

wawasamehe, wakae chini mezani wawape *guidelines* za kufanya kazi, wawape muda, waone ni namna gani wanaweza kusonga mbele, lakini wawalinde kwa sababu na wao walikuwa ni sehemu ya kuchangia uchumi kwenye nchi yetu. Maana hizi *defaulting* zote zinazoenda ku-*appear* ni kwamba bado Serikali na yenyewe inaendelea kupoteza mapato. Sasa ili twende pamoja, kwa sababu tunawahitaji, Serikali tunahitaji isipoteze, hizi *institutions* tunahitaji zisife wala kutetereka kwa sababu nchi inaweza ku-*shake*. Sasa ili tufikie hapo, basi tunaomba Serikali ishushe mkono, itoe huruma, itoe maelekezo, iangalie ni namna gani hivi vyombo vinaweza kuendelea kufanya kazi bila mvutano wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Benki ya *TIB* ambayo ni benki ya Serikali. Tunaomba Serikali iione na iipe mtaji kama nchi nyingine zinavyokuwa na benki za Serikali ambazo zinapewa fedha na kuzisimamia ili benki hizo zisife.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la milioni 50 kila kijiji. Kwenye Wilaya yangu tumekaa tukafikiri tukajipangia, tukasema ngoja tuisaidie Serikali. Mimi namsaidia Mheshimiwa Waziri. Wilaya ya Kiteto tuna vijiji 63, hivi vijiji ukitaka kuniletea milioni 50 kila kijiji ataniletea 3,150,000,000, mimi hizi zote asiniletee, sizihitaji kwa sababu Tanzania ni kubwa, Kiteto ni Wilaya katika Wilaya mia moja na kitu za Tanzania, namwomba milioni 500 tu. Hii naomba ifanyike kwa nchi iwe ni *pilot study*, watu waje wajifunze, waone ni namna gani tutakavyotumia hizi pesa zikaenda kuzunguka kwa watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejjipangia sisi tuna mpango wa *VICOBA* Wilaya nzima. Wilaya ya Kiteto inaenda kuwa Wilaya ya kwanza kwenye mfumo wa *VICOBA* ambapo pesa ya wale wanachama haipotei na mfumo ule haupotezi pesa, watu wanajilinda wenyewe. Akinipa milioni 500 mwezi wa Nane ikaanza kuzunguka kwenye *VICOBA* katika vijiji kumi tu, nifikapo mwakani mwezi wa Nane nitakuwa nimeshakwenda zaidi ya vijiji 40. Kwa maana ya kwamba zile zitakazokusanywa tunazielekeza kwenye vijiji vingine, kwa maana hiyo pesa itakayozunguka pale tutakapofika 2020

nikisimama kunadi llani ya CCM tulioyahidi mimi na Mheshimiwa Waziri huko kwa wananchi, nitakuwa nimesha-cover vijiji vyangu vyote 63 kwa hiyo pesa ya milioni 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atakapokuja naomba anipige tafu anipe hiyo ahadi ya milioni 500, anipe mimi na Wilaya nyingine Tanzania zitakwenda kujifunza pale ili tuweze kurudisha pesa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Waziri mbele yake, hizi pesa akinipa ifikapo 2020 namrudishia 500 ya kwake na wananchi wangu watakuwa wameshapata kazi na Serikali itakusanya kodi kubwa maana hawa wananchi hizi milioni 500 wanapokwenda kufanya kazi, watafanya kazi..... (*Makof/ Kicheko*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Papian kwa mchango wako.

MHE. EMMANUEL P. JOHN: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

MHE. SAUL H. AMON: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Wizara ya Fedha. Kwanza nimshukuru Waziri wa Fedha kwa kuwasilisha bajeti yake, mimi nina mambo mawili makubwa. Wakati wa kukusanya kodi, kodi ni sawa na biashara nyingine yoyote lakini hapa kuna vikwazo ambavyo wafanyabiashara wengi tunavipata na kama Waziri hajalisikia hilo atume timu yake kwa wafanyabiashara, hasa wanaoingiza mizigo kutoka nje. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna huu mfumo wa *TBS*na tukiangalia kwamba nchi ya Tanzania sio nchi yenye viwanda kwa kiasi kikubwa na wafanyabiashara wa Tanzania sio wakubwa wa kila mmoja kwenda kutafuta kiwanda chake cha kuleta mizigo. *TBS* kuna tatizo, hasa la

ile faini ya asilimia 15 ya *invoice value* ya mzigo anapoleta hapa Tanzania. Hilo ni tatizo kubwa sana ambalo naomba Serikali kwa kupitia Wizara ya Fedha ililangalie upya ni namna gani wanafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna Wizara mbili, kuna Wizara ya Afya kupitia *TFDA* kwa mambo ya vyakula na dawa na *TBS* ambayo inafanya sehemu zote. Hata hivyo, utaratibu wa *TFDA* ni mzuri, unaeleweka, pamoja na kwamba ni ghali, unakwenda unasajili bidhaa zako hapa Tanzania na wanakupa *certificate*. Ukipishapewa mara moja huna usumbufu tena baada ya hapo, kwa hiyo *TFDA* hawana matatizo ukishasajili bidhaa zako, lakini *TBS* tazito lake ambalo linawafanya Watanzania wengi wasiweze kuingiza mizigo, Watanzania wengi wapite porini ndiyo maana unasielia, Mheshimiwa Bashe ameongea hapa kwamba watu wanapita Kenya, wanapita Kenya kwa sababu ya kuikimbia *TBS*, wanaingizaje, haijulikani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* wangechukua mfumo wa *TFDA* nina uhakika kwamba ingepunguza usumbufu mkubwa sana, kwamba mimi nilete bidhaa zangu, *TBS* wazikague kwa sababu viwanda vinavyotengeneza mizigo inayopita *TFDA* ndiyo hivyo hivyo vinavyotengeneza kupita *TBS*, lakini *TBS* kila unapoingiza mizigo unakuwa na *certificate* yake. *TFDA* wakikusajili utaisajili tena hiyo mizigo yako baada ya miaka miwili, unakuta usumbufu wa *TFDA* unakuwa haupo lakini *TFDA* anakwambia chakula ingiza, unaingiza *TBS* anakwambia hujasajili na kama hujasajili *TBS* ulipe asilimia 15 ya *invoice value*. Kwa kweli imewafanya wafanyabiashara wengi sana wawe na manung'unico.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri na timu yake awaulize wafanyabiashara nini kikwazo kikubwa cha biashara. Kama anavyojua tunavyoingiza mizigo ndivyo tunavyoweza kuuzia nchi nyininge za jirani, na ukiuzia nchi nyininge za jirani tutapata faida si moja tu kwa ajili ya kuingiza mizigo, kwanza wanakuja kuchukua mzigo, wanakuja wanalala, wanatumia usafiri wa nchi wa ndani wa kwetu

na mambo mengine, akina mama lishe wanapata vyakula, wanapata hela. Kwa hiyo kupitia *TBS* kwa kweli hilo ni tatizo kubwa sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba Serikali iliangalie hilo, kwa nini kazi za *TFDA* zisiwe za kwake. Tumepita nchi nydingi, ukiangalia Nigeria, Marekani na kwingineko, ukiambiwa kwamba hawa wanashughulika na mambo ya vyakula na dawa ni Wizara nydingine na ambao wanashughulika na mambo ya viwango ni Wizara nydingine na viwango vingekwenda kwa viwango na *TFDA* wangeendelea na kazi yao ya kukagua kwamba hivi vyakula na madawa viko salama kwa mlaji. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini mapato ya nchi yataongezeka, watu watapungua. Kwa sababu ukiangalia *TRA* hakuna usumbufu kabisa kama ilivyokuwa zamani, ukiangalia bandarini hakuna usumbufu kama ilivyokuwa zamani lakini ukifika unakwama, kwa sababu sisi wafanyabiashara wa Tanzania wengi ni wadogo, ni watu ambao hatuna mitaji mikubwa, tunavyoenda kununua mizigo iwe ni Ulaya, iwe ni Marekani, iwe ni China au Dubai, tunachanganya, hivyo huwezi kupata na usumbufu wake ni mkubwa mno. Wakati unanunua mizigo utachukua zaidi ya wiki sita ili kupata *certificate* ya *TBS*. Hilo naomba waliangalie walipe umuhimu wa hali ya juu, watu wanatoroka na mizigo kupita sehemu nydingine kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hapo Mheshimiwa Waziri amenielewa na kama nilivyomwambia, sehemu nydingine zake zote ziko sawasawa; *TRA* ambako watu walikuwa wanaogopa pako sawasawa, vitu vinakwenda sawasawa wala ndani hatuingii. Ukienda *TFDA* unakwenda na *certificates* zako nimeleta mzigoo huu, hatusumbuliwi, unapewa *invoice*. Hata hivyo, ikifika sasa, kama ninavyomwambia, ni kweli nikikaguliwa nitakwenda kukaguliwa wiki sita, badala ya kuondoka siku tatu nitakwenda kukaa zaidi ya miezi miwili nikisubiria ukaguzi na mizigo, lakini kibaya zaidi, kwa nini hawa *TBS* ambao wana jukumu wasichukue kwamba wewe unachukua

kiwanda gani, mimi nitasema nauza vipodozi nachukua *Procter and Gamble*, basi lete hivyo vitu tuvipime kama viko sawasawa, au nimechukua *Unilever*, tuvipime viko sawasawa, wanipe *certificate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukatai kuvipima kama viko salama, lakini na wenyewe watupe *certificate* ili tusiwe tunasumbuka kila mara tunapoingiza mizigo. Huu usumbufu Mheshimiwa Waziri ataona sasa hivi umetengeneza *monopoly*, maana ukizungumza atakuwa analeta mtu mmoja, ukimwambia huyu ndio anayeleta chuma basi ataleta huyo huyo kwa sababu ndiye aliye na nafasi na *access* ya kwenda kwenye kiwanda hicho kinachohusika na kumpimia mizigo yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni hilo ambalo watu wengi wameliongelea, nadhani ni la kuongeza tu, kuhusu hizo milioni 50. Kwa kweli ni matatizo, Waziri akakae na timu yake, milioni 50 watu tulisha na zili kuwa kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi na kila tukienda kwenye mikutano tunaulizwa kama vile tuliwakopa. Kwa hiyo, wakae wakijua kwamba ahadi ni deni, hilo waliangalie kwa uzuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo wameliongelea watu na mimi nasisitiza tu, kwamba Serikali iangalie kwamba kuzichukua zile hela waangalie namna ya kuzirudisha na namna ya kuzifutilia lakini zirudi benki tuendelee kukopa. Mambo yetu yamekwama, benki wanakataa kutupa hela, benki kama *CRDB* ambayo walikuwa wanawenza kukupa mara moja, hawana hela. Tafuteni utaratibu, zirudisheni kule kama na ninyi mnataka riba basi chukueni riba kutoka benki ili tuendelee kukopeshwa na ndiyo uchumi wenyewe, hakuna uchumi mwingine, kama wananchi hawana hela utapata wapi hiyo kodi, maana hawanunui, utapata wapi hiyo kodi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hayo ndiyo niliyokuwa nayo. Ahsante kwa kunipa nafasi hii kutoa mchango huu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Massay, Mheshimiwa Khadija Nassir, Mheshimiwa Ezekiel Maige na Mheshimiwa Daniel Nswanzugwanko dakika tano tano.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu hapa. Kwanza nimshukuru Mungu kwa kunipa afya njema ya kusimama hapa na kuchangia. Pili, niishukuru sana Serikali kwa kufanya kazi kwa jinsi hii ambayo angalau sasa kuna matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nianzie hapa alipoishia mzungumzaji aliyeppita. Tunayo ahadi tumeitoa kule ya hizi milioni 50 (*village empowerment*), llani maana yake ni mkataba kati ya mtawala na mtawaliwa nasi tumeshaahidi kwamba wananchi tutawapatia mikopo ya milioni 50 na tumeandika. Kwa ushahidi zaidi naomba niitetee na kuiinua llani yetu ambayo tumeahidi katika uchaguzi. Ukiangalia ukurasa huu wa 112 tumeandika hapa na kwenye kifungu cha 57, kwamba tutapeleka milioni 50 kila kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Serikali ina changamoto nyingi, sikatai, lakini mwaka jana tumeahidi katika mpango ule wa bajeti kwamba tutapeleka bilioni 59, hatukuweza, mwaka umekwenda. Bilioni zile 59 tumeahidi tena nimeiona kwenye mpango wa bajeti ya sasa ya Serikali. Naomba sana Mheshimiwa Dkt. Mpango, iko bilioni 60, ndugu yangu naamini anafanya kazi nzuri, nafurahi kwa sababu ametenga mwaka huu. Ukitenga basi peleka, nimesema kwa kifupi namna hii ili ajue kwamba wapiga kura wanatusubiri, baada ya kutoka Bungeni kwa vyovyyote tunakwenda kwa wapiga kura, wanaauliza swalii la kwanza kwenye mkutano lini mnatuletea mkopo wa milioni 50 mlizotuahidi. Sasa Serikali naomba tufanye jambo hilo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri leo hii kwamba, katika kutekeleza ahadi ndiko unakomwona mwananchi wa kawaida anakubali mwelekeo mzuri wa Serikali yetu na

tukitaka tuungwe mkono tutimize ahadi. Huu ni mwaka wa pili sasa tunaenda kumaliza na ni mwaka wa kazi, basi tuanze kwa kiwango fulani ili mwananchi aelewewe kwamba, ni kweli Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeanza kutekeleza llani yake kwa kutoa milioni 50, angalau vijiji fulani vionekane, naamini wenzangu wamesema sana kuhusu haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kushauri kiuchumi. Uchumi wa nchi yoyote unahitaji maendeleo na maendeleo yanahitaji ushauri na ushauri unahitajika wa kitaalam. Ukiangalia, nimesoma kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri Dkt. Mpango, ukurasa wa 40, anaeleza jinsi Tume ya Mipango, nashauri kama inawezekana basi Tume hii iwe peke yake isiwe ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango ili inapopanga mipango yake iweze kushauri namna ya utekelezaji mzuri. Kwa sababu ikiwa pamoja inakuwa sio rahisi tena kushauri, naona kuna mkanganyiko hapo. Kama inawezekana iingle kwenye Ofisi ya Rais huko ili ikasaidie katika kutekeleza mpango wenye, maana wakati huu Tume ya Mipango inavyopanga na inapokuwa kwenye Wizara ya Mheshimiwa Dkt. Mpango, naona kuna mkanganyiko kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, katika uchumi wa nchi yoyote, sisi tuna benki, ni lazima Serikali iangalie benki zake. Kwa mfano, Benki tuliyonayo ya *TIB* Serikali isipowekeza kwenye benki yake yenye ambayo ina asilimia kubwa inayoendesha haiwezi kuendelea. Kwa nini nasema hivi; ukiangalia mitaji yoyote duniani Serikali ikiwekeza kwenye benki hii ni rahisi kwenda kwenye benki hii pia na kuona namna gani na hata ukienda kwenye soko la kimataifa huko ukiwa na asilimia 20 angalau umewekeza kwenye benki hiyo utaona pia mataifa mengine unaweza kufanya kazi nzuri katika biashara ya masoko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye *research* na wataalam wamsaidie Mheshimiwa Dkt. Mpango, najua ni mtaalam, nchi nyingi zilizoendelea zinalinda benkizao. Kama tatizo ni mtaji katika Benki ya *TIB* Serikali iwekeze pale. Kwa mfano, ukiangalia nchi ya China, China wana *Exim* na hawakubali pale mitaji yao ipotee, ukienda *South Africa*

wana DBSA, hawakubali, ukienda Norway wana DNB, hawakubali, wana benki wanayoitegemea. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Dkt. Mpango aangalie hali hiyo, nimeona nishauri haraka kwa sababu dakika zangu sio nydingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Dkt. Mpango, kwanza nimshukuru sana amenisaidia katika mambo mengi hasa kule Jimboni, lakini sasa tunao mkanganyiko wa sheria, Sheria ya Kodi au Zuio la Kodi (*withholding tax*). Sheria hii naamini katika Bunge liliopita walifanya zuio na kuondoa misamaha yote, huenda walikuwa na mapenzi mema lakini sasa mapenzi mema tumekuwa kama tumejinyonga wenyewe katika kuondoa misamaha yote na kuondoa uwezo wa Waziri kusamehe. Mheshimiwa Waziri alete ile sheria ili Bunge hili tubadilishe, tuone nafasi nzuri ya kufanya kazi kwa maslahi ya Taifa. Sitaki kutoa mwanya kwa mkwepa kodi ye yote lakini nimwombe alete sheria hiyo ili tuifanyie marekebisho kupitia Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninao mfano hai, kama Mbunge ye yote tunaomba mara nyangi misaada na kama Serikali inavyoomba misaada, nilijaribu kuandika *proposal* katika Wilaya yangu kujengewa daraja na daraja hilo ni muhimu sana, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwanza ameliona, nashukuru amelishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepewaa na Serikali ya Norway na watu tu wanaosaidia wenyewe mapenzi mema milioni 125 ya mwanzo ya kujenga daraja sasa kutokana na sheria yetu, panatakiwa pawepo mtu atakayelipa zuio la kodi la asilimia 18. Sasa basi ukienda kwenye Halmashauri zetu ukitaka walipe pesa hizo hawana uwezo Halmashauri wenyewe tu haina uwezo wa kulipa hiyo pesa ya zuio la kodi kwa sababu haina chanzo kikubwa cha mapato....

MWENYEKITI: Mheshimiwa siyo zuio la kodi ni VAT

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani ni VAT asilimia 18. Kwa hiyo basi sheria hii isipoletwa hapa tukafanya mabadiliko ndipo tunapo jinyonga wenyewe.

Kwa mfano, mfadhili amenisaidia ametupa milioni 152 za kujenga daraja, Serikali ya Halmashauri au Serikali ya Mitaa haina uwezo unapata wapi? Ukija kwa Waziri hawesi kusamehe kwa sababu sheria haimruhusu na ukisema yule mfadhili akalipe hiyo VATanakataa anasema mimi nakusaidia wewe kukujengea daraja halafu wewe unataka mimi nilipe kodi yako, haiji hata kwa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuone zile sheria ambazo zinaweza kuletwa hapa Bungeni, niombe kabisa Serikali ilete tufanye kazi kwa niaba ya wananchi, tuzibadilishe Sheria hizi kwa manufaa ya nchi yenye kwa sababu vinginevyo tutajifungia nati mpaka msumari wa mwisho. Hii maana yake ni nini basi? Tumeweka sheria hizi lakini tusijifunge moja kwa moja tukashindwa kufanya kazi kwa ajili ya sheria na kwa sababu Wabunge ndiyo tunatunga sheria, namwomba Mheshimiwa Dkt. Mpango, naomba tena sana alete ile sheria tufanye marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea kwa uchungu kwa sababu Serikali kwa bahati mbaya au nzuri haina namna ya kuleta pesa ya kujenga madaraja. Kuna kitu kinachoitwa *ceiling* (ukomo wa bajeti), ukomo wa bajeti ukishafika madaraja yetu kule katika maeneo ya vijijini hakuna namna, tunapopata wafadhili kama hawa, basi ni vizuri akakubali ili akatoa msamaha wa kodi katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimesimama ili kusudi kulisemea hili. Hata hivyo, niipongeze na kuishukuru Kamati yangu kwenye ukurasa wa 23 imeandika, hili siyo la kwangu kama Flatei, Mbunge wa Mbulu Vijiijini hapana! Hili ni jambo la Kamati lipo humu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niwaombe sheria itakapoletwa tuisaidie Serikali pia kuweka mwanya huu ambaa utasaidia Waziri, kama ikishindikana basi Waziri Mkuu apewe hiyo *authority* ya kusamehe kama inakuwa shida huku chini au tujue nani anatoa au Rais apewe basi, kuliko kuondoa kabisa ule wigo na kutoa mwanya huu wa sheria ambayo kimsingi ikiwekwa itatusaidia... (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Khadija Nassir dakika tano.

MHE. KHADIJA N. ALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Fedha na Mipango. Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ya kuweza kusimama hapa leo lakini pia napenda kuwapa heri ya mfungo wa Ramadhani Waislam wote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile dakika zangu ni chache, naomba sasa njikite moja kwa moja kwenye mchango wangu na nitaanza kuongelea mtiririko mzima wa fedha za miradi ya maendeleo. Mwaka wa fedha 2015/2016, fedha zilizotengwa kwenye bajeti ya miradi ya maendeleo ilikuwa ni bilioni 1,031.7 na kwa mwaka wa fedha 2016/2017, fedha zilizotengwa ilikuwa ni bilioni 791.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa Serikali imepunguza *budget ceiling* ya hizi fedha za maendeleo lakini bado tatizo la kupeleka fedha hizi kwenye miradi imekuwa ni changamoto kubwa. Mfano, katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wizara illidhinisha jumla ya shilingi bilioni 791.9 lakini mpaka kufikia Machi, 2017 Serikali ilikuwa imepeleka jumla ya shilingi bilioni 18.8 ambayo ni sawa na asilimia mbili tu ya bajeti ambayo imeidhinishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali juu ya hili ni kwanza, Serikali kupitia Bunge iidhinishe bajeti ambayo itaweza kwenda ipasavyo na siyo kuidhinisha bajeti kubwa ambayo haitaweza kwenda. Bajeti za Wizara ziendane na kasi ya makusanyo ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili; muda muafaka sasa kwa Serikali kuhakikisha fedha zote zinazoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo zipatikane kwa wakati ili kuendana na kasi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga Tanzania ya viwanda. Ushauri wangu wa tatu; Serikali isitegemee sana fedha za wafadhilli kwa sababu fedha hizi hazina uhakika wa kutosha, zinaweza kuja au zisije au zikaja kwa kuchelewa na hili linaweza kuathiri maendeleo ya miradi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza kuongea kwenye hili suala naomba Waziri atakapokuja kuhitimisha anipe majibu ya maswali haya yafuatayo:-

Huu mpango wa Serikali kuhamia Dodoma; Je, Serikali imetumia kiasi gani cha fedha katika mpango huu? Pili; Je, mpango huu umeathiri vipi fedha za umma ambazo zingeweza kupelekwa kwenye miradi ya maendeleo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niingie kwenye suala la misamaha ya kodi. Serikali imekuwa ikitoa misamaha ya kodi kila mwaka lakini bado misamaha hii haitolewi kwa uwazi kwa maana ya kwamba mimi na wewe na wananchi wengine hatujui misamaha hii inatolewa kwa vigezo gani. Wabunge na wananchi tunahitaji kujua *projection* ya misamaha hii lakini pia tunahitaji kujua uhalsia wa misamaha hii, pia ushauri wangu kwa Serikali ni kwanini isiwe *ina-publish* misamaha hii ili tuweze kujua kiwango na watu ambao wanasamehewa hizi kodi ni akina nani na wanatolewa kwa vigezo gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nigusie kidogo *issue* ya deni la Taifa. Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 malipo ya deni la Taifa ilikuwa ni bilioni 8,000 matumizi ya kawaida kwa mwaka huu yalikuwa ni bilioni 8,009.3 na kwa mwaka wa fedha 2017/2018 malipo ya deni la Taifa yanatarajiwa kuwa bilioni 9,461.4 na matumizi ya kawaida yanatarajiwa kuwa bilioni 9,472.7. Naipongeza Serikali kwa hili, kwa kuwa wameweza kuongeza bajeti ya malipo ya deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali ihakikishe kuwa fedha hizi zinatolewa kwa wakati ili nchi londokane na madeni yanayosababisha nchi kulipa fedha nydingi yaani ile fedha inayotoka kama riba ingawa Serikali inasema kwamba deni la Taifa ni himilivu lakini lazima Serikali iendane.....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako, Mheshimiwa Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Nsanzugwanko dakika tano tano tu.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi niseme machache katika mada hii inayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia naomba niseme nakubaliana na pendekezo au hoja iliyoko mezani naiunga mkono, nina mambo machache tu ya kushauri lakini kabla ya hayo ya kushauri naomba nianze kwanza kutoa pongezi sana kwa hatua ambazo zinachukuliwa na Mheshimiwa Rais za kuongeza mapato ya Serikali na kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze kipekee Mheshimiwa Rais kwa hatua ambazo amekuwa akizichukua kwenye suala zima la madini. Nadhani unafahamu na Bunge lako linafahamu kwamba mimi ndiye Mbunge wa Bulyanhulu. Mbunge ambae nimekuwa nikiishi na mgodi wa Bulyanhulu kwa miaka yote, nimekuwa nikizungumzia sana kuhusu Serikali kutokupata stahiki yake pamoja na wananchi, Wabunge wengi tumekuwa tukiungana kwenye hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishtuka sana juzi Jumatatu, pamoja na hatua nzuri sana iliyochukuliwa na Mheshimiwa Rais, zikatokea baadhi ya sauti hapa Bungeni zikitutisha kwamba eti tunawenza tukapata shida. Nawaomba sana Watanzania wenzangu, mimi kama Mbunge wa kule,

naomba muamini kwamba nchi inaibiwa. Tunaweza tukabishana kwenye kiwango cha wizi lakini suala la kwamba tunaibiwa halina ubishi kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 2008 na 2009 niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, wananchi wa kawaida kabisa vijijini walianza kuwa wanayavamia yale malori yanayosafirisha mchanga na kuiba ule mchanga, kwenye viroba vile vya mfuko wa saruji vya kilo 50 walikuwa wanawenza wakachenjua kwa kiteknolojia ya kienyeji na kupata dhahabu na mfuko mmoja walikuwa wanapata siyo chini ya shilingi milioni 50. Kufuatia hatua hiyo, wawekezaji walianza kusafirisha yale malori usiku kwa ulinzi mkali kuonesha kwamba kuna mali nyingi inayosafirishwa. Nilishtuka sana kusikia Watanzania wenzetu wakitia mashaka juhudhi hizo za Rais, niwaombe sana na nikuombe Mwenyekiti na Bunge lako Tukufu watu wa namna hii inabidi pengine tuenze kujiuliza sana kuhusu Utanzania wao na uadilifu wao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani hata kidogo kwamba katika nchi ambayo ina uwekezaji mkubwa na rasilimali nyingi za namna hiyo ukifika leo Kakola, tena wao wenye we wamekuwa wachochazi wa kwanza, wakifika pale wanasema hivi hapa kuna Mbunge? hakuna maji, hakuna hiki, hakuna hiki kwa sababu wanasema wanapata hasara. Wanapata hasara kwa sababu dhahabu iliyoko kwenye *container* la tani 20 wana-report kwamba kuna kilo nne wakati kuna kilo 28. Kwa hiyo kwa record za performance ya kilo nne lazima utasababisha hasara, lakini ukiweka kwa hesabu ya kilo 28 kwa *container* lile lazima una faida kubwa. Kwa kufanya hivyo maana yake wangeweza kuwa wanalipa corporate tax, wangeweza kufanya mambo mengi ambayo tunapaswa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tuungane kwenye hili jambo ni vita kama ambavyo Mheshimiwa Rais amesema na wananchi wa Msalala nilikuwa Kakola juzi nimeongea na wananchi wangu, wanamuunga mkono sana Rais na tunaomba Bunge lako limuunge mkono. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri tu kwamba katika mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Bomani yako mengi yaliyosemwa na machache yametekelezwa kwenye ripoti hiyo, nitaomba tu nikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba pengine ni vizuri *report* hiyo ikarejewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, moja ya vitu vilivyopendekezwa na Tume ya Bomani ni kwamba, katika dunia na nchi zote tulizozunguka mimi nikiwa Mjumbe, ilionekana kwamba hakuna sehemu ambayo wana utaratibu wa ku-share manufaa yanayotoka kwenye mgodi kama tunavyofanya Tanzania, kwenye nchi zingine wana *revenue sharing plan*, kwamba eneo ambalo kuna mgodi wanapata *percent* fulani kutokana na kodi na tozo mbalimbali ambazo zinatokea au zinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba baadhi ya mapendekezo ambayo hayajatekelezwa na Serikali yarejewe na yatekelezwe, hata hili la kujenga *smelter* limo tulikwenda mpaka Sumitomo mimi mwenyewe nilikwenda na tukashauri kwamba Serikali ijenge *smelter*.....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa
muda wa mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. EZEKIEL M. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru na naunga mkono hoja, nitazungumza tena kesho kwenye Wizara ya Nishati na Madini. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Nsanzugwanko.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Mbunge wa Msalala amenifurahisha anasema nchi inaibiwa kwa hiyo kama nchi inaibiwa, basi lazima tuzuie isiibiwe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono hoja hii na nimpongeze Waziri Dkt. Mpango na Naibu wake hongera sana wanafanya kazi kubwa. Pia niwapongeze wataalam kwenye Wizara yake, Gavana wa *Central Bank* Profesa Ndulu wanafanya kazi nzuri hasa katika mazingira haya mapya ambayo muda wote tumekuwa tukiibowi na watu wengi wamekuwa hawalipi kodi. Dkt. Mpango wako vizuri hongera, wachape kazi, changamoto ni nydingi lakini huo ndiyo mwendo. Mzee Mwinyi Rais wa Awamu ya Pili alisema kwamba "kila zama zina kitabu chake" sasa zama hizi ni mpya lazima tucheze ngoma kadri inavyopigwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo mawili tu ya haraka haraka, kwanza; Mheshimiwa Waziri namkumbusha ujenzi wa Ofisi za *TRA* – Kasulu, kwa maana kwamba huduma za *TRA* pale Kasulu ili mtu akafanye *registration* ya gari akitoka Kakonko, Kibondo, Buhligwe na Kasulu anasafiri kwenda Kigoma. Bosi wa *TRA* pale anasema shida yao ni mashine kwamba kuna mkubwa mmoja alikuwa haja-*release* mashine zile kwenda pale Kasulu ili wawe wanafanya *registration* ya magari. Nimepata taarifa sasa hivi kwamba *registration* ya *TIN-number* wameanza *last week*, hilo ni jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri nimkumbushe kwamba Halmashauri ya Mji wa Kasulu tumeshawapa kiwanja *TRA*, tunaomba wajenge Ofisi sasa. Wanapanga kwenye vijumba vyaa hovyo hovyo pale, wakati nina uhakika *TRA* wana uwezo wa kujenga Ofisi pale. Tunataka Ofisi ya *TRA* tumewapa kiwanja, tunaomba wajenge Kasulu kwa Wilaya zote nne ambazo zinazunguka eneo lile. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, niseme lingine dogo, Waziri naomba alisikie hili, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo tulikuwa na semina na watu wa *SADC* na watu wa *IFAD* na wafadhili wengine, wamelalamika sana wanasema Serikali, Wizara ya Mheshimiwa Waziri, Hazina hawataki kupokea fedha za msaada wa kilimo. Wote tukatazamana tulokuwepo pale. Wamelaumu kitu kinaitwa Kamati inayopitia madeni sijui

kwamba imejaa urasimu, siyo rafiki, sasa tukajiuliza wote, Mwenyekiti wangu ataniunga mkono yule pale ni kitu gani hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, hebu wakakae na hawa *partners* wetu, ni kitu gani ambacho kiko Hazina pale mpaka kinasema hawa marafiki zetu wanaotaka kutusaidia kwenye sekta ya kilimo hizo fedha hawazitaki kuzipokea. *Actually underline* wamesema hawataki kupokea fedha zao na wakaenda mbali zaidi wakasema *IFAD* wana miradi mitatu, hawataki kupokea fedha zao, *World Bank* wana miradi mitatu ya kilimo, hawataki kupokea fedha zao, *NORAD* wana mradi mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliokuwepo pale tukaanza kushangaa pale. Ni kitu gani kinatokea Hazina, fedha za *support*, zingine ni msaada unakuja, ni kitu gani pale Hazina kinaleta urasimu huo? Tunakwenda mbali zaidi Mheshimiwa Waziri wanalaumu baadhi ya Watendaji wake kwamba wamejaa urasimu na wanatupotезеа fedha nyingi katika sekta ya kilimo. Nimelisema hili kwa sababu jana limezungumzwa na wenyewe waliokuwepo pale hebu wawe *pro-active* basi, fedha zinazokuja wazipokee tuweze kuchapa mwendo kusaidia sekta ya kilimo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine dogo ni hili, kwenye kitabu ukurasa wa 89 Mheshimiwa Waziri amesema moja ya majukumu kwa mwaka 2017/2018 ya Benki ya Kilimo ni kuwasaidia na kuwawezesha wakulima wadogo. Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze hao wakulima wadogo ni wa wapi watakaowawezesha, watawawezeshaje wakati Benki yenyewe ndiyo hiyo? Wao jana walikuwepo kwenye semina hiyo, walikuwepo watu wa Tanzania *Agricultural Bank*, nao wanasema wana shida ya fedha. Ningependa hilo nalo Mheshimiwa Waziri aliweke sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, Waziri chapeni mwendo na wakati ndiyo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsanteni sana. (*Makofii*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na baraka zake kwetu. Naomba nichukue fursa hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu akiongoza timu yake ya wataalam kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo Wizara mama ambapo Wizara zote zingine zinategemea ufanisi wa Wizara hii. Naamini Wizara ya Fedha inaweza kufanya vizuri zaidi ili matumaini ya Watanzania yaweze kutimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nishauri Waziri wa Fedha alete mabadiliko ya sheria Bungeni kumrudishia uwezo wa kutoa msamaha wa kodi katika miradi mbalimbali na pia katika misaada tunayoweza kupata kama Serikali, taasisi zinazotoa huduma na Halmashauri zetu. Naamini tulikosea kufuta uwezo wa Waziri wa Fedha kutoa msamaha wa kodi. Kelele nyingi za wawakilishi na pia taasisi zetu kupunguza masuala ya kodi siyo katika hii miradi na misaada midogo, walikuwa wanalenga misamaha mikubwa kama ya kwenye migodi, utafutaji wa madini (*research*) na uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii imekuwa kero tukipata misaada kutoka kwa wafadhili ambao hawako tayari kutoa au kulipia kodi, mfano magari ya wagonjwa, miradi ya maji, madaraja, ujenzi wa hospitali na vituo vyta afya, huduma za elimu na zingine. Muhimu ni kuweka wazi misamaha hiyo na tulio wengi tusiadhibiwe kwa ajili ya wachache waliofanya vibaya kwa kutumia vibaya mfumo wa msamaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishauri Wizara iongeze wataalam zaidi katika Idara ya Mipango. Idara hii ndiyo inayoweza kuleta mafanikio makubwa sababu ya kushauri

kwenye sera na pia kuboresha mapato ya Serikali hasa kutanua wigo wa kukusanya kodi (*tax base*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri waajiriwe wataalam hasa kutoka *private sector* wenye uzoefu ili kuleta mabadiiko ya fikra (*mind set change*) ndani ya Wizara. Jukumu la Wizara ni kusimamia kukusanya mapato yote ya kikodi na yasiyo ya kikodi pia matumizi ya mapato hayo pamoja na kuweka mipango ya miradi ya maendeleo. Kwa sasa sera yetu imefanya Tanzania iwe moja ya nchi ambapo sekta isiyo rasmi (*informal sector*) kuendelea kukua kwa kasi na *formal sector* kuendelea kushuka. Hatukusanyi kodi katika sekta isiyo rasmi na kuumiza sekta rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara iangalie uwezekano wa kuleta mabadiliko ya sheria ambayo itaweka muda wa ukomo wa kodi, tozo au ushuru ambayo haijokusanya kwa muda maalum na siku mkusanyaji akizinduka usingizini anataka alipe kutoka siku sheria ilipotungwa. Sio kila mwananchi anajua sheria, ni wajibu wa Serikali ngazi zote kutafsiri sheria na kutoa elimu kwa wakati. Kwa sasa wananchi wanalamika sana, pamoja na baadhi za Halmashauri kutoza kodi, tozo za miaka mingi iliyopita, uzembe wa kutokusanya wakati huo siyo wao. Mfano ni *Motor Vehicle License, SDL, Withholding Tax* na je, hao waliosababisha kutokusanya wamechukuliwa hatua gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Wizara iangalie namna ya kuongeza fedha katika taasisi zilizo chini yake kuna *TADB* na *TIB*. Pia kupitia Sheria ya Kodi kuleta mabadiliko ya kupunguza kodi mbalimbali ili *compliance* iwe kubwa na *fine* na adhabu kwa watakaodanganya iwe kubwa. Wizara iangalie namna ya kuhakikisha mifuko iliyokuwa chini yake kama Mdhhibit wa Mahesabu ya Serikali na Mkaguzi Mkuu (*CAG*), Mahakama na Bunge zifanyiwe utafiti zaidi ili kazi zao kama mihimili tofauti na huru zifanikiwe. Pia Msajili wa Hazina, Kitengo cha Utafiti na Uendelezaji (*R&D*) kiboreshwe ili taasisi zote chini yake ziweze kuleta faida na kuchangia katika uchumi wa Taifa letu.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja. Mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

(i) Wizara ya Fedha iangalie sera zake za kutoa fedha za miradi iliyopitishwa na Bunge, fedha zinachelewa na wakati mwingine hazitolewi kabisa na miradi ya maendeleo haikamiliki.

(ii) Wizara ya Fedha ilitazame kwa makini suala la *road licence* ni kero kwa wananchi. Naomba kodi hiyo iwekwe kwenye mafuta ambako kila mtumiaji chombo kinachotembea barabarani atawezekana kulipa na itakusanywa kiurahisi sana.

(iii) Huduma kwa wastaafu, kwanza wanacheleweshwa kupewa stahili zao na nashauri maslahi yao yaongezeke kwani hali ya maisha inapanda na wanahitaji mlo mzuri kuweza kukabiliana na hali zao.

(iv) Mgawanyo wa fedha za ruzuku uangalie maeneo yaliyo nyuma zaidi ili kuyavuta mkono kwa makusudi ili wasogee maana kuna changamoto nyingi zaidi.

(v) Mikopo ya fedha ielekezwe zaidi kwenye kukuza kilimo kama tegemeo la wananchi wengi nchini na mchangiaji mkubwa wa pato la Taifa.

(vi) Walipa kodi ni wadau muhimu wa maendeleo, naomba pawepo staha zaidi katika kufuatilia kodi na wananchi waelimishwe zaidi kwa makala na matangazo mbalimbali juu ya umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari.

(vii) Benki ya Kilimo iwezeshe, kilimo kitakua kama mitaji itaelekezwa huko.

(viii) Sheria itungwe kuwasaidia watumishi ambao hujikuta wamelazimika kukopa fedha kwa wakopeshaji wasio rasmi wanaotoza riba kubwa inayofikia 30% kwa mwezi yaani

ukikopa Sh.10,000,000/= tarehe 1 - 31 Desemba wanalipa Sh.13,000,000/= ongezeko la Sh.3,000,000/= na akichelewa inalipa pamoja na *Interest* kwa Sh.3,000,000 ni Sh.300,000, watu wanaabiwa sana.

MHE. OSCAR R. MUKASA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Benki Kuu inaonesha kushuka kwa kiwango kikubwa kwenye mikopo ya mabenki kwenye shughuli muhimu za kiuchumi mfano mkopo kwa watu binafsi 4.9% kwa mwezi Machi, 2017 ukilinganisha na 37.2% kwa mwezi Machi, 2016, mawasiliano na usafiri 21.6% mwezi Machi, 2017 ukilinganisha na 27.4% ya Machi, 2016 na kadhalika. Je, mwelekeo huu unatupeleka wapi?

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, kaka yangu Mheshimiwa Phillip Mpango kwa kazi nzuri na nampa pole kwa changamoto kubwa za kuendesha uchumi wa wananchi. Pia napenda kumpongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji. Napenda kuwapongeza watendaji wote chini ya Katibu Mkuu, Ndugu James Dotto pamoja na Manaibu wake. Jimbo la Nyasa tunawashukuru sana kwa *support mnayotupa*, tunasema ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo dogo kuhusu kufungwa kwa Benki ya Mbinga, napenda kuifunza tatizo ni nini? Benki ile ilikuwa inasaidia sana wakulima wadogo wadogo hasa katika mikopo. Najua kulingana na hali halisi huenda *running costs* zilikuwa kubwa au uendeshaji usio na tija (ubadhirifu) sasa sijui ni nini kilichotokea. Kwa kuwa wananchi wameulizia sana, naomba kupata majibu na hasa juu ya hisa zao. Nawaombeni na naamini jitihada zenu zitaendelea kuzaa matunda.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, pongizi kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazofanya kusimamia Wizara ambayo ndiyo *heart beat* ya uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania inabidi tutumie

catch-up economic growth approach as opposed to endogenous technology-driven economic growth approach ambayo wenzetu nchi zilizoendelea zinatumia kwa kutumia *industrial revolution* ambayo *diffusion* yake ilianzia England na kusambaa West. Tanzania inabidi *catch-up approach* tuielekeze kwenye kilimo, ufugaji, uvuvi na ujasiriamali mdogo mdogo ili (*taken together*) tuweze kutoka kwenye umaskini ambaao ni asilimia 65 ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara iangalie na kuzipa uwezo *TIB* na *TADB* ili ziweze kuwa mstari wa mbele na *engine* ya kusukuma *catch up economic growth* ninayozungumzia. Kwa hali ilivyo sasa, kwa kweli bado *we are not walking the talk*. Nashauri mkae na *TIB* na *TADB* muangalie *synergies* na nani atafanya nini na kwa nini lakini kwa kushirikiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Sera ya Bima inayoandaliwa 2017/2018. Nashauri *NIC* ajikite kwenye kusaidia majukumu ya kibima kwenye *catch-up economic growth* hapo juu. *It has to be integrated* badala ya kuendelea na *business as usual* ambayo *quite frankly* naona tija na weledi wa *NIC in its current practice* haupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi milioni 50 kwa kila kijiji ni vema zikachelewa lakini tukajipanga, tukalenga kwenye kutekeleza *catch-up economic growth as argued above*. Nashauri mkae na *UTT* na *TADB* na kutumia uzoefu wao, washauri *model*ya kutumia milioni 50 kwa kila kijiji katika namna iliyo endelevu na inayolenga *ku-achieve* niliyoeleza hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Philipo Mpango, kwa hotuba yenye kuleta matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa bajeti ya

2016/2017, taarifa inasema kati ya fedha za maendeleo kiasi cha shilingi bilioni 18.89 kilikuwa kimetumika ambacho ni asilimia mbili tu ya fedha iliyoidhinishwa. Ni dhahiri hiki ni kiwango kidogo sana katika utekelezaji wa bajeti hii. Nimwombe Mheshimiwa Dkt. Mpango utekelezaji wa bajeti ya mwaka ujao wa fedha 2017/2018 uwe wa uhalisia zaidi kuliko kwenye makaratasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Ofisi hii ndiyo jicho letu sisi Bunge katika kuisimamia Serikali. Cha kusikitisha, ofisi hii imekuwa omboomba kwa Serikali. Hili linatia shaka na doa kwenye uhuru wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kuwa utendaji wake unatakiwa uwe huru bila ya kuingiliwa na yejote. Uhuru huo unakuwa na mashaka kama iwapo Mkaguzi anaenda kwa mkaguliwa kuomba fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu kwa mwaka 2016/2017, iliidhinishwa kiasi cha shilingi bilioni 44.6 lakini mpaka kufikia mwezi Machi 2017, Ofisi ilikuwa imepokea shilingi bilioni 32.6 ikiwa ni sawa na asilimia 73.05 ya bajeti ya matumizi ya kawaida. Ni dhahiri Ofisi hii itapata shida kama tulivyoshuhudia imeshindwa kufanya kaguzi kwenye baadhi ya Balozi na ofisi nyingine nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru na naunga mkono hoja.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Fedha za Serikali ina *impact* gani kwa ukaguzi wa kila mwaka? Ubadhirifu unaoonekana kwenye ripoti ya CAG umefanyiwa kazi gani? Wabadhirifu kila mwaka wanapatikana lakini hakuna hatua zinazochukuliwa, hivyo ni *business as usual*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, CAG kukagua fedha za Vyama vya Wafanyakazi kama vile *CWT* ni halali? Sheria iliyounda vyama hivyo imetaja Mkaguzi kuwa ni yule aliyetambuliwa na Msajili wa Vyama vya Wafanyakazi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo kwa Ofisi za *TRA* Kakonko ni jambo linaloleta usumbufu kwa wafanyabiashara kufuata huduma kilomita 300.

MHE. QAMBALO W. QULWI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuishauri Wizara hii na Waziri wake kuongeza uwazi na umahiri katika ukusanyaji wa kodi. Wananchi wetu hawakatai kulipa kodi ila iko mianya mingi ya ukwepajji wa ulipajji wa kodi sahihi. Wapo watumishi wa *TRA* wanapokisia kodi wanachukua asilimia kubwa na Serikali inapata kidogo. Serikali izibe mianya ya wizi wa kodi ili ipate mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Maji ya *KAVIWASU* (*Karatu Villages Water Supply*) ni chombo cha wananchi (*COWSO*) kilichosajiliwa kwa sheria ya nchi *Cap.375* kutoa huduma ya maji katika Mji wa Karatu na vijiji vinavyozunguka mji huo. *KAVIWASU* hawafanyi biashara bali wanatoa huduma ya maji kidogo wanachopata kutokana na mauzo ya maji kinatumika kuendeleza mradi katika maeneo ambayo mtandao wa maji haujafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mshangao wa wengi wameshtuka *TRA* Karatu wameitaka *KAVIWASU* ilipe kodi yenye jumla ya Sh.200,000,000/= na zaidi la sivyo watakatiba huduma na kukamatiwa mali. Mheshimiwa Waziri, *DAWASCO*, *AWASA*, *DUWASA* na bodi nydingine nydingi tena za daraja A hazilipi kodi hiyo iweje *KAVIWASU* tena chombo cha wananchi ambacho hata hakipati ruzuku yoyote kinalazimishwa kulipa kodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii aangalie suala hili kwa kuwaelekeza *TRA Karatu* wasitishe madai yao hayo yanayokiuka sheria. Ikiwa sheria inawataka *KAVIWASU* kulipa kodi basi Waziri kwa mamlaka aliyonayo asamehe kodi hiyo ili wananchi wa Karatu waendelee kunufaika kwa huduma ya maji.

MHE. DEVOTHA M. MINJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nichangie kwa maandishi hotuba ya Waziri

wa Fedha na Mipango. Baada ya kumsikiliza sana kwenye uhamasishaji wa Wabunge kuunga mkono hoja ya Wizara hii ni lazima tushauri ili kusaidia maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara kama wadau muhimu wanaotegemewa na Taifa kuongeza mapato, wako katika wakati mgumu sana na wengi wamefunga biashara zao hasa katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Tano kutokana na kuelemewa na kodi nyingi zisizo na tija. Kwa nini wafanyabiashara wasipewe fursa wezeshi za kuwezesha wafanye biashara hizi wapate faida na waweze kulipa kodi bila kukimbizana? Serikali lazima ifungue milango ya biashara na kuwaona wafanyabiashara ni marafiki na wadau muhimu wanaotakiwa kusaidiwa ili biashara zao kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa ya Waziri, kwa nini hajaleta taarifa za hali za biashara, kwa nini hajasema wafanyabiashara wangapi wamefunga biashara, wawekezaji wangapi wamehamisha uwekezaji au wamesitisha uwekezaji wao? Waziri angeleta *status* ya hali ya biashara nchini na *challenges* zilizopo ili tuone mikakati ya Serikali ya kufufua biashara hizi au kuhamasisha wafanyabiashara kurudi kwenye biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za Afrika Mashariki mfano Rwanda mifumo yao ya kukusanya mapato ni rafiki na kila mfanyabiashara anajikuta anaona umuhimu wa kulipa kodi/mapato kwa faida ya Taifa lake. Kwa nini tusiige mfumo huo ambapo hata ukitokea biashara imekufa wanapeleka wataalam wa biashara, wanazungumza nao na kuwapa *indoor training* jinsi ya kufufua biashara badala ya hivi sasa biashara ikifa hamna anayejali hata Serikali haioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake (*TWB*), tumesikia hadithi za kuwa benki hii itapeleka matawi mikoani. Je, kwa nini Benki hii ya Serikali iliyoanzishwa kwa ajili ya kutoa ahueni kwa wanawake imebaki kuwa ya watu wachache kwa maana ya mikoa michache? Benki zingine

zimeanzishwa nyuma baada ya *TWB* sasa hivi zina matawi karibu kila mkoa, kuna shida gani kwa nini benki hii ya Serikali isifungue matawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *interest* ya Benki hii ya Wanawake ni kubwa hata kuzidi Benki ya Posta, kwa nini? Lengo la benki hii ni kusaidia wanawake wapate fursa za kukopa na kuendeleza ujasiriamali lakini cha kushangaza inaonekana kuwa na *interest* za juu hali inayopelekea wanawake wengi kushindwa kumudu gharama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwe na mipango mipyä ya kupata vyanzo nya mapato, wataalam wabuni vyanzo vipyä nya mapato kupitia miradi mipyä ya kilimo, uvuvi na mifugo ambapo zipo nchi zimeendelea kwa kutegemea *blue economy* yaani uvuvi tu. Kwa nini Serikali isiflikirie uwekezaji kwa maana ya kuwa na wataalam ambao watalipatia Taifa mapato badala ya hivi sasa inakimbizana na wavuvi haramu na kuingia gharama nyingi za kuharibu nyavu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wawekezaji wameanza kufunga viwanda. Kwa nini Serikali haifanyi utafiti na kuja na mawazo/mbinu za *ku-retain* wawekezaji badala ya kukaa kimya na kusubiri wawekezaji wapya?

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango; Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa uwasilishaji wa bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Serikali ikifanya juhudzi za kurasimisha biashara zisizo rasmi, Wizara ya Fedha kupitia *TRA* haioneshi juhudzi za makusudi kuwakomboa wananchi wa hali ya chini kuinuka kiuchumi na kuweza kuchangia pato la Taifa kutohana na taratibu ngumu zilizowekwa kwa wafanyakia biashara katika kuanzisha na kuendesha biashara zao. Taratibu hizo ni pamoja na:-

- (i) Kumkadiria kodi mtu anayetaka *TIN* ya biashara na anatakiwa alipe kadilio hilo kabla ya biashara kuanza;
- (ii) Kumbaka mfanyabiashara aambatanishe *invoice* yake ya *EFD receipt* wakati wa kuwasilisha *invoice* ya mradi kwa mtu aliyempatia huduma kabla hata yeye hajalipwa, mfano Idara za Serikali ambapo malipo yenewe hayalipwi kwa wakati;
- (iii) Kuwataka wafanyabiashara kununua *EFD machine* kwa fedha zao chache za mtaji wakati *EFD ni machine* inayoiwezesha *TRA* kukusanya mapato yake. Ni kwa nini tusifanye kama *TANESCO* ambapo mita ya umeme inakuwa mali ya *TANESCO* hivyo kuipunguzia gharama ya ufuatiliaji wa madeni ya kodi? Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Tano alitoa na kuzigawa bure ili zisaldie kukusanya kodi lakini utaratibu huo ulifanyika kwa kipindi kidogo tu na haukuendelea tena;
- (iv) Kuzuia ugawaji wa *Tax-Clearance* kwa mfanyabiashara anayedaiwa kodi jambo ambalo si sahihi kwani kunamkwamisha mfanyabiashara huyo kuendelea kufanya biashara ili aweze kupata fedha ya kulipia deni la kodi anayodaiwa ukitilia maanani kuwa hata leseni haitolewi kwa mtu asiyekuwa na *Tax Clearance*. Kwa nini usiwepo utaratibu mwingine wa kumruhusu huyu mtu akaendelea kufanya biashara wakati mwingine anakuwa anakadiriwa makadirio ya kodi makubwa kuliko pato halisi. Akinyimwa *Tax Clearance* anashindwa kuomba kazi matokeo yake anafunga biashara. Serikali inawavunja moyo wasifanye biashara halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuanza kulipa madeni ya wazabuni kiasi cha shilingi bilioni 796.22 kati ya kiasi cha shilingi triliuni tatu kinachodaiwa. Hata hivyo, bado wazabuni wengi wanadai labda ni vizuri Serikali itangaze katika magazeti wazabuni waliohakikiwa na wale walolipwa madeni ili waweze kujua sababu kuna wengine walikuwa wanadai lakini hawajui hatima yao mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Wanawake ilianzishwa ili kuweza kuwasaidia wanawake kupata mtaji wa biashara baada ya kuona udhalilishaji mkubwa wanaopata katika baadhi ya taasisi. Mwaka 2010 Serikali ilitoa ahadi ya kuipatia Benki ya Wanawake shilingi bilioni 10 kwa miaka mitano maana yake shilingi bilioni mbili kila mwaka. Mwaka 201/2012 – Serikali ilitoa shilingi bilioni mbili; 2012/2013 – Serikali ilitoa shilingi bilioni 1.75 na 2013/2014 – Serikali ilitoa shilingi bilioni 1.5. Jumla Serikali imeweza kutoa shilingi bilioni 5.75. Je, shilingi bilioni 4.25 itatolewa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TIB (Tanzania Investment Bank)*, Tanzania tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda lakini bila kuiwezesha benki hii tutapata shida sana, sababu ndiyo benki itakayosaidia kuwezesha miundombinu ya viwanda. Serikali iliahidi kuipatia mtaji wa shilingi bilioni 500 na tena shilingi trillioni tatu lakini walipatiwa shilingi billioni 150 tu. Je, nini mkakati wa kuisaidia benki hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara yenye majukumu muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Sisi kama Wabunge tuna wajibu wa kuwakumbusha na kuwashauri. Majukumu ya Wizara hii ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje ya nchi pamoja na matumizi yake;
- (ii) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi na kijamii kwa ujumla;
- (iii) Kuandaa na kutekeleza bajeti ya Serikali;
- (iv) Kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kupunguza umaskini katika sekta mbalimbali;
- (v) Kusimamia Deni la Taifa na upatikanaji wa rasilimali fedha;

- (vi) Kusimamia Tume ya Pamoja ya Fedha;
- (vii) Kulipa na kuandaa watumishi Serikalini;
- (viii) Kudhibiti biashara haramu ya fedha pamoja na ufadhilli wa ugaidi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati sasa umefika kwa Serikali kulipa deni la ndani. Kwa kulipa madeni ya ndani itatufanya tuweze kuendelea katika masuala mbalimbali ya kimaendeleo na kutimiza vizuri mikakati tulioiweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upatikanaji wa fedha kutoka Hazina limekuwa ni la kuchelewa sana. Kwa muda mrefu sana sasa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango imekuwa ikichelewesha sana kupeleka fedha kwenye Wizara na Idara mbalimbali za Serikali kama zilivyoidhinishwa na kufanya shughuli za kimaendeleo kushindwa kufanyika na kushindwa kutimiza malengo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za Muungano ni changamoto ya muda mrefu. Iko wazi kabisa kwa kuwa kuna mamlaka tatu ambazo ziko dhahiri wala henziepukiki lakini imekuwa utamaduni fedha za Muungano kutumiwa na Tanganyika wakati Zanzibar ikikoseshwa fedha hizi ambazo ziko kisheria. Hivyo, tunaiomba Wizara ya Fedha kupitia Serikali kutatua kero hii ya muda mrefu na mamlaka hizi zipewe haki zake na zionekane ili kuепusha migongano isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya mazingira imetengewa fedha kidogo sana ukizingatia mazingira ni eneo muhimu kwa maisha ya viumbe vyote vyenye uhai. Kwa hiyo, nashauri sekta hii iongezewe fedha ili iendane na hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti naishauri Serikali kupunguza utitiri wa kodi kwa wananchi na wafanyabiashara. Jambo hili linapelekea biashara nyingi kufungwa na Serikali kukosa mapato ya kuendesha nchi yetu. Pia Serikali ifike mahali ifahamu kwamba katika biashara ya kila Mtanzania Serikali

ni *shareholder* kwa asilimia 30% hivyo iwawezeshe wafanyabiashara wafanye biashara ili kuendeleza biashara na kuleta pato kwa Tanzania badala ya kuwafukuza na kufunga biashara na Serikali kukosa mapato kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwe inatekeleza ahadi zake na utekelezaji uonekane. Hii imeonekana kwani mwaka jana Serikali iliahidi kugawa *EFD machine* kwa wafanyabiashara lakini mpaka leo haijagawa *machine* hizo. Hili linarudisha nyuma maendeleo ya umma. Pia napenda kujua ni utaratibu gani unatumika kugawa *EFD machine* na watu gani wanapaswa kutumia hizi *EFD machine*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakiki madeni ya watumishi na watoa huduma. Bado tunasisitiza Wizara ya Fedha na Mipango kuendelea kuhakiki na kulipa madeni mbalimbali ya ndani hasa watumishi, wakandarasi, wazabuni na watoa huduma wengine ambao baadhi yao walikopa benki kupata mtaji ili waweze kutoa huduma kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. JUMA OTHMAN HIJA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Fedha. Nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake, pamoja na Watendaji wake wote kwa kutayarisha hotuba hii na kuiwakilisha kwa ufanisi mkubwa. Katika kuchangia hotuba hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi kirefu sasa, mwenendo wa thamani ya fedha yetu imeendelea kuporomoka. Hii inaleta tabu kwa wafanyabiashara na wananchi. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, Serikali ina mpango gani kuzuia mporomoko huu? Ni vema Serikali ikachukua hatua za haraka kuzuia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu bado linaendelea kutegemea misaada kutoka nje ya nchi, hilo ni jambo baya

na halifai kuendelea kuwepo. Serikali inatakiwa kuweka mipango mizuri ili kuondokana na utegemezi. Serikali yetu ina vyanzo vingi vya kiuchumi ambavyo kama tutavidhibiti, vitaweza kutuongezea pato na kuondokana na utegemezi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya fedha ni miongoni mwa Wizara muhimu sana katika kuendeleza nchi hii. Hivyo namwomba Mheshimiwa Waziri kuendeleza mpango wa mafunzo kwa Wizara (*training program*) ili kuweka katika hali ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itoe msamaha kwa wafanyabiashara wote wa magari na pikipiki ambao waliuza vyombo hivyo vya moto lakini wanunuzi hawakubadilisha majina. Natoa ushauri huo kwa sababu mbili kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Sheria ya *Annual Motor Vehicle License* haimlazimishi muuzaji kulazimisha mnunuzi kufanya mabadiliko ya umiliki. Sheria inampa mnunuzi siku saba mpaka thelathini za kufanya mabadiliko ya mmiliki (*Transfer of Ownership*), hivyo hata asipofanya mabadiliko ya umiliki hakuna namna ambavyo muuzaji anaweza kufahamu kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hiyo inafanya vyombo vingi vya moto kubaki na majina ya wauzaji kwenda muda mrefu, hivyo kusababisha wafanyabiashara wa magari na pikipiki kudaiwa madeni makubwa kupitia *TIN* zao. Mheshimiwa Waziri, akitaka kuwasaidia wafanyabiashara hao, ni jambo la busara kutoa msamaha wa madeni wanayodaiwa ili wasifilisiwe na *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, madeni hayo yamekuwa ya muda mrefu sana kutokana na Mamlaka ya *TRA* kutokumbusha wafanyabiashara wa magari na pikipiki kwamba wanabeba jukumu la kulipa *Motor Vehicle License*

kwa vyombo ambavyo walikwishauza, lakini wanunuzi hawakubadilisha umiliki wake. Makampuni mengi yameshafanyiwa ukaguzi zaidi ya mara moja na wakalipa kodi ya Serikali. Nadhani siyo jambo la afya sana kuwabebesha wafanyabiashara hao mzigzo huo mkubwa wa deni ambao siyo wa kwao moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa hoja yangu ni kwamba Serikali ni lazima ijenge mazingira rafiki kwa wafanyabiashara kwa vile ndiyo wateja wao. Hivyo, kutokana na ukweli kwamba kuna eneo ambalo mamlaka yenye we ya *TRA* iljisahau kuwakumbusha wafanyabiashara wajibu wao katika kufuatalia mabadiliko ya umiliki wa vyombo vya moto kwa wanunuzi, ni vema Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa mamlaka aliyonayo akaona busara ya kutoa msamaha wa madeni hayo makubwa wanayodaiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri aelewewe kwamba madeni mengine yana miaka 10 au zaidi, hivyo ni vigumu sana kwa wafanyabiashara kuweza kulipa madeni hayo. Nashauri Mheshimiwa Waziri atoe msamaha wa hayo madeni ya *Motor Vehicle Licence* ili waanze ukurasa mpya na wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri mambo mawili muhimu katika suala la mashine za *EFD*. Kwanza, kuna maeneo mengi katika mikoa ya nchi hii ambayo hayajalazimishwa kutumia *EFD machine*. Mikoa kama ya Dodoma na mingineyo, biashara nyingi kubwa hazina *EFD machine* wakati Mkoa kama wa Kilimanjaro biashara ndogo tu zinatumia *EFD machine*. Naishauri Serikali ihakikishe *EFDs machine* zinatumika sawasawa na kwa haki nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, *EFDs machine* zinaharibika mara kwa mara, hivyo kuwafanya wafanyabiashara wabebe mizigo mikubwa katika kuzirekebisha au kufanya matengenezo; na għarama za matengenezo ni kubwa kuanzia kati ya Sh.50,000/= mpaka Sh.150,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Upotevu wa Mapato ya Serikali: Waziri wa Fedha akichukua mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naamini tutapiga hatua. Upotevu wa mapato ya Serikali upo wa kutosha katika vyanzo vyetu. Mfumo wa *machine* za *EFD* lengo lake ni zuri kabisa lakini bado kuna upotevu mkubwa japo *machine* hizo chache zilizopo pia baadhi ya wafanyabiashara huidanganya Serikali. Ni lini mtaongeza *machine* za *EFD* kila Wilaya nchini ziwepo za kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inasimamia wafanyabiashara ambao wanafanya udanganyifu katika biashara zao? Unakuta mfanyabiashara tayari ana risiti za bidhaa ambazo zinakuwa na bei ya chini. Je, kupitia hili ni wafanyabiashara wangapi wanakwepa kuandika katika *machine* bei ya halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukadiriaji wa kodi kwa wafanyabiashara ni kero na jambo hili linafanyika siyo kwa maslahi ya kuwasaidia wananchi, bali inawaumiza. Unawezaje kumlipisha kodi mfanyabiashara kabla ya biashara yake haijasimama? Je, hamwonni kuwa ule mkakati wa kupunguza umaskini kupitia kupungua makato makali ya kodi umefeli? Je, mpango wa kupunguza umaskini umefeli? Shilingi milioni 50 kila kijiji nadhani sasa ni muda muafaka wananchi wapewe fedha walizowaahidi katika llani ya CCM, watekeleze ili Watanzania wapate ahueni ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya Taasisi za Fedha zimekuwa zinakwepa kodi na kumekuwa na ufinyu wa ufuutiliaji wa matumizi ya fedha katika Taasisi za Serikali; *TBI, TANAPA, TANESCO, DAWASCO*: Je, nani anafuutilia hili na kutoa taarifa kwamba matumizi ni sawa na kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwenye Taasisi zisizo za Serikali baadhi zimekuwa zikipunguza gharama, hivyo

hazisemi ukweli na hivyo Serikali inashindwa kupata kodi ambazo ni halisi. Nini mkakati kuelekea Bajeti Kuu ili kusimamia taasisi hizi ili zilipe kodi halali na siyo kuiibia Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Jamii ya PSPF na NSSF ilikuwa na lengo zuri sana lakini katika kuwasaidia watumishi na wastaafu, changamoto ni moja kubwa katika mifuko hii ya jamii. Unakuta mtumishi amestaafu na anaishi mkoani na ni kijijini; ili apate mafao yake inampasa afuatilie mafao yake na inamlazimu kufika Makao Makuu na ukizingatia mifuko hii mingi iko mikoani. Kupitia bajeti hii, huu usumbufu utakwisha lini ili wananchi wapate huduma hizi kwa wakati, lakini pia wasisafiri umbali mrefu kufuata haki zao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu ubadhirifu wa mapato na matumizi katika Halmashauri (Mpanda). Kulikuwa na ununuzi wa gari la taka zaidi ya shilingi milioni 100, gari halipo; Kumekuwa na ununuzi wa mashine ya kusaga na kukoboa zaidi ya shilingi milioni 90, haipo; vile vile kuna matumizi mabaya ya ardhi nje ya makubaliano na mikataba (shamba la Benki NBC – Kakese (Mpanda).

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na uchumi imara na kuwa na mchango mkubwa wa pato katika uchumi ni muhimu Wizara kama msimamizi wa uchumi nchini iwe na kipaumbele katika ujenzi wa uchumi wa viwanda. Nashauri kwamba Wizara iwekeze katika viwanda vinavyohusiana na kilimo ili kuchochaea uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo jema kuwa suala la *pension* kwa wastaafu limezingatiwa katika bajeti hii. Nashauri kwamba uhakiki ukamilike mapema na malipo yafanyike kwa wakati wakiwemo waliokuwa watumishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) ni muhimu sana katika kudhibiti nidhamu ya matumizi Serikalini, lakini imekuwa

haiwezeshwi kwa kiwango cha kutosha. Hivyo, nashauri CAG apewe fedha za kutosha kulingana na bajeti yake na fedha hizo zipatikane kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa umuhimu wake ipewe mtaji wa kutosha na kutanua mtandao wake ili iweze kuwafikia watu wengi zaidi wanaohitaji huduma yake hasa walioko vijijini, mfano, Ukerewe. Pia ukopeshaji katika benki hii utoe fursa vile vile kwa Sekta ya Uvuvi kunufaika na benki hii jambo ambalo litaongeza sana nguvu ya kiuchumi ya watu wetu hasa vijijini.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa kumpongeza Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu, Manaibu Makatibu Wakuu, pamoja na Uongozi mzima wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa hotuba yao nzuri ya mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kwa leo nichangie eneo la Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Hili ni eneo muhimu sana na ni sawa na mishipa ya binadamu inavyopitisha damu. Mapato yanayotokana na kodi mbalimbali ndiyo ambayo yanaweza kupeleka maendeleo ya dhati ya nchi yetu. Naishauri Wizara kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania bado haijaweza kuinua wigo wa kukusanya mapato kwa sababu bado kuna maeneo mengi ambayo wenzetu wa *TRA* hajaweka utaratibu wa kukusanya mapato, nako ni sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huko kuna mapato mengi sana, lakini *TRA* hawakusanyi kodi, mfano ni watoa huduma za ushauri (*consultants*), wafanyabiashara ndogo ndogo; jamii yote hii inatumia miundombinu kama barabara, hospitali na kadhalika ambazo zinajengwa kutohakana na sekta rasmi. Nadhani umefika wakati sasa Wizara kuitia *TRA* waandae mazingira rafiki ya sekta isiyo rasmi iwe sehemu ya kuongeza chanzo cha mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni muhimu katika kukusanya mapato na ambalo halijawekewa

mkazo mkubwa ni kutumia *EFDs machine*. Mfano wa kutumia mashine za kielektroniki katika kukusanya mapato ya Serikali ni vyanzo muhimu sana. Bado Wizara kupitia *TRA* hajiasimamia utaratibu wa kutumia mashine hizi kwa mantiki kwamba siyo taasisi zote pamoja na watu binafsi wenye kuendesha biashara kubwa na ndogo, wanaotumia mashine hizi. Hili linaisababishia Serikali upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe mashine hizi zinapatikana kwa wingi na kwa bei za chini ili kila mtu aweze kununua na kutumia. Mfano ni mahotelii mengi hata hapa Dodoma hawatumii stakabadhi za *EFDs* na sijaona kama wenzetu Mamlaka ya Mapato wakichukua jithhada za dhati za ukaguzi. Tulichukulie suala hili kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia nichangie juu ya bajeti za Wizara na taasisi zetu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Utaona kwamba kiasi kilichopelekwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na fedha za maendeleo, takriban utaona ni asilimia 50 au pungufu ndizo zilizopelekwa. Hii inatoa tafsiri kwamba bajeti yetu haitoi uhalisia wa makisio yetu. Nashauri sasa tuweke bajeti ambayo itaakisi uhalisia japokuwa asilimia 80 hii itasaidia kufikia malengo ya Serikali yetu, kuliko kuweko makisio makubwa ambayo ni nadra kuyafikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kutokupeleka fedha kwenye Halmashauri kama ziliviyopitishwa katika bajeti. Kama tunavyoambiwa Serikali inakusanya fedha wakati mwingine hadi kuvuka lengo, kwa nini sasa hazipelekwi katika Halmashauri zetu? Kutokutoa *OC* za Idara za Halmashauri zetu ni kuzidhoofisha na kusababisha makusanyo

wanayokusanya kushindwa kufanya kazi iliyokusudiwa na badala yake fedha hizi za makusanyo ya Halmashauri kutumika kama *OC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokulipa madeni ya Wazabuni kwa wakati, wakiwemo Mawakala waliosambaza pembejeo. Hii ni kuendelea kufanya wananchi wafilisike na kufilisiwa na taasisi zinazotoa mikopo ya fedha na vile vile kufanya huduma zilizokusudiwa kutotolewa kwa wakati na kwa kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kushindwa kurejesha asilima 30 ya makusanyo yanayotokana na makusanyo ya kodi ya majengo, hivyo kuyumbisha malengo na bajeti za Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Serikali kuheshimu bajeti zinazopitishwa na Bunge. Matumizi ya fedha za Serikali yafuate bajeti iliyopitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. MAFTAH A. NACHUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu na kitichako na katika Wizara hii ya fedha naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kodi ya Majengo (*Property Tax*), naomba sana irudishwe kwenye mamlaka ya mwanzo ambayo ni Halmashauri ili ziweze kukusanya ipasavyo. Tangu Serikali Kuu ichukue kodi hii ya majengo, Halmashauri zimekosa mapato na kodi hii haikusanywi tena. Serikali Kuu irudishe kodi hii Halmashauri kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti iliyopita, kuna fedha nyingi sana hazijapelekwa Halmashauri ili miradi mingi iende kama ilivyopangwa. Ucheleweshaji wa fedha za maendeleo kama ilivyopangwa ni kurudisha nyuma kasi ya maendeleo nchini. Naomba suala hili liangaliwe ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitendo cha Serikali kukopa ndani ya nchi na hasa mashirika ya Hifadhi za Jamii kama vile *PSPF*, *LAPF*, *NSSF* na nyingine, kunaleta ushindani na wananchi wa kawaida ambao huweka fedha zao huko kwa wakati maalum hivyo wanapotaka kujitoa huwekewa vingi vingi kwa kuwa mifuko hii inakosa fedha. Pia Serikali inachukua muda mrefu sana kulipa madeni ya mifuko ya Hifadhi ya Jamii, hivyo mifuko hii hudumaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba, kwa kuwa inakopesheka nje ya nchi, basi ifanye hivyo ili mzunguko wa fedha ndani ya nchi kuititia mifuko hii ya Hifadhi za Jamii na mabenki yetu ziendelee kutoa mikopo kwa wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabenki hutoa riba kubwa sana kwa wananchi wanaowakopesha. Wananchi hawa hushindwa kulipa mikopo hiyo na hatimaye kufilisiwa mali zao na vitu vyao vya ndani, hivyo kuwafanya kuwa maskini zaidi badala ya kuwainua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge kila mwezi analipa fedha nyingi sana ya VAT na kodi ya mapato kuititia mshahara wake kila mwezi. Kitu cha ajabu, Wizara imewe kodi nyingine kwenye kiinua mgongo kilicholipiwa kodi kabla hakijawekwa kutunzwa. Hali hii ni mbaya sana na siyo ya kuvumilika kuweka kodi juu ya kodi kwenye *gratuity* ya Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Mashirika ya Umma yakaguliwe na CAG kwani matumizi yao, mfano kuna taasisi ya A/CC iliyopo Arusha ambayo kazi yake kubwa ni kujenga Vituo vya Mikutano kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha Sheria ya Taasisi hii ya A/CC. Bahati mbaya badala ya kufanya kazi yao, wanatumia shilingi bilioni 3.5 kwa kukarabati ukumbi wa Simba na huku wakijenga nyumba kubwa yenye ghorofa sita kwa shilingi bilioni 1.8 tu. Haiwezekani ukarabati uzidi majengo makubwa. CAG akague Arusha A/CC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vema Wizara ikaweka

katika bajeti zake shilingi milioni 50 za kila Kijiji ambazo ziliwekwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa nini haziwekwi kwenye bajeti?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri fedha za Mfuko wa Jimbo ziongezwe Mtwara Mjini, watu ni wengi, hazitoshii.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar ni visiwa; uchumi wake ni wa huduma kwa ajili ya kusaidia Tanganyika ili iweze kuendelea. Mfano mzuri ni Singapore na Malaysia. Leo Malaysia inakua kiuchumi kwa haraka sana. Gruiz au Meli za kitalii, leo zinaondokea Singapore. Kwa hiyo, watalii wote wanataka kusafiri na meli za kitalii wanakwenda Singapore ndiyo waanze safari yao. Singapore ndiyo nchi ya kwanza iliyorusha *Air Bus 380* kutoka Singapore kwenda Australia kwa mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kisiwa cha Penang kinachangia Malaysia kiuchumi kwa asilimia 60. Sasa wakati umefika wa kuiachia Zanzibar itekeleze uchumi wa huduma na baadaye kuisaidia Tanganyika kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Accountya Pamoja* ni lazima ifunguliwe na ianze kazi na mgawo wa mapato ya Muungano yawekwe wazi kila nchi ipate haki yake. Kuendelea kulipuza jambo hili litaleta madhara makubwa katika Muungano.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi hii. Naipongeza sana Serikali kwa juhudzi zake za kuleta maendeleo nchini. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu wake na timu yake yote ya wataalam inayowasaidia kutekeleza kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja niende kwenye utaratibu wa kupunguza umaskini. Vigezo vya MKUKUTA I na II ni kuwa na wastani wa kila mtaa kutoka Sh.770,464.3 mwaka 2010 hadi Sh.1,918,928/= mwaka 2015 kwa mujibu wa Mpango wa Taifa 2016/2017. Pia kasi hiyo inaendana na matarajio ya kutoka asilimia 24.5% iliyokuwepo

mwaka 2015 na kushuka hadi kufikia 16.7%. Njia kubwa ya kuondoa umaskini ni pamoja na kujitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba upatikanaji wa chakula kwa wingi chanzo chake ni upatikanaji wa mbegu bora, tafiti na umwagiliani na bajeti ya kutosha kwenye mahitaji ya kilimo. Ni kwa nini bajeti ya kilimo inaendelea kutengwa ndogo ambapo inahitaji mipango ambayo inaweza kuendeleza kilimo na kuweza kujitosheleza kwa chakula ili kuondoa umaskini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi au wahitimu waliochukua mikopo kwa ajili ya kuijendeleza. Wahitimu hawa waliingia mkataba na Bodi kwa kukubali kulipia 5% baada ya kumaliza masomo bila riba. Jambo la kusikitisha au linalowashangaza wengi ni kwa nini wameitwa wadaiwa sugu wakati wengi wao wapo kwenye Wizara za Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili Serikali imewashtukiza kwa kuongeza riba ya kutakiwa kulipa asilimia 15 badala ya 5% iliyokuwa awali. Ni kwa nini kwa vile wapo kwenye Wizara, Serikali isiwe inakata marejesho ya mikopo hiyo bila riba baada ya kurudi kwenye Wizara zao? Sheria ya kuongeza riba kwa mikopo hiyo ni kuwapa adhabu, kwani wengi wao ni maskini sana, hawana uwezo wa kifedha na hawataweza kujidoresha kimaisha. Ni vema kubaki na 5% kama awali ya mikataba yao inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa kauli kwamba mwaka 2015, Benki ya Wanawake ilifikia mtaji wa shilingi bilioni 20, lakini pia ilifungua vituo vya kutoa mafunzo na mikopo katika mikoa mbalimbali, jumla ya wananchi 12,874 wakiwemo wanawake 9,693. Nataka kujua mionganoni mwa wananchi waliopatiwa elimu hiyo kwa upande wa Zanzibar, imejipanga vipi? Kwani mtaji wa Benki ya Wanawake, baadhi ni michango ya hisa za Waheshimiwa Wabunge toka Zanzibar na hati za uthibitisho zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Pamoja ya Fedha, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa ujumla mashirika

tisa yanayotekeleza masuala ya Muungano kwa sehemu kubwa mtaji wake ultokana na Tanzania bara. Ni kweli, swali, je, kama mtaji umetokea upande mmoja wa Muungano, lakini upande wa pili ukawa umewekeza na rasilimali, taratibu za kimapato kwa mujibu wa sheria za nchi na Katiba ya 1977 zinasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Mazao ya Misitu Mafinga/Mufindi vs *TRA* Mkoa ni kubwa na inakua kwa kasi hasa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hususan Iringa na Njombe. Ni Sekta ambayo tulishirikisha wadau katika masuala yanayohusu sekta hii. Serikali itapata mapato na sekta ita-grow. Hata hivyo, hali ilivyo ni kinyume kabisa na hapa naomba niwe *open*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hulka yangu kama Mbunge niliyetokea kwenye Utumishi wa Umma, siyo mtu wa kupiga mayowe, lakini ninakoelekea nahisi nitaanza kupiga kelele na mayowe jambo ambalo siyo jema, kwa jitihada zangu kufuatia usumbufu uliokithiri kwenye *check point* ya Iringa. Niliwasiliana na Waziri na Kamishna Mkuu akiwa Kidatu kuhusu usumbufu na manyanyaso wanayopata wavunaji na wasafirishaji wa mazao ya misitu/mbao pale kwenye *check point* ya Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nifafanue kidogo. Uvunaji wa mbao uko wa aina kama mbili. Kwenye msitu wa Serikali ule wa *Sao Hill* ambaao mfumo wake uko very clear kwenye misitu na mashamba ya watu binafsi ambapo nako kuna mashamba makubwa kama kuanzia ekari hamsini na kuendelea. Ni wenye mashamba madogo kama ekari moja, mbili mpaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inatoka mvunaji mdogo ananunua kwa kuungaunga mpaka kujaza *semitrailer* au *Scania* ile tunaita kipisi, mtu huyu anasafirisha mbao lakini akifika *check point* ya Iringa anadaiwa risiti ya mashine ya *EFD*. Sasa mtu huyu aliyenunua kwa mwanakijiji ambaye hajui

chochote kuhusu *EFD*, itatoka wapi? Maana nimenunua kijijini kwa mkulima na hana mashine, maana yeze kauza nusu ekari ili apate fedha ziende kumlipia ada mtoto au matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjasiriamali huyu anatozwa faini kati ya Sh.250,000/= mpaka Sh.750,000/= wakati mzigo wake hauzidi Sh.3,000,000/= kabla ya gharama za usafiri. Mbaya zaidi watu wanatishwa, wanalipa fedha na hawapewi risiti. Fedha inaingia mfukoni mwa *individual*. Mtu huyo huyo akifika Kibaha anabugudhiwa kwa kuwa ni *syndicate*, wanapigiana simu na wale wa *check point* ya Iringa kisha wanamruhusu huyo mjasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifanya nini? Baada ya mawasiliano na Mheshimiwa Waziri na Kamishna wa Kidatu, nilipewa mawasiliano na Kamishna anaitwa Yusufu tukashauriana *TRA* Mkao ikae na wadau tujadili muktadha mzima wa biashara hii ili Serikali ipate chake na wajasiriamali walipe bila kufilisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha (lazima niwe wazi) Meneja wa Mkao akiwa ana shaka lakini nikawasihi kuwa mkutano nitausimamia na utakuwa wa amani na wa kujenga. Nashukuru tulikaa na tukaafikiana kuunda *Task Force* ikihusisha *TRA* na wafanyabiashara wa mbao. Hata hivyo bado uonevu unaendelea. Juzi hapa malori yamezuiliwa siku tatu. Kiuchumi hii ni hasara kubwa mno. Sitetei kuwa wasilipe, hapana tuwe na utaratibu ambao utazingatia mazingira halisi ya biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina kawaida ya *ku-personalize issues*, lakini kuna mtu anaitwa Onyango ana *damage* Serikali kwa vitisho, kauli na hata matusi. *He is not cooperative at all*. Amegeuka kero kuliko kuwa *facilitator*, labda kwa kuwa amekaa miaka mingi Iringa watu wa Iringa, Mafinga, Kilolo na Mufindi *are very humble* hawahitaji vitisho zaidi ya kuelekezwa tu, Mawakala wanawatisha watu, wanachukua rushwa, Onyango akipigiwa simu ni vitisho tu. *Please* naomba mtushirikishe mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauliza hivi nakisi ya bajeti ni 3.9% au ni 11.9%? Kwa sababu mikopo na misaada ni *around* trillioni 11 lakini deni la Taifa ni trillioni tisa na mikopo siyo uhakika. Kwa nini tuisimame kwenye kilio chetu? Naona kama we *are not realistic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia zaidi kwenye bajeti; lakini hili la mbao miltazame. Hii sekta ni uchumi mkubwa na angalieni Mufindi inavyochangia pato la Taifa, *one of the source* ni mbao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

MHE. BAHATI ALI ABEID: Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara iondoe kodi na tozo ya mitambo na vifaa vya miradi ya gesi ili miradi hii iweze kuendelea na utekelezaji wake kama ilivyopangwa kwani wakati mwingine miradi hii huwa ina mitambo mizito na mikubwa. Kama *TANROADS* huwa wanataka sheria iliyowekwa kwa ajili ya tozo hizi ziendelee kama zilivyo. Ni sawa, lakini miradi hii au mashine hizi ni za muda mfupi, siyo za kila siku. Naomba tuondoe tozo hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima hadi kufikia wakati huu tukijadili bajeti ya pili toka niingie katika Bunge lako Tukufu. Katika mjadala wa bajeti wa mwaka huu wa fedha tunaomalizia, 2016/2017, nilisema humu katika Bunge lako Tukufu kwa namna wataalam na hivyo Wizara hii mahsusи inayohusika na suala hili wanavyofanya suala hili muhimu kimazoea tu. Hii maana yake ni kuwa Wizara hii inaonesha kushindwa kutekeleza majukumu yake muhimu kama Waziri alivyoorodhesha katika hotuba yake hasa yale ya ukurasa 75 mpaka ukurasa wa 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inahusika au ndiyo yenye jukumu la uandaaji na usimamizi wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali? Mheshimiwa Waziri atueleze ni vipi jukumu

hili muhimu sana kwa uhai na mustakabali wa nchi yetu wamelitekeleza? Wizara zote zilizowasilisha bajeti zao zimeonesha hali ya kusikitisha kwa namna mipango, matarajio na utekelezaji wa malengo na majukumu yao ulivyokuwa chini sana. Eneo la bajeti za maendeleo kwa Wizara zote ndiyo limeathirika zaidi kwa kutopelekewa fedha ambazo Bunge lako Tukufu liliidhinisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali imekuwa mbaya katika maeneo yanayogusa moja kwa moja maisha ya wananchi kama vile afya, maji na huduma za usafiri, lakini pia katika eneo ambalo linabeba hadhi ya nchi yetu katika Jumuiya ya Kimataifa kwa maana ya Wizara ya Mambo ya Nje. Hotuba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Taarifa ya Kamati husika ya Bunge ameeleza hali za Balozi zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii inaandaaje bajeti zisizotekelzeza? Bajeti ya Serikali maana yake ni hizi bajeti za Wizara moja moja. Wimbo umekuwa ni ule ule miaka nenda miaka rudi. Kutenga fedha, kutopeleka fedha kunakohusika, kushindwa kutekeleza yale yaliyopangwa. Hebu tufike mwisho kwenye hili. Serikali ipeleke fedha zinazoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisoma bajeti iliyopita na Waheshimiwa Wabunge wengine na hasa Kambi Rasmi ya Upinzani wanasema kwamba tuwe na vipaumbele vichache vinavyotekelzeza badala ya wataalam kuachia Wizara kuwa mipango isiyotekelzeza. Hivi wataalam hawajui au ni nini hasa kinachoendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uwezekano kwa sehemu nyingine za hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri kwamba imerudia tu yale ambayo imekuwa ikiripoti miaka yote (i.e. *cut and paste*). Mheshimiwa Waziri anasema katika hotuba yake, ukurasa wa 75 aya 125, kuwa katika mwaka 2017/2018 itafanya uchambuzi na tathmini ya miradi ya kuondoa umaskini ngazi ya Wilaya na Viji. Hivi ni kweli muda wote huu uchambuzi na tathmini hajifanyika/haikufanyika? Utekelezaji utakuwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yamesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi waliopata fursa ya kuchangia kwa kuzungumza kuhusu masuala halisi kama vile deni la Taifa kutovumilika, viforo visivyomalizwa kama Tume ya Pamoja ya Fedha, mfano ya wastaaifu, riba za mabenki kwa mikopo kwa wananchi, ahadi ya milioni 50 kila kijiji na mengine yote yakionesha kushindwa kutekeleza yanayopangwa au yanayoahidiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalize kwa kuiomba Wizara hii ibadilike, ijipime kwa namna inavyotekeleza majukumu yake. Hivi ni kweli inaridhika na utendaji huu? Mbona Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wake ni watu makini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nina heshima ya pekee naomba kuwasilisha mchango wangu wa maandishi ili nami niweze kuwasilisha ushauri wangu juu ya ufanisi wa shughuli za Serikali chini ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nitapenda niguse masuala makuu matatu nayo ni kilimo, ufugaji pamoja na miradi mikubwa ya uwekezaji kwenye sekta ya miundombinu hususan miradi ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ugomvi wa wakulima na wafugaji na hata migogoro kati ya wafugaji na Serikali yamekuwa yanakithiri siku hadi siku na moja kati ya vyanzo vingi vinavyopelekea migogoro hii ni pamoja na *conflict of interest*. Kwa upande wa wafugaji, wakati Serikali inaweka juhudhi za makusudi katika kuhifadhi *eco -system* kwa kusisitiza wafugaji wafuge kwa idadi ndogo ambayo ni *manageable*, wafugaji nao wamekuwa kwa muda mrefu wakiongeza idadi ya mifugo ili kuweza ku-*maximize profit* bila ya kuwa na mchango wowote kwa Serikali kuititia Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ya kawaida huko

vijijini unaweza kukuta mfugaji mmoja anamiliki ng'ombi 2000, mbuzi 500 na hata kondoo 300 lakini mfugaji huyu unakuta hachangii chochote kwenye miundombinu ya uhitaji wa wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kosa kubwa tena nafikiri lisilopaswa kufumbiwa macho kwa mfugaji mwenye umiliki wa idadi tajwa ya wanyama wenyewe thamani zaidi ya shilingi bilioni moja kufikia kudai Halmashauri imjengee bwawa la kunyweshea wanyama maji ama majosho ya kuogeshea wanyama. Ni Mawazo yangu na ushauri wangu kwa Serikali kuwa majosho, mabwawa, nyumba za Madaktari wa wanyama na gharama ndogo ndogo zinazofanana na hizi basi zisitoke tena Serikali Kuu kupitia Halmashauri na badala yake wafugaji washiriki kikamilifu kabisa kwenye ujenzi wa miundombinu tajwa kwani kwa kufanya hivi nao watakuwa *responsible* kwa miundombinu hiyo *in case* kutakuwa na uharibifu ama kuzuia uharibifu. Vile vile kwa wafugaji hawa wenyewe idadi kubwa ya wanyama itafika mahali watakuwali kwa wepesi kauli na miongozo ya Serikali juu ya kufuga kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niunge mkono hoja na maelekezo ya Serikali na kwa kupitia *speech* za Mheshimiwa Rais juu ya utayari wa Serikali, katika kutoa vyakula vya msaada naamini kabisa hakuna sababu yoyote ya Serikali kutoa chakula cha msaada na badala yake Serikali ihimize wananchi wawajibike katika kutafuta chakula, kuhifadhi na kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali yangu iweze kusaidia wananchi wake katika kushiriki kikamilifu kwenye kilimo, tumtoe Mkulima wa Taifa hili kwenye kilimo cha msimu mmoja kwenda kwenye kilimo cha misimu miwili kwa kufikisha pembejeo kwa wakati pamoja na kuvuna maji ya mvua ama kwa kuchimba visima au mabwawa ili kuwezesha kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Elimu Bure bado ni sera ya msingi na ina umuhimu mahsus katika ustawi wa

Taifa hili, lakini si jambo bay Serikali ikafikiria kuja kuponzeza baadhi ya *itemskwenye package* nzima ya elimu bure. Ikiwa tutafaulu kumnyanya mkulima na tukatengeneza ajira nafikiri elimu bure inaweza kufanyiwa tathmini kikamilifu ili kuona kama kuna sababu za msingi katika kuendelea na sera za elimu bure ama laa. Siyo mbaya Serikali ikaenda na sera ya elimu bure kwa miaka 10 ikiwa uchumi na pato la mmoja mmoja utaimarika basi nafikiri elimu bure yawezekana ikaja kuwa ni mzigo mkubwa kwa Serikali yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la shilingi milioni 50 kwa kila kijiji nalo linahitaji kuwa *redefined*, tunahitaji kuwa na tafsiri mpya juu ya umuhimu na *impact* tarajiwa kupitia gawio la milioni 50 kwa kila kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi naona kuna sababu za msingi kabisa kuchelewa kuitoa hiyo milioni 50 kama hatutakuwa na tathmini kamilifu juu ya umuhimu na matarajio ya Serikali juu ya gawio la shilingi milioni 50 kwa kila kijiji. Ni ushauri wangu kwa Serikali yangu kupitia llani ya Chama cha Mapinduzi iweze kueleza kwa ukamilifu hiyo shilingi milioni 50 ni kwa ajili ya nini, sera iseme matarajio ama mlengo wa Serikali juu ya gawio la shilingi milioni 50 kwa ukamilifu wake. Leo kuna watu wanafikiri hii fedha ni zawadi ya Serikali ama ujira wa uchaguzi kwa wananchi walituchagua, wengine wanafikiri hii fedha ni *VICOBA* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya ujenzi wa barabara, utamaduni tulionao kwa muda mrefu katika miradi hii ya barabara ni kwamba Serikali kupitia vyanzo vyake mbalimbali, imekuwa ndio ikifanikisha miradi ya ujenzi wa miradi mikubwa ya barabara kupitia makandarasi nje na ndani ya nchi. Nikiwa sipingani kabisa na utaratibu huu wa Serikali, lakini nafikiri ingekuwa jambo jema kabisa kama Serikali ingefanya tathmini (*cost and benefit analysis*) na kuona kama tuna sababu mahsus kwa miradi kama hii itegemee fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kuwa mifumo ya udhibiti juu ya ubadhirifu wa mali ya Serikali bado haijaimarika na ndio maana Mheshimiwa Rais bado amekuwa akikabiliana na zoezi la kuwawajibisha Watendaji Wakuu wa Taasisi za Serikali kila iitwapo leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo yangu ni kuwa Serikali iangalie upya juu ya umuhimu wa Serikali kushiriki moja kwa moja kwenye miradi ya reli, bandari, barabara, viwanja vyta ndege, madaraja, meli na umeme, ni mtazamo wangu kuwa miradi hii mikubwa mikubwa iachiwe taasisi binafsi (*private sector*), Serikali ibaki kukusanya kodi na mapato mengineyo. Fedha ya Serikali ibaki kwenye mahitaji muhimu mfano elimu, afya, ajira na hata ulinzi wa wananchi na mali zao. Kwa kufanya hivi Serikali itabaki na majukumu machache ya kisera na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja ya Serikali. Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Serikali yetu ya Awamu ya Tano, Mungu Mbariki Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera sana Mheshimiwa Waziri, Dkt. Philip Mpango na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji kwa kazi nzuri mnayolifanyia Taifa letu. Kazi kubwa ni pamoja na ongezeko la ukusanyaji wa mapato ambayo yamepelekea kulipa deni la Taifa kwa kiasi kikubwa. Nina ushauri katika eneo la misamaha ya kodi inayotolewa katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, mifugo, afya, michezo, elimu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa vema wataalam wakaisaidia Wizara kutaja vitu vyote vionekane katika sheria ili kuondoa usumbufo kwa maafisa wa TRA wanaohusika na utozaji kodi, kwani inapotokea jina la kitu husika hakikutajwa katika sheria wanalazimisha kutoza kodi. Vilevile sera ya michezo inaelekeza kutoa unafuu wa kodi kwa vifaa vya michezo na kutotoza kodi kwa vile vifaa ambavyo vimetolewa kama msaada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili kuna malalamiko mengi kutoka kwa wananchi ambao ni wadau wa michezo kwamba vifaa vya michezo viliviyotolewa kama msaada vinaozea bandarini. Hata hivyo, Mheshimiwa Makamu wa Rais aliahidi suala hili kufanyiwa kazi siku alipokuwa akizindua mazoezi ya viungo ya kila Jumamosi ya pili ya kila mwezi mwaka jana Novemba, 2016. Naomba Wizara ilifanyie kazi suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitakia Wizara kila kheri na naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii kuchangia kwa maandishi ndani ya Bunge lako Tukufu. Napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu na Wataalam wote katika Wizara hii ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo zilizotolewa Hazina ni shilingi bilioni 5.8 kati ya bilioni 740.15 ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge (sawa na asilimia 0.8), namna hii ya utoaji fedha za maendeleo kidogo (asilimia 0.8) ni dhahiri kwamba Hazina haijafanya vizuri kadri ilivyopangwa awali katika mambo ya maendeleo. Naishauri Serikali kuwa mara fedha zinapopatikana ziwe zinatolewa kadri zilivyopangwa na kupitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshauri Mheshimiwa Waziri kuwa ingawaje bado deni la Taifa linalipika, tuwe tunalipa kadri ipasavyo. Serikali ijitätidi kwanza kwa vyovoyote vile kulipa deni hili la Taifa, jambo hili litasaidia kuendelea vizuri na miradi ya maendeleo kwa hiyo, pale inapowezekana Serikali iendelee kulipa na kupunguza deni hili la Taifa badala ya kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaweza kutoa au kulipa suala hili kipaumbele. Hata hivyo, naipongeza Serikali kwa kipindi hiki, kulipa Shilingi Trillioni 4.64 kwa deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ihakikishe na kujitahidi ili madeni ya watumishi wote yaendelee kulipwa, ili kuwapatia moyo wa kufanya kazi kwa bidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa mapato; Serikali kusimamia mkakati kabambe wa ukusanyaji wa mapato kutoka kwa wafanyabiashara kwa kutumia mashine za kielektroniki (*EFD*). Ni vema kuwafuatilia wafanyabiashara ili wanaopaswa kulipa kodi wakalipe ni dhahiri wengine wanakwepa eti, hawana mashine au mashine mbovu, kiasi cha kupoteza mapato mengi. Wafanyabiashara hasa wafuatiliwe ili tuweze kupata mapato ya ndani yanayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa milioni 50 kwa kila Mtaa na kila Kijiji; ni kweli mwaka 2016/2017 hazikutolewa, tafadhalii vikundi vya wajasiriamali wanazisubiri kwa hamu. Nashauri hizo shillingi billioni 60 zillizotengwa kwa 2017/2018 jitihada iwepo, zipatikane na kutolewa kama ilivyopangwa. Naomba niwaambie Mheshimiwa Waziri, kuwa wananchi wanazisubiri sana, nashauri Serikali isichelewe kuanza kutoa fedha hizi angalau kwa awamu, isikike kuwa fedha hizi zimeanza kutolewa, hivyo itekelezwe kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma kwa wastaafu; nawapongeza kwa kazi nzuri ya Serikali kwa kuwatambua wastaafu. Nashauri Serikali iendelee kuangalia pensheni zao, bado wale waliostaifu zamani pensheni zao ni ndogo sana. Wastaifu wanaomba na pia nashauri kwa sababu waliifanya kazi nzuri Serikali yao, mara mishahara inapopandishwa na wenyewe angalau wapandishiwe pensheni yao ili kumudu maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mikopo, ni dhahiri kuwa wananchi kupokea mikopo kwa kutumia hati ya ardhi, bado benki nyingi hawatambui. Ni vema zifulikane benki zinazokubali hati hizi ili wananchi wa kawaida hasa wawewe kupata mikopo. Nashauri Serikali, Benki ya Kilimo pamoja na mambo yote iweze kuongezewa fedha ili wakulima wakope kwa urahisi ingawaje matawi ya benki hii bado hayajasambaa mikoani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunatambua kuwa asilimia 65 ya Watanzania wanategemea kilimo, pia viwanda (Tanzania ya Viwanda) vinategemea malighafi ya kilimo, ni kwa nini Serikali isichukue jukumu la kuongeza fedha kwenye Benki ya Kilimo ili wakulima wakope. Pia Serikali iangalie jinsi ya kuwaongezea fedha, Tanzania tunataka maendeleo ya viwanda ni vema wakulima tuwawezesha kwa njia ya mikopo nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukarabati wa mikakati ya kupunguza umaskini katika aya ya 26 limeongelewa suala na mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Ustawi wa Jamii, je nini tofauti ya kada hizi? Kwa nini isijumuishwe ikawa kada moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu taasisi za mafunzo aya ya 165, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijiji (IRD); pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 5,852 hadi 6,500 bado idadi hiyo ni ndogo ukilinganisha na idadi ya wanafunzi wanaoomba nafasi katika Chuo hicho na hivyo wakati mwininge kupunguza mapato na kufanya Chuo hicho kushindwa kujidhesha. Je, Serikali inasema nini kuhusu suala hilo? Je, Serikali inasema nini kuhusu kupeleka OCkwa wakati ili vyuo hivyo viweze kujidhesha na kufanya kazi zake za kutoa taaluma kikamilifu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *road licence* ni vema sasa Serikali ikaangalia upya mpango huu hasa kwa yale magari ambayo hayatembe. Ili kuondoa malalamiko kwa wananchi ni vema sasa tozo hii ikahamishwa kwenye mafuta ili mtumia chombo cha usafiri aweze kulipia tozo hiyo kwa chombo kinachotembea na yale yasiyopo barabarani yaachwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MHE. OTHMAN OMAR HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua fursa hii kuipongeza hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa ushauri ililoutoa juu ya kuishauri Serikali katika suala zima la kuleta maendeleo ya uchumi ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kero za taasisi tatu ambazo binafsi napenda nipate ufanuzi wa Waziri mwenye dhamana. Mapato yatokanayo na *A/CC*. Katika kikao cha 10 cha Mkutano wa Sita cha tarehe 10 Februari, 2017, Waziri wa Fedha nilimnukuu wakati akijibu swalii la pili la nyongeza liliolizwa na Mheshimiwa Ali Saleh kutokana na swalii la msingi Na. 110 ambalo lilihusu ruzuku ya Zanzibar kutokana na Shirika la *A/CC*. Mheshimiwa Waziri wa Fedha alijibu kama ifuatavyo nanukuu:

"A/CC haijawahi kupata gawio kwamba Joint Finance Commission na Ofisi ya Msajili wa Hazina wameunda kikosi kazi ili kusaidia kituo kupata faida na kuleta gawio Serikalini kuanzia mwaka ujao wa fedha".

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ya Waziri wa Fedha inakinzana na taarifa za shirika la *A/CC*, taarifa ya Waziri wa Mambo ya Nje na zile za Msajili ya Hazina. Taarifa ya *A/CC* inaeleza kwamba shirika linajiedhesha kwa faida na ufanisi mkubwa na kwamba halitegemei ruzuku ya Serikali na linachangia kwenye Mfuko wa Serikali. Naomba ufanuzi wa kina kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu mchango wa mapato ya *A/CC* Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), *TRA* inaleta usumbufu kwa Wazanzibari, unapoingiza bidhaa kwenye ardhi ya Tanzania Bara kutoka Zanzibar ushuru wake unalingana na bidhaa zinazotoka nchi nyingine. Ushuru wa bidhaa unaodaiwa na *TRA* na *ZRB* kwa mfanyabiashara wa Zanzibar inamfanya mtafuta riziki huyu kutoa ushuru mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni baadhi ya kero ambazo zinawakandamiza Wazanzibari na zinazowarudisha

nyuma kiuchumi. Naomba ufanuzi wa Waziri wa Fedha kuhusiana na *TRA* kwa wananchi wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (*TADB*), Benki ya *TADB* tayari imeshatoa elimu ya matumizi ya benki hii na tayari imetoa mikopo na kupokea maombi ya mikopo kwa wananchi wa Tanzania Bara. Jambo la kusikitisha, Benki hii licha ya kuwa hajafanya mambo hayo Tanzania Visiwani hata kujulikana na wananchi wa Zanzibar hawaijui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha apeleke huduma ya *TADB* Zanzibar kama huduma hii inavyotolewa kwa upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niipongeze Wizara ya Fedha kwa hotuba yao nzuri iliojaa matumaini makubwa. Naomba niishauri Serikali katika suala zima la *road license*, ni ukweli usiopingika kwamba Serikali inatakiwa ikusanye mapato ya kutosha ili nchi iweze kujindesha yenyewe, lakini mimi kama Mbunge nimegundua tunakosa mapato mengi kwa kulipia kila gari, ikizingatia magari mengi yamekuwa na mengine yamekatwa skrepa, Serikali inayavizia ilyaone barabara ili yakamatwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa ukusanyaji huu tutakuwa tunapoteza mapato mengi sana. Niishauri Serikali longeze hata shilingi tano kwenye kila lita ya mafuta, ukipigia hesabu ya kila gari kwa mwaka itakuwa imelipia fedha nyingi sana, itakuwa mara kumi ya ukusanyaji huu unaotumika sasa, kwa kufanya hivyo Serikali itagundua ilikuwa inapoteza fedha nyingi sana kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali yangu kuhusiana na *TRA*. Kila *TRA* hasa za Wilaya zipandishwe hizi ziwe zinatoa huduma zote mfano *TIN* namba *road licence*.

leseni za udereva, *motor vehicle* na kadhalika. Serikali ikifanya hivi itaongeza mapato mara dufu kuliko ilivyokuwa sasa ukizingatia wananchi walio wengi wanaishi vijijiini, anaona ngumu kwenda kukata leseni mkoani hivyo yupo tayari aendeshe chombo cha moto kwa kujificha ili mradi asitumie gharama kwenda kutafuta vitu hivyo. Kwa hiyo, Serikali imekosa mapato kwa kutopeleka huduma karibu na wahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuhusu wafanyabiashara. Mfanyabiashara anakadiriwa mapato wakati hata hajafungua biashara. Niishauri Serikali ishawishi watu wafungue biashara kisha baada ya mwaka ndipo anafanyiwe makadirio kama sheria inavyosema. Sasa hivi *TRA* na wafanyabiashara ni kama maadui wakati Maafisa hawa wanatakiwa wawape elimu wafanyabiashara ili Serikali iweze kupata mapato au kukusanya mapato mengi zaidi kuliko ilivyokuwa sasa Maafisa wa *TRA* wanawatisha mno wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mashine za *EFD*, mashine hizi hazitumiki kama ipasavyo hasa katika Halmashauri zetu, kuna wizi mkubwa sana unafanyika katika Halmashauri baadhi kwani watendaji wengi wa Halmashauri wanatoa maelekezo kwa maafisa wanaokusanya ushuru kuwa kuna sehemu za kutumia risiti za *EFD* na sehemu nyingine wanatumia *manual*, hii inasababisha upotevu wa makusanyo na kuitia Serikali hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika Halmashauri nyingi hapa nchini hasa zile zinazotiliwa mashaka zifanyiwe ukaguzi wa mara kwa mara (*special auditing*), mfano Halmashauri yangu Lushoto inakusanya mapato mengi lakini mwisho wa siku unaambiwa mapato yameshuka. Mimi kama Mbunge napata mashaka sana na kama mnavyojua Halmashauri ya Lushoto ina wakulima na wafanyabiashara wengi, haingii akilini ukiambiwa kwa mwaka Halmashauri imekusanya asilimia 38 tu wakati huo unaona kuna vitu vya hovyo vinafanyika bila kufuata taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Halmashauri ya Lushoto ikafanyiwe *special auditing*, mimi kama Mbunge nimeliona hilo.

Mungu ibariki Tanzania, Mungu mbariki Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mjaalie afya njema na umzidishie umri ili aendelee kuwatumikia Watanzania hasa wanyonge wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kushika kalamu na kutoa mchango wangu kwa njia hii ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kujadili juu ya Mashirika ya Umma yaliyouzwa kwa bei ya kutupwa. Hapa nitajikita zaidi kwenye Shirika lilokuwa la Usagishaji la Taifa (*NMC*). Shirika hili lilikuwa na Matawi karibu katika kila mkoa lakini uuzwaji wake haukuzingatia thamani ya mali za shirika hilo. Mfano, kiwanda cha mahindi cha *Plot 33* hadi leo hakijulikani kama kimeuzwa au hakijauzwa. Ndugu Amani na Ndugu Mwaipopo walikuwa Wakurugenzi wa Shirika hilo wamehodhi kiwanda hiki kwa faida yao, mpaka sasa mgogoro mkubwa baina ya hao niliowataja na mnunuzi wa awali ambaye alishinda tenda ya shilingi milioni mia sita (600,000,000/=).

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo kwa wastaafu, Serikali imekuwa na kigugumizi kikubwa juu ya kulipa wastaafu hasa kwa wale waliokuwa katika mashirika yaliyouzwa. Mfano, wafanyakazi waliokuwa Shirika la *NMC* Tawi la Kurasini hadi leo Serikali imeshindwa kuwalipa madai yao ingawa kesi yao imekwishaamuliwa. Hata hivyo, wafanyakazi wa *TTCL* nao wanaidai Serikali mapunjo yao, nao hadi leo hakuna kinachoendelea. Hawa ni watu walioitumikia nchi hii kwa uadilifu mkubwa. Hivyo ni bora Serikali ikamaliza na watu hawa kwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafao kwa wazee ambao hawakuwa wakifanya kazi katika mashirika au Serikalini, hawa ni wakulima je, Serikali ina mpango gani na wazee hawa ambao wakati wao walitulisha kwa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wingi wa kodi, bidhaa zinazotengenezwa hapa nchini zinashindwa kushindana kwenye soko kwa kuwa ghamama za uzalishaji ni kubwa sana zinazochangiwa kwa kiasi kikubwa na wingi wa kodi na wingi wa mamlaka zinazofanya kazi zinazofanana. Mfano, *TFDA*, *TBS*, *OSHA*, *FIRE* na kadhalika, jambo hili ni muhimu sana kuangaliwa upya, Wawekezaji wanashindwa kuja kuwekeza kwa wingi huu wa kodi na mamlaka za usimamzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika kilimo; sekta hii hajapewa kipaumbele kama inavyostahili shida kubwa hapa ni upatikanaji ardhi kwa wawekezaji. Jambo la uhaulishaji wa ardhi imekuwa ni kikwazo. Mfano, katika Halmashauri ya Liwale imepata mwekezaji wa kilimo cha alizeti lakini hadi leo anahangaika kupata ardhi, ni miaka miwili sasa. Sasa ni kwa namna gani tunaweza kuingia katika uchumi wa kati wakati sekta ya kilimo ambayo inaa jiri watu wengi hatuko tayari kuwekeza katika kilimo.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, Msajili wa Hazina Fungu Na. 7, kuziongezea uwezo taasisi zilizo chini ya Msajili wa Hazina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NARCO*, taasisi hii ingeongezewa uwezo wa kuwa na ranchi nyingi katika maeneo ambayo yana mifugo mingi. Pia taasisi iweze kutoa taaluma kwa wafugaji wa wanyama wa asili ili mifugo yao iwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Tanzania ni ya pili/tatu kwa mifugo Barani Afrika lakini pia ni nchi yenye migogoro ya wakulima na wafugaji, hivyo basi tutumie changamoto

na uimara huu kuptitia ranchi zilizo chini ya *NARCO* kuweka hali sawa. Pia taasisi hii ingepewa uwezo zaidi wa kuzalisha mitambo ya maziwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANAPA*; Tanzania ni ya pili duniani kwa kuwa na vivutio vya utalii baada ya Brazil. Hivyo, taasisi hii iwezeshwe zaidi katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, iongezewe uwezo wa kujenga miundombinu ili vivutio hivyo viwe vinafikika na watalii wa ndani na nje pia kujenga uwezo wa kuweza kuvitangaza vivutio hivyo ili kupata watalii wengi kwani uchumi tunao lakini tunaukalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSTECH*; (Taasisi ya Utafiti) kwa uchumi wa viwanda, tuwekeze zaidi katika kufanya utafiti hasa kwa kuwatia moyo wabunifu. *Income from Investment* pia Serikali iwekeze zaidi katika mashirika yanayofanya vizuri ili tuweze kupata pato kutoka kwenye uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Takwimu; Tunakwenda katika uchumi wa viwanda, lakini mpaka sasa kuna upotoshwaji wa takwimu kama vile sukari inayohitajika kwa matumizi ya ndani ya nchi, hivyo imepelekea kupata upungufu wa sukari na bei ikapanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuhusiana na uamuzi wa kuzidisha mwaka 2016/2017 asilimia 10 kwenye mafuta ghafi hatimaye bei imepanda na tunatumia mafuta hayo kutoka nchi jirani kwa magendo kutokana na kukosa takwimu sahihi. Ofisi ya Takwimu ipo wapi? Kwa nini hatuna takwimu sahihi? Kwa nini tunatumia takwimu za wafanyabiashara badala ya kutumia takwimu toka Ofisi ya Takwimu tukaacha kupotoshwa? Izingatiwe kwamba wafanyabiashara hawa wapo makundi mawili kila kundi linataka kuangusha mwenzake.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri wa Fedha na Mipango,

Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na Wataalam wa Wizara kwa kazi nzuri ikiwa ni pamoja na kuandaa hii bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi ya kusimamia mapato, jukumu la Wizara ya Fedha ni kusimamia udhibiti wa matumizi ya fedha za umma. Matumizi mazuri ya fedha, yanaweza kutekelezeka kama kutakuwepo na utendaji wenye tija kwa kada ya ukaguzi wa ndani pamoja na Kamati za Ukaguzi katika Halmashauri zetu. Imezoleka kuona Idara ya Ukaguzi wa Ndani kutofanya kazi zake kwa uhuru, kwa muundo tulionao sasa ambapo Mkaguzi wa Ndani anasimamiwa na Mkurugenzi wa Halmashauri. Pia hata Wakuu wa Idara ya Uhasibu imekuwa kawaida kutekeleza kazi zao kinyume na misingi na kanuni za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kushangaza imejitokeza katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kwa Mhasibu mwenye sifa na mwaminifu kuondolewa kwenye nafasi yake kwa kuwa alikataa maagizo ya Mkurugenzi kufanya malipo kinyume na kanuni. Huyu Mhasibu mwenye cheti cha juu cha uhasibu (*CPA*) amehamishiwa kufanya kazi za ukarani kwenye Sekondari ya Kijijiini. Pia Idara ya Ukaguzi wa Ndani akiwemo Mkuu wa Idara wapo katika wakati mgumu kwa vile waliandika ripoti iliyoibua ubadirifupi kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ripoti hiyo Baraza la Madiwani lilichukua hatua za kinidhamu kwa wahusika, lakini kwa sasa linapingwa na viongozi kiasi cha kuwagawa Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Wizara ya Fedha, kuimarisha Idara ya Ukaguzi wa Ndani ikiwemo idara hii kuwa huru (*Independent*). Pia Wizara ifanye ukaguzi wa miradi ya maendeleo ambayo kwa kiasi kikubwa kuna upotevu mkubwa wa fedha. Kuwepo na mkakati wa kudhibiti matumizi ya fedha za umma badala ya kusubiri ripoti za Mkaguzi (*CAG*) ambayo ni *postmortem*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Msajili wa Hazina ina umuhimu wa kipekee wa kusimamia Mashirika ya Umma. Mashirika ya Umma ni muhimu na chanzo kikubwa cha mapato yasiyo ya kodi. Lengo kuu la Ofisi ya Msajili wa Hazina ilielekezwa kuboresha utendaji wa Mashirika ili yatoe mchango mkubwa kwenye kuinua uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Msajili wa Hazina ifanye tathmini ya mashirika ambayo hayana tija na kuyatengenezea mkakati wa kuyafufua au kubadilisha malengo kupelekea yawe na tija. Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kuna mashamba makubwa yaliyokuwa ya Tanganyika *Packers* katika Mji Mdogo wa Mbalizi kutokana na Sheria za Mipango Miji mashamba hayo yanakosa sifa za kuwepo Mjini. Kutokana na hali hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imetafuta ardhi kubwa ya zaidi ya ekari 7,000 kuwa mbadala wa haya yaliyokuwa mashamba ya kunenepesha ng'ombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukumbusha Wizara, kukubaliana na ombi la Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ili uwekezaji wa iliyokuwa Tanganyika *Packers* uhamishiwe kwenye eneo mbadala ambalo ni muafaka kwa mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za kibenki hazijafika vijijini kama ilivyo mijini. Mabenki karibu yote yanasisita kuhudumia wakulima wadogo na wananchi wa vijijini. Huduma za kibenki ni muhimu sana kwa kilimo cha tija ambacho ndiyo mhimili wa uchumi wa Tanzania. Kutokana na changamoto za mtaji wa Benki ya Wakulima (*TADB*) napendekeza Serikali ielekeze *revolving fund* ya shilingi milioni 50 kwa kila kijiji kusimamiwa na *TADB*. Kwa kuipa *TADB* jukumu la kusimamia huu mfuko wa milioni 50 kwa kila kijiji utawezesha usimamizi mzuri wa huu mfuko na wakati huo kuiwezesha *TADB* kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

MWENYEKITI: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, najua muda siyo rafiki. Nina tangazo la tanzia, ni la masikitiko kidogo.

Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe anaomba niwatangazie Wabunge kwamba aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Moshi Mjini kuanzia mwaka 2000 - 2015, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo amefariki dunia leo asubuhi saa tano kasoro robo (4.45), katika hospitali ya *KCMC* ambako alikuwa amekimbizwa kwa matibabu.

Waheshimiwa Wabunge, taratibu za mazishi zinasubiriwa na taarifa itatolewa baadaye kwa hivyo, tunamwomba Mwenyezi Mungu aipokee roho ya marehemu na ailaze mahali pema peponi. Tulimfahamu sana huyu Mzee na Mzee huyu humu ndani kuna binti yake ambaye ni Mbunge mwenzetu kachangia, nilikuwa nimemruka nilipopewa taarifa hiyo, lakini kama ilivyo masuala haya yeye alikuwa hajapata taarifa hiyo, ndiyo maana akasema mbona umenitaja halafu umeniruka lakini ndiyo mipango ya Mungu. Kwa hiyo, tutaeendelea kupewa taarifa za msiba wa huyu Mzee aliyekuwa Mbunge mwenzetu wa Bunge liliopita.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, sina tangazo lingine, mchana mnajua muda ndiyo huo hatutaweza kupata nafasi kwa wachangiaji wengine tutakwenda *straight* kwa Naibu Waziri na Waziri baadaye ahitimishe hoja yake, mengine haya kwa sababu tunakuja kwenye Bajeti Kuu ya Serikali nadhani haya yanayohusiana na yale ya msingi kuishauri Serikali mtapata nafasi hiyo baadaye wiki ijayo.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 10 jioni leo.

(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

Waheshimiwa Wabunge, mchana kabla sijasitisha shughuli za Bunge, niliwapeni taarifa ya tanzia ambayo nilipewa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni kuhusiana na msiba uliotupata kwa aliyejikuwa Mbunge wa Bunge liilopita kuanzia mwaka 2000 hadi 2015, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo.

Sasa sote tunafahamu humu ndani tuna Mbunge mwenzetu ambaye Marehemu ni baba yake mzazi, Mheshimiwa Lucy Owenya. Naelewa kwa mujibu wa kanuni zetu tukio kama hili halijatajwa, lakini kwa ubinadamu tu kwa sababu ni mwenzetu nilikuwa naomba tusimame kwa dakika moja ili angalau tutambue msiba huu uliotupata.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walismama
kwa dakika moja kumuombea Marehemu
Mhe. Philemon Ndesamburo)*

MWENYEKITI: Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya Marehemu Ndesamburo. Ahsanteni sana. Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Fedha na Mipango

(Majadiliano yanaendelea)

MWENYEKITI: Ahsante, tunaenda moja kwa moja, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Kijaji, una dakika 25 mtagawana na Mheshimiwa mtua hoja dakika 35. Karibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyejekiti, ahsante. Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru

Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliye niwezesha siku ya leo kufika salama na kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa ajili ya kuchangia hoja iliyowasilishwa jana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda niwataki Ramadhani njema na saumu zenye kukubaliwa wale wote wanaofunga mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema naomba sasa nichangie hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango katika baadhi ya hoja zilizopendekezwa na kuchangiwa na Waheshimiwa Wabunge katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ambayo napenda kuitolea ufanuzi ni hoja ilioletwa na Kamati yetu ya Bajeti nayo ilikuwa inapendekeza kwamba ni muhimu kitengo cha kusimamia Deni la Taifa kufanya tathmini ya ulipaji wa deni la Taifa kwa kuzingatia mapato ya ndani badala ya kutumia vigezo vingine kwa lengo la kuifanya Serikali ikope zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja hii napenda kusema kwamba, jambo la msingi ambalo tunatakiwa kujuliza, ni kwa nini tunakopa? Nim-quote mwanafalsafa mmoja alisema; *"What matters is not how much you have borrowed, but for what you have borrowed."* Kwa hiyo, hilo napenda tuliseme vizuri kabisa kwamba kinacho-matterzaidi siyo kiwango gani umekopa, lakini umekopa kufanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba deni ambalo tunaendelea kulilipa kama Serikali, Serikali yetu ilikopa kwa ajilli ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ili kufungua fursa za kiuchumi kwa wananchi wetu na Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sote ni mashahidi, miundombinu ya Taifa letu inaelekea kuwa mizuri, sasa

tunaona Taifa letu limefunguka kwa kiwango kikubwa, ni rahisi sasa kusafiri kutoka mkoja mmoja kwenda mkoja mwingine bila tatizo lolote. Ni rahisi kusafirisha bidhaa zinazotoka Sumbawanga kufika Dar es Salaam kwa muda wa siku moja au siku moja na nusu. Hii yote ni miradi iliyotekelawa kupitia mikopo iliyokopwa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hili tunajifunza kwamba uchumi wa Taifa letu unafunguka, ajira zinaongezeka katika Sekta za Kilimo, Sekta za Usafirishaji; na hii ni muhimu sana tuweze kuelewa tunapoliongelea deni letu la Taifa. Katika hili, wachumi wanasema, *bottleneck inflation* inaondoka kwa sababu sasa bidhaa inayozalishwa kutoka sehemu moja inaweza kusafirishwa na kufika sehemu nydingine ambako bidhaa hizo hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiashiria kilichopendekezwa na Kamati yetu ya Bajeti ni sahihi, kinatumika katika kupima kiwango cha uhimilivu wa deni letu la Taifa. Vile vile kuna viashiria viwili vinavyotumika na hiki kilichosemwa ni kimojawapo kati ya hivyo. Kiashiria cha kwanza ni kiashiria ambacho kinapima uwezo wa Taifa letu kuendelea kukopa (*solvency indicators*). Katika *solvency indicators* kuna viashiria vidogo vitatu, cha kwanza ni thamani ya sasa ya jumla ya Deni la Taifa kwa Pato la Taifa letu (*present values to total public debt*) ambayo nayo inaonekana bado tuko vizuri tunaweza kuendelea kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *indicator* ya pili ni thamani ya sasa ya deni la nje pekee kwa Pato la Taifa (*present value to external debt*). Nayo pia tupo katika *level/nzuri*, hatujafika hata nusu ya viashiria ambavyo vimewekwa. Kiashiria kilichopendekezwa na Kamati yetu ya Bajeti ni hiki kiashiria kidogo cha tatu ambacho ni thamani ya sasa ya deni la nje kwa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili kwa sasa hivi tuko asilimia 145.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 250. Kwa hiyo, kwa uhalsia kabisa, bado Taifa letu linaweza kuendelea kukopa kwa sababu viashiria vyote vitatu kwa ajili ya ukopaji

vinaruhusu Taifa letu kuendelea kukopa. Katika hili, siyo kwenye kukopa tu, kiashiria cha pili kikubwa ni kiashiria kwa ajili ya uwezo wa Taifa lolote lille kulipa ambayo ni *liquidity indicators*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *liquidity indicators* kuna viashiria viwili vidogo, kiashiria cha kwanza ni ulipaji wa deni la nje kwa mapato ya ndani ambayo kwa sasa tupo katika asilimia 11.5 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20. Kwa hiyo, bado tuna uwezo wa kulipa madeni yetu kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiashiria kidogo cha pili, ni ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mauzo ya bidhaa nje ambapo Taifa letu tuko katika asilimia 7.8 ukilinganisha na ukomo wa asilimia 20. Kwa hiyo, viashiria vyote vya kukopa na vya kulipa vinaonesha bado Taifa letu la Tanzania tuna uwezo wa kukopa na tuna uwezo wa kulipa bila tatizo lolote kabisa. Hiyo ilikuwa ni hoja ya kwanza ambayo nilipenda kuitolea ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ambayo pia Waheshimiwa Wabunge wengi wameichangia inahusu hilo hilo Deni la Taifa lakini katika nyanja nyingine, ambapo walisema takwimu zinaonesha kuwa kiasi kikubwa cha mapato ya ndani kinakwenda kulipia Deni la Taifa na hivyo Serikali kushindwa kugharamia masuala mengine ya maendeleo, ukatolewa na mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba kama nilivyosema kwenye hoja ya kwanza, Serikali yetu hukopa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Katika hili nilitegemea tupongezwe kwa sababu Serikali imeweza kulipa Deni la Taifa katika kipindi cha mwaka huu kwa kiwango kikubwa kwa kutumia mapato yetu ya ndani. Ndiyo ile niliyosema katika jibu la kwanza kuhusu *liquidity indicators*.

Kwa hiyo, tuna uwezo mzuri wa kuweza ku-service deni letu bila tatizo lolote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulipaji wa Deni la Taifa ni wajibu wa kisheria kabisa na hatuwezi kukwepa kama nilivyo sema mwanzo, tumekopa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Tuliingia makubaliano pia ambayo ni ya ukopaji pamoja na umuhimu wa kulipia miradi iliyotekeliza miaka ya nyuma wakati mikopo hiyo ilipopokelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ulipaji wa Deni la Taifa kwa kutumia mapato ya ndani ni mojawapo ya sifa kama nilivyo sema ya kuonesha uwezo wa kukopa zaidi na uaminifu. Tena tumeweza kulipa kwa mapato yetu ya ndani. Kwa hiyo, tunaonesha kwamba pamoja na kwamba tuna miradi ya maendeleo, lakini kipaumbele chetu ni kulipa ili tuweze kutengeneza sifa nzuri ya Taifa letu. Sisi sote ni wanadamu, tunaishi katika uchumi wetu na tunafahamu ukiwa na deni lazima kulilipa na ndicho ambacho tumekifanya. Kwa uhakika kabisa na miradi yetu ya maendeleo tutawenza kuitekeleza baada ya kuonesha kwamba Taifa letu lina dhamira ya dhati ya kulipa madeni ambayo tumeyakopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu ambayo ningependa kuitolea ufanuzi ilikuwa ni kuhusu Serikali kulipa shilingi bilioni 796 kati ya kiasi hicho inachodaiwa na wazabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti nayo ilipendekeza pia kuwa kwamba tuweze kuwalipa Wazabuni, Wakandarasi pamoja na Watumishi wetu. Tumekuwa tukiliambia Bunge lako Tukufu, Serikali yetu ina lengo la dhati kabisa la kulipa wakandarasi, watumishi, wazabuni pamoja na watoa huduma wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu imekuwa ikilipa madeni haya kulingana na upatikanaji wa mapato kama ambavyo Sheria ya Bajeti Namba 11 kifungu 45(b) kinavyotuelekeza kufanya. Katika bajeti yetu ya mwaka huu wa fedha, tulitenga kiasi cha shilingi bilioni 626 ili kulipa madeni haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi, kwa kuonesha dhamira njema ya Serikali yetu, tumeweza kulipa shilingi bilioni 796 zaidi hata ya bajeti tullyotenga kuonesha kwamba dhamira ya Serikali ni njema, tunataka kulipa madeni haya, tunawathamini wazabuni wetu wanaohudumia Shule yetu, Magereza pamoja na Majeshi yetu mengine. Tumekuwa tukiwalipa mwezi hadi mwezi na kitakwimu tunalipunguza deni hili kulingana na mapato ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzuia madeni haya yasiendelee kulimbikizwa, Wizara ilitoa angalizo na mwongozo kwa Maafisa Masuuli wote, kwamba hawaruhuswi sasa kuendelea kulimbikiza madeni haya. Ninavyoongea, kwa mwaka huu wa fedha hakuna deni lolote ambalo tumelimbikiza. Kwa hiyo, hii ni nia njema na lengo bora kabisa la Serikali yetu kuhakikisha kwamba sasa tumejiandaa kuwalipa watu wetu wanaotoa huduma, tunafahamu wanavyosumbuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwongozo huu uliotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali, niseme tu kwa Maafisa Masuuli kwamba yejote atakayekiuka mwongozo huu atakuwa amejifukuzisha kazi mwenyewe, kwa sababu Wizara imekuwa ikipeleka pesa kila mwezi kwa ajili ya malipo ya watoa huduma na wazabuni wetu.

Kwa hiyo, sisi kama moja ya Wajumbe wa Baraza la Madiwani katika Halmashauri tunazotoka, tuhakikishe pesa hizi zinapokuja kwenye Halmashauri zetu, zinatumika vizuri kulingana na maelekezo ambayo yanakuja na pesa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya nne ambayo ningependa kuitolea ufanuzi ni utekelezaji wa ahadi ya shilingi milioni 50 kwa kila kijiji, mtaa na shehia. Nimeona jana imesemwa kwa uchungu sana na Waheshimiwa Wabunge wameendelea kuisema. Napenda niseme kwamba hoja hii ilitolewa ufanuzi pia wakati wa bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini siyo vibaya mimi kama Naibu Waziri wa Fedha pia nikaweza kuisemea kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo imesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi kwenye hoja hii, ni kwamba kwa mwaka huu wa fedha Serikali yetu ilitenga shilingi bilioni 59.5 kwa ajili ya kuanza utekelezaji katika *pilot areas*. Wakati tunaendelea kutaka kutekeleza hili, zipo changamoto ambazo zimegundulika na hatuwezi kufanya makosa ambayo yaliwahi kufanya huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ambazo zimeonekana ni pamoja na changamoto zilizolikumbuka Taifa letu kutoptera na utekelezaji wa *JK Fund*. Hatutaki tena katika hizi milioni 50 kwa kila kijiji changamoto hii iweze kujirejea. Lazima tujifunze kutoptera na makosa yetu na tuweze kuyarekebisha na kuhakikisha kila kinachotolewa kinawafikia walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pilii ambayo imesababisha tuchelewe kutekeleza hili, ni wananchi kuwa na mtazamo hasi wa fedha hizi kwamba ni fedha za bure. Tunahitaji kufikisha elimu ya ujasiriamali kwa wananchi wetu, wapate elimu waweze kujua fedha hizi siyo za bure. Fedha hizi wanawezeshwa ili atakayewezeshwa leo iwe ni *revolving fund* aweze kuwezesha na wengine. Kwa hiyo, ni lazima tuandae wananchi wetu ili waweze kuzipokea na kuweza kuzifanya kazi ambayo ilikusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumegundua changamoto nyingine kuhusu vijiji vingi kuwa na vikundi ambavyo havijasajiliwa kisheria. Katika hili, vikundi havijasajiliwa kisheria na vipo vingine ambavyo vinasajiliwa specifically ili vipate fedha hii. Kiuchumi hiki ni kitu ambacho hakiwezekani, kwamba kinasajiliwa kikundi, kinasubiri pesa ili waanze utekelezaji, tunategemea nini? Ni kurudia makosa yale yale ambayo yalitokea huko nyuma na hili hatutaki tena liweze kutokea katika shilingi milioni 50 hizi, tunahitaji zionekane zina *impact* iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, Waheshimiwa Wabunge ni Madiwani viongozi katika Halmashauri zetu. Katika Halmashauri zetu, tunaona

changamoto pia za utekelezaji wa asilimia tano za *own source* ya Halmashauri zetu kwenda kwa wanawake na asimilia tano kwenda kwa vijana; utekelezaji wake haujaka vizuri. Kwa hiyo, baada ya kugundua haya yote, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja na Ofisi ya Rais, (TAMISEMI) wanaandaa utaratibu mzuri na utakapokuwa umekamilika, fedha zote hizi zitatolewa katika vijiji vyote ambavyo Serikali yetu iliahidi na tutaweza kutekeleza kwa asilimia mia moja ndani ya miaka mitano ya utawala wa Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo napenda kuitolea ufanuzi ilikuwa ni ushauri kuhakikisha kuwa pensheni kwa wastaafu inatoka haraka na kwa wakati ili kupunguza usumbufu kwa wazee wetu. Ushauri huu kama Wizara tunaupokea, lakini ninavyofahamu, wastaafu wote wanaollipwa pensheni kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, hata baadhi ya mifuko wanalipwa sambamba na mishahara ya wafanyakazi kila mwezi kwenye akaunti zao. Kwa hiyo, hakuna ucheleweshaji wowote ambaa unatokea hasa kwenye pensheni ya kila mwezi kwa wastafu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyowahi kuliambia Bunge lako Tukufu, tulikuwa tukiwalipa miezi mitatu mitatu, wakalalamika na sisi tukafanya *analysis* ya kutosha tukajiridhisha na sasa tunawalipa kila mwezi na wote wanapata pesa zao siku ambayo mishahara ya Serikali inalipwa. Niseme tu kwamba hili tunalichukua, kama ipo baadhi ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ambayo haliipi pensheni za kila mwezi kwa wakati, tutalifanyia kazi, tutalisimamia vizuri kuhakikisha wazee wetu wanaweza kupata pensheni yao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Kamati yetu pia ilishauri kwamba Serikali itimize ahadi yake ya kutoa *non cash bond* kwa ajili ya shilingi trilioni 2.6 ya mfuko wetu wa PSPF. Katika hili naomba kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba nimekuwa nikijibu maswali na nikiliezea Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ilikuwa inakamilisha tathmini na sasa tathmini imekamilika

kwa ajili ya hii shilingi trillioni 2.6 ambalo ni deni la kabla ya mwaka 1999 pamoja na malipo pia ya mifuko mingine ambayo iligharamia miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali yetu ni njema kabisa na sasa tuko kwenye hatua za mwisho kuhakikisha kwamba hii *non cash bond* inaweza kuandikwa na kuanza utekelezaji wake mara moja baada ya uhakiki na tathmini kuwa imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilitoka Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba Serikali iilekeze Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kuwekeza kwenye miradi yenyé faida na ya haraka hususan maeneo yanayochochea ukuaji wa uchumi kama vile reli na bandari. Katika hili naomba kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali yetu kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii imetoa miongozo ambayo imeainisha maeneo ya uwekezaji kwa kuzingatia faida na tija kwa jamii. Mojawapo ya maeneo hayo ni kama ilivyopendekezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba ni ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika miongozo hiyo, Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii kwa kushirikiana na Benki Kuu inaweka ukomo wa uwekezaji kwa kuzingatia athari za uwekezaji na siyo faida ya haraka. Unaweza ukapata faida ya haraka halafu baadaye uwekezaji ule ukawa siyo endelevu. Hilo haliwezi kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutatekeleza lile ambalo ni lenye faida endelevu kwa ajili ya mifuko hii kama tunavyojuu wateja namba moja wa mifuko hii ambao ni wastaa fu wetu ili waweze kuendelea kulipwa kwa wakati na muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna hoja ililetwa kwamba Serikali iweze kutoa taarifa ya hesabu za robo mwaka za kila Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Katika miongozo hii niliyoitaja ina kipengele inayojielezea mifuko hii kutoa

taarifa kwa wateja wao kila robo mwaka. Kwa hiyo, hili lipo na linatekelezwa na mifuko yetu yote ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili la Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kulikuwa na mapendekezo pia kwamba Ofisi ya Msajili wa Hazina ichukue usimamizi. Napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii pamoja na Msajili wa Hazina na Benki Kuu hushirikiana katika kuvisimamia mifuko hii ya hifadhi ya jamii. Kila mmoja ana majukumu yake na kila mmoja anatekeleza majukumu yake kama yalivyowekwa katika sheria na taratibu za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunaomba watu hawa watatu; Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi Jamii, Msajili ya Hazina na Benki Kuu wote kwa pamoja waendelee kunya kazi yao kwa pamoja ili kuhakikisha mifuko hii ya hifadhi ya jamii inafanya kazi kwa faida, kwa ajili ya wateja wao ambao ni wastaifu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kwamba kwa mujibu wa ripoti ya Benki Kuu mfumuko wa bei umepanda kutoka asilimia 5.4 mwezi Machi, 2016 mpaka asilimia 6.4 mwezi 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu kwamba mfumuko wa bei uliongezeka kutoka asilimia 5.1 mwezi Aprili, 2016 hadi asilimia 6.4 mwezi Aprili, 2017 ni sahihi na hii sote tunafahamu sababu kuu inayosababisha mfumuko wa bei ni tatizo la bei ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote ni mashahidi, sababu kubwa iliyotokea ni hali mbaya ya hewa katika msimu wa kilimo wa mwaka 2015/2016 kuliwasababisha upungufu wa mazao ya chakula katika masoko ndani ya nchi yetu. Hata hivyo, mfumuko wa jumla wa bei umeendelea kudhibitiwa na kubaki katika wigo wa tarakimu mmoja ambapo Serikali yetu imeahidi kwamba ni lazima tutahakikisha mfumuko wa bei unabaki katika tarakimu mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliambiwa tuseme na mikakati ambayo tunaitekeleza. Katika hili tunaendelea kuimarisha miundombinu ya masoko yetu na barabara kama nilivyosema mwanzo ili kuwezesha usafirishaji wa chakula kutoka eneo moja kwenda eneo lingine iwe ya urahisi na kuweza kuhakikisha kwamba upungufu wa chakula haupo kwenye maeneo ambayo hayakupata mvua za kutosha. Pia tunaendelea kutoa ruzuku ya pembejeo, kuimarisha huduma za ugani na uimarishaji wa miundombinu ya umwagilaji ili kupunguza utegemezi wa mvua katika kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaendelea kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na kuimarisha upatikanaji wake katika masoko yetu. Serikali yetu, ni wiki mbili tu zilizopita imeweza kutoa chakula kupeleka katika zile Halmashauri zilizoathirika zaidi na uhaba wa mvua na hii tumepeleka katika lengo hilli hilli la kuhakikisha *stabilization* ya bei ya chakula ili kuhakikisha kwamba mfumuko wa bei hauvuki ile *digit* moja kama nilivyosema mwanzo.

Hoja nyininge zilitoka kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, nayo ilikuwa ni kuhusu Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kuongezewa bajeti pamoja na kuha....

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kwa kusema kwamba nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliota hoja madhubuti na mijadala mizuri yenye tija kwa ajili ya uboreshaji wa bajeti yetu ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kwa kusema, naunga mkono hoja, hoja iliyowekwa mezani na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, ahsante sana. *(Makof)*

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa mchango wako. Sasa namwita mtoa hoja mwenyewe Waziri wa Fedha na

Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, unazo dakika zako 35. (*Makofii*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendesha vizuri mjadala huu wa bajeti kwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutambua michango iliyotolewa na Kamati ya bajeti chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Hawa Abdurahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini; na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kandege, Mbunge wa Kalambo, Iakini pia mchango uliotolewa na Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mombasa na Kaimu msemaji Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango; Iakini pia Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza au kwa maandishi hapa Bungeni. Ninawashukuru wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya Wabunge ambao wamechangia hoja niliyowasilisha, jumla yao 79 na kati ya hao 41 wamechangia kwa kuzungumza, waliobaki wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, ninafarijika sana kwa michango mizuri iliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wote. Nitapenda nieleze kwa muhtasari majibu ya hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge na ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa kunisaidia kujibu baadhi ya hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kabisa sitaweza kujibu hoja zote na wala kujibu kila kitu ambacho kimesemwa kwa sababu ya muda, Iakini naomba niwahakikishie kwamba majibu ya hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge tutazileta kwa maandishi kabla ya kuahirishwa kwa mukutano huu wa Bunge. Baadhi ya hoja nyingine kwa

hakika zilikuwa na mwelekeo wa Bajeti Kuu ya Serikali, basi nazo tutajitahidi kuzitolea ufanuzi kadiri inavyowezekana wakati wa mjadala wenyewe wa Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo hoja ambazo zimetolewa na Kamati ya bajeti; zipo zilizotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na zimerudiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi amba baadhi ya hoja hizo nitapenda nizitolee ufanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza kubwa sana ambayo nitapenda nitumie muda kuileza ni hoja ya upelekaji hafifu wa fedha na hasa fedha za maendeleo kwamba zimeathiri utekelezaji wa bajeti, lakini hasa miradi ya maendeleo. Bajeti ni maoteo; na maoteo maana yake ni kwamba siyo halisi. Ni maoteo ya mapato na matumizi ya Serikali katika mwaka mmoja. Sasa pamoja na jithada ambazo zinafanya kuhakikisha kwamba maoteo yanakaribiana na hali halisi, ulimwenguni kote ni nadra sana mapato yakalingana na matumizi. *Really, they seldom balance*, ndiyo maana Serikali zote duniani zinakopa. Zinakopa ndani na nje na ndiyo maana kuna kubana matumizi na kupunguza matumizi na ndiyo maana tunaweka vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa fedha kwa mafungu yote, unategemea hali halisi ya upatikanaji wa mapato. Hili limesitizwa katika kifungu namba 45(b) cha Sheria ya Bajeti namba 11 ya mwaka 2015. Najua Waheshimiwa Wabunge wengi wanao weledi wa kuelewa mambo haya upatikanaji wa mapato unategemea mambo mengi. Niseme mawili tu la kwanza, ni ukubwa wa uchumi lakini pia muundo (*structure*) ya uchumi. Kwa hiyo, kwa mfano, uchumi amba unategemea kilimo cha kujikimu au uchumi amba unakuwa na sekta kubwa isiyo rasmi ulimwenguni kote, maana yake ni kwamba wigo wa kukusanya mapato unakuwa ni mdogo. Ukilinganisha nchi ambayo ina *industrial base* kubwa, nchi ambayo ina viwanda vingi, wao wanakuwa na wigo mkubwa zaidi wa kukusanya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, viko vingi; nchi ambayo ina Serikali dhaifu na Baba wa Taifa alitukumbusha kama mna-*weak governance*, kama mna rushwa iliyokithiri, daima hamtakusanya mapato. Ni vizuri pia Waheshimiwa Wabunge tukakumbuka na hili nafurahi sana limesemwa na baadhi ya wachangiaji, tunalo tatizo kwamba hata fedha hizi ambazo zinatolewa, zinatumika vibaya. Kwa hiyo, haitoshi tu kusema tumepeleka fedha, ni lazima kuangalia ile *quality of expenditure*. Pale Hazina tuna Kitengo cha *Expenditure Tracking*, kwa kweli ukiangalia taarifa zao ni madudu matupu kwenye Serikali Kuu na pia kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taarifa mpaka unasikitika. Mtu anasema amenunua ubao wa mninga, lakini kanunua mpodo, bei tofauti. Ningeweza hata kutaja Halmashauri ambazo wanasesma wametumia fedha kwenye mradi; mradi haupo, ni mradi hewa. Uko udanganyifu vilevile, fedha hizi hizi ambazo tunapeleka, kumbe iko haja ya kuangalia mambo mengi, iko haja pia hata ya kuangalia Serikali yetu ukubwa wake, imepanuka haraka sana japo kwa nia njema kabisa ya kufikisha huduma kwa wananchi wake. Ni lazima tujitathimini tuangalie kama inaendana na uwezo wa Taifa letu kumudu ukubwa wa Serikali ambayo imefikia hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge, mwaka 1996/1997 tulifanya maamuzi kutohana na nidhamu ndogo ya bajeti. Kabisa kulikuwa hakuna *fiscal discipline* tukafanya uamuzi kwamba tutatumia fedha kadiri tunavyokusanya, tukaanza utaratibu wa *cash budget*. Kwa hiyo, ni lazima pia kutumia vizuri kile kidogo ambacho tunakusanya kulingana na uchumi wetu. Kwa hiyo, ndiyo sababu kubwa kwa kweli kwa nini fedha ambazo zimekusanywa mpaka hivi sasa, kigezo kikubwa ni uwezo wetu wenyewe wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, napenda nitumie *podium* hii kuwataka Maafisa Masuuli wote, tena wa mihimili yote, Serikali, Bunge na Mahakama kutumia

vizuri fedha hizi ambazo tunazikusanya kwa wananchi wetu masikini. Kila Wizara, kila Taasisi, Halmashauri, Mashirika, Mihimili yote ni lazima kujifunza kubana matumizi, kutumia fedha hizi ambazo tunakusanya kutoka kwa wananchi vizuri. Tusiangalie tu asilimia ya kiasi cha bajeti iliyokwenda, tuangalie hizo fedha zimefanya nini? Tuangalie uwezo wa taasisi mbalimbali kutumia hata hizi fedha ambazo ziko.

Waheshimiwa Wabunge, ziko taasisi ambazo hata hizo fedha ambazo zimebakii, wanazo kwenye akaunti mpaka leo hii. Kwa hiyo, ni muhimu sana viongozi wote tuhangaike kuhakikisha kuwa kila raia wa Tanzania anatimiza wajibu wake wa msingi wa kulipa kodi ili mapato yaongezeke, lakini ni lazima tuhakikishe kwamba na wale ambao wanakiuka huo wajibu wa msingi kwa kukwepa au kuvujisha mapato, lakini wanaendelea kufurahia huduma za Serikali, hao ni lazima tuwabane, hatuwezi kuwaacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyininge ambayo ilikuwa kubwa sana ni imani ya wafanyabiashara kwa maana ya *private sector confidence*. Hoja ilikuwa kwamba baadhi ya matamshi ya viongozi yanakimbiza watu, lakini pia biashara zinafungwa na kadhalika. Nisisitize kwamba *private sector confidence* ni jambo muhimu sana na ni lazima lilelewe, *it must be nurtured*. Sekta binafsi tulishakubaliana ndiyo injini ya uchumi wetu, lakini katika maeneo tofauti huwa nasema, Serikali na sekta binafsi zinafanana na mapacha walioungana. Kama mapacha walioungana wasipofanya mambo yao kwa pamoja na kwa maelewano, basi hayo maisha hayawezekani na kadhalika hivyo hivyo kwa upande wa Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika hivyo hivyo kwa upande wa Serikali na sekta binafsi na maana yake ni kwamba lazima pawepo majadiliano (*dialogue*) kuhusu malengo ya Taifa letu, kuhusu vipaumbele, sera na mikakati. Hii ndiyo sababu kati ya mikutano ya kwanza ambayo Mheshimiwa Rais amefanya mara baada ya kuchukua kijiti cha uongozi wa Taifa letu, mikutano yake ya mwanzo kabisa amekutana na wafanyabiashara chini ya utaratibu wa *TNBS*

na hivi karibuni amefanya nao tena mikutano na katika mkutano ule waliokuwepo ni mashuhuda siyo tu ameelekeza kwamba viongozi wa Serikali ambao watakwamisha juhudzi za sekta binafsi katika Taifa letu, hao wawajibishwe mara moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ameacha wigo wazi na kusema kwamba hata wafanyabiashara ambao wako tayari kuja kuweka viwanda yuko tayari kuwapa *tax holiday*. Sasa nafikiri ni vizuri kidogo tuwe tunayapima haya ambayo yanasesmwa. Mbali na *TNBC* katika ngazi ya kitaalam kuna majadiliano yanayoongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi chini ya *TPSF (Tanzania Private Sector Foundation)*, lakini katika ngazi za Mawizara tumeendelea pia kuzungumza. Siyo zamani sana, mimi na mwenzangu Mheshimiwa Waziri wa Viwanda tuliitisha mkutano hapa Dodoma, tukakaa na wafanyabiashara tukawasikiliza na tumekubaliana tataendelea kukutana kila baada ya miezi minne Wizara ya Viwanda na Biashara imekuwa inakutana na wenzetu kutoka Sekta binafsi kwa kuendana na sekta.

Kwa hiyo, tunazungumza na mlango uko wazi kabisa maana Taifa ni letu wote. Tanzania isipoendelea, hakuna cha kusema huyu ni wa Sekta binafsi na huyu ni wa Serikalini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana sheria za mchezo zikawa wazi pande zote. Ni lazima sheria za mchezo zisibadiliike badiliike, siyo upande wa kodi peke yake, lakini pia na mambo mengine nitaeleza kidogo. Ni lazima gharama ya kufanya biashara kwa wafanyabiashara wetu, ziwe ndogo kadri inavyowezekana na ndiyo maana Serikali inahangaika kuwekeza kwenye umeme, kuboresha usafirishaji, kupambana kidete na rushwa, lakini pia kupambana na ukiritimba kama Mheshimiwa Rais wetu anavyoongoza njia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo katika mchezo wowote, mchezo lazima uwe na pande mbili, Serikali inao wajibu, lakini Sekta binafsi nayo inayo wajibu. Kwa mfano,

ni muhimu sana sekta binafsi nayo izingatie *business ethics*. Ukwepaji kodi, madai ya marejesho ya kodi yasiyo na uhalisia lakini pia hata haya yaliyofichuka hivi karibuni kuhusu makasha ya mchanga ambayo yalikuwa yanapelekwa nje, ni kielelezo wazi kwamba hakuna uwazi na Watanzania tumekuwa tunaibiwa. Jamani hili liko wazi, hata watu ambao hawakwenda shule wanajua mambo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba viongozi wetu wana dhamana ya kulinda rasilimali za Watanzania kwa niaba yao. Kwa hiyo, pale ambapo kuna mushikeli wa wazi, ni lazima waseme na ukweli utabaki kuwa ukweli. Koleo haliwezi kuwa kijiko hata siku moja! Kama Mheshimiwa Rais mwenyewe anavyosema, msema kweli daima atabaki kuwa mpenzi wa Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nlongezee hapo kuhusu kufungua au kufunga biashara. Kufungua au kufunga biashara ni jambo ambalo limekuwepo tangu binadamu alipoanza kufanya biashara. Jambo la muhimu ambalo tunatakiwa kila mara kuzingatia ni kujua ni kwa nini biashara zimefungwa na kwa nini zimefunguliwa? Aina gani za biashara zimefungwa? Zipi zimefunguliwa? Sababu zake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape tu mfano Waheshimiwa Wabunge. Katika miaka ya 1980 ukiitazama China ilivyokuwa baadhi ya mambo haya tunayoyaona ya biashara kufungwa, siyo jambo geni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina kitabu hapa kimechapishwa mwaka huu ambacho kinaeleza juu ya uongozi ndani ya Kampuni ya HUAWEI, mila ambazo wanazifuata na jinsi ambavyo walikuwa wanaungana na wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kitabu hiki unaona kabisa kwamba *phenomena* tunayoiona sasa hivi hapa nchini, inafanana kabisa na wenzetu ambacho walikuwa wana-experience China wakati wanafanya mageuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja ninukuu kidogo sehemu ya kitabu hiki. Inasema hivi, nanukuu kwa Kiingereza kama kilivyoandikwa. Inasema: "*Over the decades of reform and opening up there have been many countless stories of rise, decline and heart-wrenching downfall of private companies, their many caucuses lining the street of transformation.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani anaeleza mengi tu kuhusu biashara zilivyokuwa zinafungwa na zile ambazo zilikuwa zinahangaika na mpaka zikaendelea katika mazingira yao. Kwa hiyo ni kweli kabisa zipo biashara zimefungwa lakini zipo nyingi zaidi zilizofunguliwa. Niseme tu kwamba biashara ambazo zimefunguliwa ni zaidi ya zile zilizofungwa, lakini pia ni muujiza kutarajia kwamba hizi ambazo ni nyingi zilizofunguliwa jana, basi leo leo zitakapofunguliwa zitazaa kodi kuliko hizo ambazo zimekuwepo na zimefungwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunafanya mabadiliko makubwa ya kimfumo. Kwa kweli hatuwezi kuendelea na uchumi ambao ulijengwa juu ya misingi ya utapeli na ujanja ujanja. Utaratibu uliokuwepo siyo endelevu na ulikuwa unawanufaisha watu wachache. Ni lazima tupige hii hatua na makampuni ambayo yanafuata taratibu hakuna mtu anayasumbua. Mfanyabiashara anayefanya biashara yake halali, anazingatia sheria huyo ni rafiki wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni kusema tutoe *amnesty* kwa wale ambao huko nyuma walizoea hivyo na tunawadai kodi; jamani mtakumbuka wakati baadhi ya makampuni yaliondoa makontena bandarini bila kulipa kodi, Mheshimiwa Rais aliwapatia wiki mbili za kulipa kodi. Sasa mnataka *amnesty* ipi? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja niseme kidogo juu ya Tume ya Mipango na hasa kwa sababu nina historia nayo; toka uhuru ukifuatilia historia ya Tume ya Mipango imekuwa inahama. Leo iko Wizara ya Fedha, kesho ni Wizara tofauti, kesho inakuwa Tume, kesho inakuwa kitu kingine. Nchi

nyingine utaratibu huo unaonekana wazi na huu ni mjadala ambao haujawahi kukamilika popote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo faida za Tume ya Mipango kukaa peke yake. Mimi nikiwa Tume ya Mipango, hoja ilikuwa kwamba nakosa hela za kutosha kuendeshea Tume kwa sababu Wizara ya Fedha iko mbali nami. sasa Tume ya Mipango imeunganishwa na Wizara ya Fedha, imekuja kinyume chake. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, pia naomba mkumbuke kwamba mwenye Mamlaka ya kutengeneza Muundo wa Serikali ni mwenye Serikali. Kwa hiyo, tumwachie maamuzi yake. Yeye anaona ni busara zaidi vyombo hivi viwili vikifanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejitalidi katika Wizara ya Fedha kama ambavyo tunafanya kwa Taasisi nyingine yoyote. Tumeipatia Tume ya Mipango fedha kulingana na upatikanaji wa mapato. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 Tume ya Mipango ilikuwa imepokea shilingi bilioni 2.84 ambayo ni sawa na asilimia 70.38 ya bajeti yake ya matumizi ya kawaida. Kwa hiyo, haiwezi kushindwa *ku-operate* kwa sababu hiyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuliambiwa pia kwamba tutoe fedha shilingi bilioni 1.9 zilizobaki kwa Tume ya Mipango ndani ya mwaka huu wa fedha. Kwa kweli hata kama fedha hizi zingekuwepo, Tume haiwezi kutumia fedha zote hizi kwa tija ndani ya mwezi mmoja uliobaki kabla ya mwisho wa mwaka. *Let us just be realistic.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwepo hoja hapa kwamba na ushauri kwamba Serikali ihakikishe Wizara, Idara na Taasisi zake zinatumia mashine za kieletroniki katika kukusanya maduhuli. Huu ni ushauri mzuri tunaupokea kwa moyo mmoja. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niliarifu Bunge hili kwamba nimeshatoa maelekezo na tulianza na Wizara zile

ambazo zinakusanya maduhuli makubwa kwamba wahakikishe wanatumia mashine za *EFD* katika kukusanya maduhuli ya Serikali. Niliahidi Bunge lako, tunapomaliza Bunge hili nitakwenda kuhakiki nikianza na Wizara Kuu ambazo zinakusanya maduhuli ya Serikali. Maafisa Masuuli wanisikie waliyeko hapa; wale ambao watakuwa hawatumii *EFD* hao basi wajiandae kwa shughuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tumeendelea na jitihada nyingine ikiwa ni pamoja na kutengeza *revenue get way system* ambayo itakuwa inatumiwa na Wizara na Idara mbalimbali katika kukusanya Maduhuli ili tuongeze tuboreshe usimamizi wa mapato. Kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, tumeanza kufanya majaribio ya mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwepo pia hoja kwamba katika mwaka 2015/2016 kuna Wakala 11 zillilipa takriban shilingi bilioni 2.97 kwa Wazabuni bila kudai risiti za kieletroniki na hii ilisababisha walipa kodi kukosa kodi na kuisababishia Serikali mapato. Naomba tena kusisitiza kwa Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali, kutumia Wazabuni waliosajiliwa na wanaotumia mashine za kieletroniki ili kuhakikisha kwamba mapato ya Serikali hayapotei, asiyefanya hivyo nimeshamwagiza Mlipaji Mkuu wa Serikali awadhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikumbushwa hapa kwamba ni muhimu Serikali iendelee kuchukua hatua zaidi kupunguza misamaha ya kodi na hususan kwenye mafuta, lakini pia kwenye makampuni ya uchimbaji madini ili tuweze kufikia lengo la misamaha yote kuwa chini ya 1% ya pato la Taifa. tunakubaliana kabisa na ushauri huu na ndicho tumekuwa tunafanya. Shida kubwa iko kwenye vivutio ambavyo ni vya kimkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, zimesikika sauti mara nyingi kwamba ni muhimu sana pia Taifa letu likawa linatoa vivutio ili kuvutia uwekezaji mwingi zaidi. Bado tunabishana, mimi ni mmoja wa watu ambao wanaamini kwamba kodi sio kivutio peke yake. Kwa hiyo, tutaendelea kuichambua hii mikataba lakini pia hata

kuhakiki yale maombi ya misamaha ili kuhakikisha kwamba hautumiki kama upenyo wa uvujaji wa mapato. Lengo letu bado ni lille lille; na tulikuwa tunakwenda vizuri mpaka mwaka 2015/2016 misamaha yote ilibakia kuwa 1.1% ya *GDP*. Kwa hiyo, tulikuwa tumekaribia lengo kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kwamba Ofisi ya Msajili wa Hazina inafanya kazi kubwa sana kama msimamizi wa mali za Serikali. Tunakubaliana na tulichofanya mpaka sasa Wizara imeandaa Waraka wa Balaza la Mawaziri ambao una lengo la kurekebisha sheria iliyopo ili kuimarisha usimamizi unaofanywa na Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waraka huo sasa uko kwenye ngazi za maamuzi na kwa kweli Serikali tunaona huo umuhimu wa kuimarisha Ofisi hii, na tutaendelea kuijengea uwezo na hususan iweze sasa kuhakikisha kwamba vile viwanda vyote vilivyobinafsishwa, basi waliokiuka mikataba kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, tunavirejesha viwanda hivyo Serikalini kama hawawezi kuchukua hatua za dharura kuhakikisha kwamba vinafanya kazi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kwa nini Serikali inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya ununuzi wa ndege, wakati Kampuni yetu ya ndege ina upungufu mkubwa? Kwanza naomba tu niwakumbushe kwamba suala la kununua ndege mahususi kwa ajili ya kuimarisha Sekta yetu ya Utalii, ni kipaumbele ambacho kiko katika mpango wa pili wa maendeleo wa miaka mitano ambao ulipitishwa na Bunge hili mwezi wa sita mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani pia shirika hili ndiyo *national pride* na ndiyo maana Mheshimiwa Rais na Serikali yake, inahangaikia kupata ndege hizi. Nina hakika wamo Waheshimiwa Wabunge humu ambao wamenyanyasika sana na *delays* na *cancellations* za ndege za wenzetu kuja Dar es Salaam. Tutaendelea mpaka lini? Ziko hata nchi ndogo ambazo zina *airline* zake zinafanya kazi. Kwa nini watalii wapite nchi nyingine badala ya kupita hapa kwetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie kwamba tunatambua upungufu huu na ndiyo maana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekamilisha ukaguzi wa Shirika letu la Ndege ili kuweze kusafisha mizania ya hii kampuni, lakini pia tumeamua kwamba tutachukua madeni yote ya *ATCL* ili kuweza kusafisha hiyo mizania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameteua Bodi mpya ya Wakurugenzi ambayo ina weledi katika masuala ya usafirishaji wa anga na usimamizi wa fedha. Menejimenti mpya, lakini pia kuhakikisha kwamba shirika linakuwa na mpango wa biashara wa muda wa kipindi cha kuanzia mwezi Julai mpaka Juni, 2017. Pia wameandaa mpango wa biashara na hatua zote hizi zinalenga kuwa na Shirika la Ndege ambalo litachochea ukuaji wa Sekta ya Utalii, lakini pia kubakiza *pride* ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja juu ya Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kwamba kwa ye ye kuomba fedha Wizara ya Fedha, basi anakuwa omboomba, anapoteza uhuru. Kwanza naomba niseme tu kwamba ni *good practice* kwamba taasisi yoyote ya umma lazima iwe na mahali pa kuomba fedha. Hata mwenye mamlaka anapangiwa hata mshahara. Bajeti ya Ikulu, inajadiliwa humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu pia Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ikawa na mahali ambapo fedha zake zinapitia ili kuomba idhini ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili limeitendea haki bajeti ya *CAG*. Limekuwa linahoji pale ambapo tunakuwa kwa upungufu wa mapato tumeshindwa kumpatia fedha za kutosha, lakini kwa mwaka ujao wa fedha kama mtaipitisha bajeti ya Wizara yangu, tulikubaliana kwenye Kamati ya Bajeti kwamba Ofisi ya *CAG* kwa mwaka ujao basi ipewe fedha kama ilivyoomba na tutahakikisha kwamba fedha zinatoka kadri ukusanyaji wa mapato utakavyoruhusu. Uhuru wake uko pale pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna ofisi ambayo ina msaada kwa Wizara ya Fedha kama Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, huyu ndiye anayenifuchulia mchwa. Mheshimiwa Rais alinipa kazi ya kutafuta mapato na kuyagawa kwa mafungu mbalimbali ya Serikali, Ofisi hii ya CAGndiyo inanionesha nani anatumia vibaya. Kwa hiyo, kwa kweli Wizara ya Fedha itakuwa ni taasisi ya mwisho kabisa kuibana Ofisi ya CAGkwa ya maana kumpatia fedha za yeche kufanya kazi yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kuhusu Mfuko wa Pamoja. Akaunti ya Pamoja ya Fedha katika Serikali mbili, hoja ilikuwa kwamba hajafunguliwa na hatua zilizochukuliwa kuhusu suala hilo ni nini? Kufunguliwa kwa Akaunti ya Pamoja ya Fedha kwa kifupi, kutafanyika baada ya uamuza kuhusu mapendekezo ya Tume ya Pamoja ya Fedha kufikiwa na pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kila upande wa Muungano umeendelea kunufaika na mapato ya Muungano yatokanayo na kodi ya mapato, ushuru wa forodha na ushuru wa bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi yanayopatikana katika kila upande.

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Malizia tu Mheshimiwa.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme moja tu nimalizie hili kwamba kwa mwenendo wa sasa wa mgawanyo wa mapato ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inapaswa kupokea 21%, ndiyo ilikuwa hoja kwamba ilitakiwa ipate 21% na SMT 79% ya mapato. Kwa mujibu wa hotuba ya bajeti ya Waziri anayesimamia masuala ya Muungano, mgao wa SMZ wa 21% na SMT 79% ni kuhusu ajira, siyo mapato. Ni kuhusu ajira katika Taasisi za Muungano na siyo mgawanyo wa mapato. Kuhusu mgawanyo wa mapato ya Muungano, mapendekezo yake bado yanafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, hoja ni nyingi na tutazijibu kwa maandishi. Naomba kwa heshima na taadhima niishie hapa nikilendelea kuomba kwamba Bunge lako Tukufu likubali maombi ambayo tumeweka mezani ili twende tukatekeleze kazi zilizoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makof*)

MWENYEKITI: Toa hoja.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa, Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja illitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja imetolewa, imeungwa mkono. Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgt*.....Sh. 7,371,377,000

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, ninayo majina nitaanza nayo. Tuna makundi mengi, lakini kwa sababu ya muda tujaribu tuone watatu wa kwanza upande huu na wawili upande huu. Safari hii nitakapofika huku nitaanza na *CUF*. Tunaanza na Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kupata ufanuzi kwa Waziri wetu wa Fedha kwa sababu Wizara ya Fedha ndiyo yenye jukumu kubwa la

kukusanya mapato na pia kusimamia matumizi yake, lakini pia kuweka sera nzuri ya kuhakikisha kwamba yote hayo yanaenda vizuri na hayawi bughudha na kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, niliandika kuomba Mheshimiwa Waziri aje atueleze kuhusu kuwa na muda maalum wa kikomo wa kukusanya kodi, tozo na ushuru mbalimbali kwa Serikali na Taasisi zake (*regulatory bodies*), kwa sababu sheria inapotungwa hapa Bungeni na kule kwenye Halmashauri na kanuni mbalimbali ambazo zinapitisha sheria, siyo kila mwananchi anapata fursa kujua zile sheria, ni jukumu la Serikali na hizo Taasisi kutoa elimu ili zile kodi na tozo zikusanywe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na wao kushindwa kukusanya kwa wakati huo, ni uzembe ambao unafanyika au wakati mwingine ni changamoto ya kifedha, unakuta inakaa miaka mitano, 10 au 15, wanakuja wanaanza kudai *backlog* yote. Hiyo ni moja katika sababu Tanzania *informal sector* imeendelea kuwa kubwa na wale walioko kwenye *formal sector* wanakimbia hiyo *formal sector* na kurudi kwenye *informal sector* kwa sababu ya kuogopa kwamba asije akitolewa mdudu huko, unakuja kudaiwa kitu cha ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano hiyo *motor vehicle licence*, leo watu wanadaiwa mpaka miaka kumi au 15 nyuma. Kwa mfano *SDL* na mifano mingine kama *TFDA*; ukija kwenye *fire, weight and measurements*; mtu anakuja kwenye labda hoteli ndogo iliyosajiliwa kwamba imesajiliwa mwaka 2001. *TFDA* ilitakiwa kutoa kibali kipindi hicho hicho, lakini wamekaa, leo 2017 wanakuja wanakudai hiyo ya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwamba tuwe na sheria. Mwisho pawe na kikomo kwamba kama ni miaka mitatu, ili huko nyuma kama kuna uzembe ulifanyika na hawakukusanya, mwananchi huyu asibebe huo mzigo. Hiyo itasaidia watu wengi kubaki kwenye *formal sector* na wasihame tena kutoka *formal*/kwenda *informal*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makampuni mengi yakifika miaka mitano au sita, wana tabia ya kubadilisha majina kwa sababu ya kuogopa hizo kodi na tozo ambazo hawazjui na wanakuja kufuatwa. Hata wakati wanapoenda kukata leseni, basi ilikuwa ni wajibu wa yule Afisa Biashara kumweleza huyo mtu kwamba wewe unatakiwa ...

(Hapa kengele illilia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. JITU V. SONI: ...leseni, uwe na moja, mbili tatu, nne, tano, tozo...

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo, naomba nimalizie kwamba pia kuna kodi...

MWENYEKITI: Hapana Mheshimiwa, muda umekwisha. Malizia...

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nisipopata majibu ya uhakika, nitazuia shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mtoa hoja.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kumekuwa na hasa siku za karibuni kwamba mamlaka iliyokabidhiwa kazi ya kukusanya mapato imekuwa ikienda kudai malimbikizo. Naomba nisisitize tu kwamba kila mlipa kodi kwanza lazima ajue wajibu wake. Kodi ni mali ya Serikali ili Serikali iweze kuhudumia wananchi wake. Kwa hiyo, kama unatumia sababu yoyote ile kutolipa kodi kwa wakati, Serikali ni lazima ibakize haki ya kuidai na ndicho kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya nchi yetu ambayo taarifa mbalimbali za biashara aidha zinafichwa kwa makusudi au kwa sababu mbalimbali, basi kodi stahiki hailipwi, ni vizuri na sheria ndiyo zinasema hivyo na sheria zilizotungwa na Bunge, kwamba Serikali bado iende

kudai ile kodi. Kwa hiyo, ukiifunga sana katika mazingira ya nchi yetu mimi nina hofu sana kwamba tutakuwa tumekwenda kupunguza sana uwezo wa Serikali kuendesha shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli namshauri sana Mheshimiwa Jitu Soni kwamba muiachie Serikali nafasi hii ya kuweza kukusanya hizo *backlog*.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba kutokana na mazingira anaona kwamba kuna watu wanataka kuficha taarifa, lakini siyo yote yanayojadiliwa humu Bungeni yanamfikia mwananchi hasa kwa mfano wa kule Babati. Miaka michache tu huko nyuma redio zilikuwa hazishiki, tv hazishiki, magazeti ni shida, huyo mwananchi wakati anaenda pale Halmashauri kukata leseni, si ndio alitakiwa kupata elimu yote kupitia Halmashauri yake!

Sasa kama uzembe unafanyika, kuna Ofisi ya *TRA* pale, unakaa miaka kumi na kitu; hatuzungumzii watu binafsi, kodi ya 2013 Halmashauri yangu imekamatwa...

MWENYEKITI: Mheshimiwa unatoa shilingi, hutoi!

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi, naomba ijadiliwe.

MWENYEKITI: Toa hoja bwana!

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja wenzangu waniunge mkono ijadiliwe.

MHE. MAULID S. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Haya tuchukue majina. Mheshimiwa Allan Kiula, Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Mheshimiwa Mtulia, Mheshimiwa Kigola, Mheshimiwa Omari Kigua na kwa upande wa Serikali Mheshimiwa *Engineer* Ngonyani na Mheshimiwa Suleiman, uko upande wa Serikali eeh! Mheshimiwa Kiula.

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja hii. Kwanza namwomba kabisa mtoa hoja arudishe shilingi na naomba Waheshimiwa Wabunge wote wakubaliane kwamba shilingi irudi, kwa sababu nchi haiwezi kuendeshwa bila kodi na kila siku huwa tunasema humu ndani kwamba kodi za ndani zinatakiwa ndizo ziendeshe nchi, siyo *international taxes*; na mlipa kodi ana wajibu wake na taasisi inayokusanya kodi ina wajibu wake na Sheria ya Kodi inapitishwa na Bunge. Kwa hiyo, hakuna nafasi ya mtu kusema kwamba mimi sikujua kwamba natakiwa kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unaonyesha, mimi nimefanya kazi *TRA*, watu wengi wanaodaiwa kodi wanajua kabisa kwamba wanapaswa kulipa kodi na wanakwepa kwa makusudi. Ukichukua takwimu, utaona kwamba watu wachache sana ambao hawana uelewa huo ndio wanapata tatizo hilo, lakini watu wengi wanajua na ni wa....

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mtulia.

MHE. MAULID S. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii adhimu kabisa ya mimi kuchangia. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Jitu Soni pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha kwamba watu hawapewi taarifa za kudaiwa kodi kwa wakati, lakini mbaya zaidi limefanyika jambo linasikitisha sana kwamba mtu anaombwa taarifa zake za kulipa kodi anaonesha, Maafisa wetu wanasema aah, inaonekana ulikadiriwa vibaya, wanamkadiria upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wetu wameiata hasara kubwa; unakadiriwa kodi upya za miaka mitano, mtu analipishwa shilingi bilioni mbili, shilingi bilioni tatu. Kwa utaratibu huu wafanyabiashara wetu tunawaua bila sababu. Ni lazima *TRA* itekeleze wajibu wake kwa kukusanya kodi kwa wakati. Kama kweli wanashindwa kukusanya kodi kwa wakati, kwa nini wanaongeza kodi za *property tax* wanachukua wao kumbe hata kukusanya kodi kwa...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa, muda ndio huo. Mheshimiwa Kigola.

MHE. MENDRAD L. KIGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Jitu. Hapa *issue* siyo kwamba watu wasilipe kodi, kila mtu ana wajibu wa kulipa kodi. *Issue* ni kwamba wanatakiwa kumkumbusha yule mfanyakibashara anayedaiwa kodi. Kwa mfano, hata masuala ya viwanja, watu wamekaa miaka kumi, miaka 20, watu wanajisahau, hakuna *message* inayokwenda kumkumbusha. Kwa hiyo, tunachotaka hapa *TRA* na wahusika wa kukusanya kodi wakumbushe hata kwa *message*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupa mfano, watu wa ving'amuji unaweza ukaona king'amuji chako hujalipia lakini *message* inakuja kwenye simu yako, kwamba mteja unatakiwa kulipia king'amuji chako. Wanakumbusha hata kwa *message* tu. Tunachotaka sisi, watu wakumbushwe kwa njia ya *message* au kwa njia yoyote ile ili waweze kulipa kodi. Hiyo ndiyo *issue* ambayo iko hapa kwa Mheshimiwa Jitu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kigua Omari.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Kwanza niseme kwamba

naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Jitu hapa. Suala la kodi ni suala la lazima na nchi haiwezi kwenda bila ya kodi, lakini kwa utaratibu upi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Mheshimiwa Waziri akubali hapa kwamba suala hili linaleta kero na linaleta chuki kwa wananchi. Lazima tukubali hapa kwamba pawe pana *time frame* kwamba ni miaka mitatu au miaka mingapi? Tuchukulie tu suala la magari; gari ya mwaka 1994 iko *garage*, leo unamfuata mwenye gari aweze kulipa kodi. Ni sawa, tuweke basi utaratibu. Kama hilo umeliamua liwe hivi, tuweke utaratibu wa kulipa taratibu ili Serikali ipate mapato lakini pawe pana utaratibu rafiki na wananchi wetu isiwe ni chuki. Ahsante. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Nami naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Jitu Soni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kwamba *ignorance of the law is not an excuse*, lakini kwa vile nia ya Serikali ni kuongeza mapato, basi kuna kila haja Serikali ikawa inatenga bajeti kwa ajili ya kuelimisha umma ili ulipaji wa kodi *compliance* iongezeke bila kutoza kodi kwa kushurutisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile nia ya Serikali ni kuongeza wigo wa mapato na tunataka tulete *informal sector* kwenye *formal sector*, hii *case study* aliyoleta Mheshimiwa Jitu Soni inaonesha namna Serikali inavyohitaji kujipanga ili ku-*attract informal sector* iweze kuja kwenye *formal sector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sidhani kama nia ya Mheshimiwa Jitu Soni ni kushika shilingi, anataka kupata *commitment* ya Serikali namna inavyojipanga kuhakikisha

tunakuwa tunajenga *compliance* ya wananchi bila kushurutisha ili tuweze kuongeza mapato bila kuwakandamiza wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer Ngonyani*.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa. Naamini Mheshimiwa Mto Hoja ameelewa kwamba shilingi irudi na sababu kubwa ni kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge ndio tunaopitisha Sheria za Kodi humu ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunachoongelea, hoja aliyoitao Mheshimiwa ni kusamehewa, kwamba wewe umekaa miaka kumi, 15 hujalipa kodi, sasa unasema usamehewe, badala yake ulipe miaka mitatu tu ya karibuni. Nadhani hiyo hoja siyo sahihi kabisa. Vinginevyo tutakuwa tunahamasisha *non-compliance* na hatimaye Serikali itashindwa kuijendesha. Vinginevyo hatutafika mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Jitu Soni, tuliongea na nimetoka Magala kwako, rudisha shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mto Hoja, kabla sijamwita mwenye hoja, unasema nini?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Jitu Soni, naamini anakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwamba hadhamirii kweli kushika shilingi ya mshahara wangu. Nasema siyo vyema tuweke hii *time frame*. Bunge lako likiamua kuweka *time frame* tutakuwa tumengeneza

uchochoro mkubwa sana wa kutolipa kodi mpaka huo muda ufile. Watasubiri tu kipindi hicho kipite, basi anajua kodi hiyo imeondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tuangalie na mifano ya nchi nytingine. Nenda Marekani kama hujalipa kodi hata upotee miaka kumi, ukikanyaga ardhi ya Marekani utalipa tu kodi. Sasa nchi maskini kama hii ndiyo tusilipe? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Serikali tunafanya jitihada kubwa sana sasa hivi kujenga uwezo wa kitengo chetu cha kufanya *audit* na hiki ndiyo kitapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ili tuisitengeneze uchochoro, lakini wakati huo huo tuhakikishe kwamba mambo yanakwenda, ni vizuri Mheshimiwa Jitu Soni aendelee kuiachia ili tusiweke *time frame* wakati tunaendelea kujenga uwezo wa Mamlaka ya Mapato kufanya *thorough auditing* na kuweza kupeleka hizo *returns* na madai mapema zaidi.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Jitu Soni, baada ya maelezo hayo!

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo hapa siyo watu wakwepe kulipa kodi na siyo kwamba zile kodi ambazo umeshaniletea *demand notice* na ninajua kwa mfano kwenye *income tax* natakiwa kulipa, ni pamoja na hizi *Regulatory Bodies* zote.

Wakati napewa leseni kila Mtanzania hawezি kujua sheria zote, najua sheria ile siyo kinga mahakamani, lakini unapokaa miaka kumi hujanielimisha na unaendelea kila mwaka kunipa leseni, ungekuwa umeshanipa *demand notice*, mimi ningombwa muda wa kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunachotaka ni kwamba uzembe unaofanyika huko katika taasisi zetu za kukusanya hizi kodi ili baada ya miaka kumi tuwe mbele kimaendeleo, leo tunataka hiyo iondoke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la muhimu ni kwamba elimu; kitengo siyo cha *audit* ile uendelee kuninyanya, kitengo chako cha elimu ndiyo kinatakiwa kiwe kinafanya kazi vizuri zaidi kumwelimisha mwananchi kwamba unatakiwa kulipa (a), (b), (c) na lengo hapa ni kuhakikisha kwamba *informal sector* irudi kwenye *formal*. Hapa unanifanya nikishajua kwamba miaka mitatu imepita, nabadilisha jina, nakuwa mtu mwingine. Hutani pata tena kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *loophole* hiyo ipo. Kama mkwepaji atakwepa tu. Hao wakwepaji wachache wasifanye wengine wote ambao hatuna nia ya kukwepa tuumie kwa ajili ya uzembe wa watu wachache ambao hawafanyi kazi yao vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina lengo la kushika shilingi. Lengo ni kwamba Serikali ijue kwamba taasisi nyingine zinamwangusha Mheshimiwa Waziri, siyo wewe wala Naibu wako, lakini huko chini wanafanya uzembe na huo uzembe unaafanya watu waende kudai rushwa kubwa ambapo inaumiza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa maelezo yako. Nadhani Serikali imekusikia. Kuna kazi ya kufanya hapo. Tunaendelea, Mheshimiwa Subira Mgusu.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuleta jina langu.

MWENYEKITI: Haya. Mheshimiwa Dau. Mheshimiwa Masele Augustino, Mheshimiwa Keissy.

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sikupeleka jina.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tuko hapa kutenda haki. Mimi naenda majina matatu yale, pamoja na kwamba hawamo, lakini ndiyo ukweli huo. Nimeletewa na

Chama husika. Sasa naenda kwa Mheshimiwa Ally Saleh, (Alberto).

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimesikiliza kwa makini hoja ya Mheshimiwa Waziri juu ya Akaunti ya Pamoja na ninatangaza kwamba kama sitapata majibu ya kuridhisha, nitatoa shilingi, kwa sababu Tume hii ipo Kikatiba, hata katika mapendekezo ya Warioba ilikuwemo, lakini hata katika Katiba Pendekewza tumeichukua vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuambiwa kwamba Tume hii bado inaendelea kujadiliwa, tangu iwe *concepted* mpaka hivi leo miaka 40 na bado hapajapatikana suluhu! Hata huo mgao walousema kwamba sasa 21% na 79% unakubalika, siyo wa Kikatiba, ni makubaliano ambayo hayajakuwa na nguvu za Kikatiba bado. Bado hivi sasa Zanzibar ina haki ya kupata mgao kutoka kwenye rasilimali za Muungano. Hatupati! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mgao wetu bado hauna hakika. Hizo *corporate tax* anazozisema zinakaa *accumulated* kwa muda ndiyo zinapelekwa Zanzibar, kwa sababu bado hapajakuwa na ule akaunti ambayo ingesimamia kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado sijaridhika na maelezo ya Mheshimiwa Waziri aliyoyatoa pale na ninataka maelezo ya ukamilifu, kwa nini Akaunti ya Pamoja haiundwi mpaka hivi leo? Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante. Mtoa hoja, kwa nini Akaunti ya Pamoja haiundwi?

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wowote duniani una changamoto na changamoto hizi zinajadiliwa mpaka pale ambapo mtafikia muafaka. Pande hizi mbili zimekuwa zinazungumza chini ya uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais na nakumbuka mara ya mwisho kwa maana ya kukutanisha Wizara zote ili

kuweza kusukuma mambo ambayo yanakwama, tulifanyia kule Zanzibar. Sasa ziko taarifa mbalimbali za kitaalam ambazo zimekuwa zikifanyika kuhusu namna bora zaidi ya kuhakikisha kwamba mgao basi unaridhiwa na pande mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Ally Saleh, Muungano umetufaidia pande zote na ni vizuri tukatumia busara, tusije tukaishia na kitu ambacho bado hakitatufikisha kule tunakotaka kwenda. Ni muhimu tutakapofikia hiyo *formula* iwe ni *formula* ambayo kweli itadumu. Tumekuwa na changamoto nyingi sana ambazo pole pole zimekuwa zinapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni haki ya kila upande kupata mgao sahihi na hili lote kila mtu analitambua. Ni vizuri tulifanye vizuri hata tukiling'ang'aniza wakati ambapo hatujafikia muafaka halitafanyika. Nadhani kilicho muhimu ni kuhakikisha kwamba Tume hii inaendelea kufanya kazi yake mpaka pale tutakapofikia muafaka.

Mheshimiwa Ally Saleh mimi nakuomba kabisa, katika mambo magumu ya namna hii bado lipatiwe nafasi ya kuendelea kujadiliwa kwa faida ya Muungano wetu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Saleh!

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimesikia majibu yake, lakini bado nasema kwamba uelewa wa Waheshimiwa Wabunge wengi humu wanaona Zanzibar wanabebwa na wengine wametoa mpaka kauli kwamba huku sisi hatuna chetu, lakini kumbe sisi ndio tunaonewa kwa maana ya mfumo wa matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawaziri wa Muungano humu ndani hawazidi wanne, wanaobakia wote ni Mawaziri wa Tanganyika. Ndiyo muundo ambao tunao hivi sasa na kwa hivyo ingekuwa kuna akaunti ya pamoja, tukaweka pesa zetu za Muungano hizi kadhaa halafu wale Mawaziri wa Tanganyika na Wizara zao watumie kwa Wizara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mawasiliano, siyo Wizara za Muungano, lakini wanatumia rasilimali za Muungano. Hiyo itaondoaa fitina hiyo. Pia Zanzibar inahitaji ijue chake ni kipi? Mpaka hivi leo Zanzibar hajui chake kwa maana ya mgao uliopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, naona kwamba kuna *implication* ya kisiasa ndiyo inayoogopwa isichukuliwe hatua kwamba tutajua fedha za Muungano ni kiasi gani na kwa hivyo mgao utakuwa huu, kila mmoja atata haki yake na ndiyo tutaelekeea huko kwenye Muungano ambao wa masikilizano. Kwa sababu haya yameshaingia katika Katiba Pendekewza, kwa nini isichukuliwe hatua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe hoja na niungwe mkono kwamba llijadiliwe hilli illi tujue mustakabali, lini hii Tume itaundwa na hii Akaunti ya Pamoja itaundwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kutoa hoja.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imeshapata wa kuunga mkono. Tunaanza na Mheshimiwa Ali Khamis, Mzee mwenyewe Mheshimiwa Masoud...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mtolea.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtolea na...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Khatib.

MWENYEKITI: Ngoja tutende haki na huku, unajua tena. AG, Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, unataka kuchangia? Haya Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla,

Mheshimiwa Taska, Mheshimiwa Khatib. Mheshimiwa Yussuf, mwachie huyo! Wametosha, muda jamani, mnajua na ninyi. Mheshimiwa Khatib, tunataka kujenga Muungano siyo kubomoa.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuambie, katika watu wanaopenda Muungano kama sisi hakuna, lakini tunataka Muungano wa haki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni aibu kwa watu wenyewe kujielewa kusema miaka 40 wanajadili juu ya kuunda tume ya kusimamia jambo hilli, hii ni aibu! Inaonesha ni kwa kiasi gani ambavyo dhamira ya dhati kwenye mioyo yenu hamnayo. Tuambiane ukweli, haiwezekani, yamepita mambo mengi sana na yamejadiliwa yamefikia mwisho. Leo Mheshimiwa Makamu wa Rais, kila mwaka vikao haviishi, viguu na njia, wala hakuna muafaka juu ya jambo hilli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar wakati mwingine tumekuwa; mimi ninaposimama hapa nazungumzia Jimbo langu Zanzibar, Jimbo la Konde halipo sasa hivi. Wananyanya Wabunge wengi humu tunawasikia wakisema kila siku sisi tunabebwa. Hatutaki tubebwe, kwa sababu mwanaume kamili habebwi! Tunataka kusimama kwa miguu yetu, lakini tunachotaka ni haki itendeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kwenye Muungano tunastahiki kuchangia kiasi fulani, lakini ni wajibu vile vile tujue tunastahiki kupata pato la Muungano kiasi fulani. *Otherwise*, hiyo itakuwa ni haki isiyio na wajibu. Haiwezekani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri atoe *commitment* ya kusema kwamba jambo hilli *in specific litafikia mwisho lini?* Kamati na Tume hii ya Pamoja ya Fedha...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa. Ahsante sana. Muda ndiyo huo.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Mwenyekiti, naam nashukuru...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ali Khamis kwanza. Mheshimiwa Yussuf, hapana. Mheshimiwa Ali Khamis.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Si uliniambia baada ya huyu!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ali Khamis.

MHE. ALI SALIM KHAMIS: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Jana hapa nilichangia katika hoja hii. Mambo yako wazi, katiba iko wazi, sheria iko wazi, lakini inaonekana hapa kwamba bado upande wa pili wa Muungano wa Tanganyika haujawa tayari kumaliza jambo hili na tukafikia ule Muungano ambao tuliutarajia ambao viongozi wetu walituunganisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie hapa kwamba ukiitazama Katiba yetu, mambo ambayo yametajwa ni ya Muungano, karibu Wizara zote ni za Muungano, zote! Huwezi kubagua hii ni ipi na hii ni ipi, lakini zote ni za Muungano. Ndiyo maana kinachoonekana hapa, leo upande wa pili wa Muungano unakataa kuiunda hii Tume kwa sababu wanaona kwamba Zanzibar itanufaika baada ya kupatikana haki kwa pande hizi mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo Mheshimiwa Waziri atuambie hapa, kwamba ili Muungano huo uendelee kudumu basi atuambie Akaunti hii ya Tume ya Pamoja inaanishwa lini na mapato yote ya Muungano yanaingizwa katika akaunti hii na mgao ufanyike, ili kila...

(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Tunaendelea na Mheshimiwa Taska Mbogo.

MHE. TASKA R. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Mimi simuungi mkono mto hoja, Mheshimiwa Ally Saleh kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, suala la Muungano ni mazungumzo ambayo bado yanaendelea, kwa hiyo, siyo suala la kulileta hapa kulizungumzia sasa hivi. Nafikiri mto hoja angesubiri yale mazungumzo yanayoendelea baina ya nchi mbili yatakapoisha ndiyo alete hoja zake. Kwa hiyo, siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Ally Saleh. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nimpe taarifa kwamba hakuna nchi ambayo inaitwa Tanganyika, kuna nchi inaitwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nchi ya Tanganyika ilikuwa mwaka 1964 ilipoungana na Zanzibar. Kwa hiyo, naye aeewe kwamba Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea, Mheshimiwa Masoud.

MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ally Saleh yaani Alberto kwa sababu zifuatazo:-

La kwanza, Mheshimiwa Waziri leo nitakushangaa sana, ikiwa mwenyewe unaona kwamba kwa muda wa miaka 40 tume hii haijaundwa na kwa kuwa jambo hili limo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, baada ya miaka 19 ndiyo sheria ikaundwa. Baadaye kuna kusucasua, maelezo mengi yametolewa juu ya kupatikana kwa haki hizi, nitamshangaa Mheshimiwa Waziri kama jambo hili hatasema ni lini Tume ya Pamoja ya Fedha itaundwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ingekuwa ni mtoto na mjukuu wameshapatikana zamani. Jambo hili linataka

nia, kama nia njema ipo, hakuna anayekataa Muungano. Watu wote wanataka Muungano, lakini Muungano wa aina gani? Muungano ule ambaa utatoa haki kwa pande mbili zote za Muungano.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Gekul. Mheshimiwa Paresso, *I am sorry.*

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ally Saleh. Hatuelewi ni kwa nini Serikali inapata kigugumizi kuunda hii Tume ya Pamoja. Mmekuwa mktuambia hapa Bungeni kwamba mnapunguza kero za Muungano, zinapungua lakini ukweli ni kwamba mnazidi kuziongeza na kuziimarisha kwa sababu hamtaki kuunda hii Tume ya Pamoja.

Kwa hiyo, Serikali mtuambie, kuna nini ambacho hamtaki kifanyike? Mnatuambia tusubiri wakati muafaka; huo wakati muafaka ni lini? Ni lini huo wakati utafika? Tunapoongea leo ni karibu miaka 53 ya Muungano, lakini hatuoni utekelezaji na jambo hili lipo kwa mujibu wa Katiba. Viongozi wetu mnapoapa mnasema mtailinda na kuitetea Katiba hiyo wakati mnaivunja katiba hiyo. Kwa hiyo, Serikali mtuambie ni kwa nini mnapata kigugumizi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Ally Saleh. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsilizika Mheshimiwa Ally Saleh na hoja yake, ni ya msingi kwa sababu ni suala lipo kwenye Katiba. Kama unavyofahau, masuala yote yaliyoko kwenye Katiba pia au kwenye sheria yamewekea namna ya utekelezaji. Kwa sababu suala hili linahusu pande mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameshasema hatua ambazo zimechukuliwa, suala

hili sasa linashughulikiwa na Kamati ya Masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshauri Mheshimiwa Ally Saleh, aiachie Serikali suala hili ili lihitimishwe kwenye kamati ile ya masuala ya Muungano kwa sababu linashughulikiwa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Ally Saleh airejeshe shilingi kwa bajeti ya Mheshimiwa Waziri.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa AG. Mheshimiwa *Chief Whip* wa Serikali, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba tu nimwambie Mheshimiwa Ally Saleh kwamba uzuri jambo hili tunalolizungumza hapa wote tunakubaliana kwamba ni jambo la Kikatiba. Sasa kama ni jambo la Kikatiba, haya yote yamewekewa utaratibu maalum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Orodha ya Kwanza ya Nyongeza ya Pili, unakuta mambo ya msingi yanayohusu Muungano yameelezwa pale na yapo wazi katika Katiba yetu, lakini ukenda pia kwenye Orodha ya Pili, ukurasa wa 130 wa Katiba, unakuta kabisa mambo yale yanayohusu Muungano yameelezwa pale. Vilevile kama unataka kutafsiri Baraza la Mawaziri katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ukienda kwenye katiba Sehemu ya Tatu imetoa maelezo fasaha kabisa. Sehemu ya Nne ya Katiba inaeleza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haya mambo yote ni ya Kikatiba, hata hili suala linalohusu masuala ya fedha kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa ni masuala ya Kikatiba huwezi ukakaa tu hapa ndani Waziri akasema akatoa *commitment* hapa ndani, yana utaratibu wake wa kuyashughulikia ili kufikia muafaka. Hivyo ndivyo itakavyotusaidia kuyashughulikia bila kuvunja katiba tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo tunaweza tukawa tunakuja humu ndani tunatoa matamko ambayo yanaenda kinyume na katiba tulionayo. Namwomba Mheshimiwa Saleh aipe Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utaratibu uliowekwa, tutakuja siku tutapata suluhu na kero za Muungano tutaendelea kuzitatua na Muungano wetu utadumu na Mheshimiwa Ally Saleh ataendelea kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa AG.

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Ally Saleh, baada ya maelezo hayo ya wote waliochangia wakikusihi. Kuna neno?

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Baada ya maelezo hayo, ndiyo kwanza nazidi kusema nitaitoa shilingi, kwa sababu hiyo kamati anayoisema ya majadiliano haina baraka za Kikatiba, siyo ya Kikatiba, haikuundwa Kikatiba, hilo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hicho anachosema kwamba haya mambo anakubali kama ni ya Kikatiba, kwa hivyo Katiba imesiginwa kwa miaka 40. Kwa hiyo, natoa hoja Bunge liamue kwa kupiga kura. Ahsante.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

MWENYEKITI: Ahsante. Wasioafiki wameshinda. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Flatei.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, katika mchango wangu nilielezea kabisa suala la VATkwenye msamaha hasa wa kodi kwa wafadhili hasa kwenye Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namtaka Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa jambo langu analifahamu na nimelizungumzia sana leo, anisaidie kwa sababu jambo hili linakumba maeneo mengi hasa katika misaada ya wafadhili ambayo moja kwa moja inasaidia Tanzania na Taifa kwa ujumla na kwa sababu tu jambo hili tunalotaka hatuna maana mbaya tuna maana ya kuisaidia Tanzania na fedha hizi au misaada tunayoipata hata Serikali inahitaji ili kuwasaidia watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kutusaidia sasa, tunafanyaje katika suala hili la msamaha wa kodi wa VAT ambayo inatokana na misaada ya wafadhili na kuna sharti hili ambalo linapaswa kutafuta mahali popote pa kulipa msamaha wa kodi? Yeye kwa kweli hana jinsi ya kutusaidia, hasa anaweza kuniambia nini ili tusipate hasara na wale wafadhili wasiweze kukimbia?

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Kama sijaelewa...

MWENYEKITI: Mtoa hoja.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ni kweli kabisa hii hoja imewasilishwa kwangu mara nyingi na jibu langu lina sehemu mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba sana Wabunge katika Majimbo yao wanapokumbana na jambo kama hili ambalo limemkuta mwenzetu huyu pamoja na Wabunge wengine, kitu cha kwanza tuwakumbushe kwamba kabla hawajaingia mikataba na haya mashirika, wahakikishe kwamba wanaihusisha Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi nimekuwa napata maombi baada. Kwa hiyo, hilo ni la kwanza, ni muhimu sana Wizara ya Fedha ihusishwe kuanzia mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa maana ya kutafuta suluhisho, nimemshauri Mheshimiwa Flatei na wengine wenyewe tatizo kama hilo walete maombi Wizara ya Fedha na tutayaangalia *on merit* ili tuone kama pale ambapo Halmashauri kweli haiwezi kulipa hiyo kodi, basi Serikali Kuu iweze kubeba hilo jukumu ili wananchi wasikose hiyo huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, yapo maeneo ambayo tayari tumeyapatia ufumbuzi na yale yalikuwa yanahusu nani asaini ule mkataba? Sheria iko wazi, mwenye mamlaka ya kusaini misamaha ile na mikataba ni Waziri mwenye dhamana ya fedha. Kwa hiyo, viongozi wa Halmashauri walikuwa hawawezi kusaini ile mikataba ya makubaliano baina wahisani na Halmashauri. Tumelitafutia ufumbuzi wa kurekebisha kanuni na basi hili...

(Hapa kengele illia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Flatei.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anafahamu kabisa kwamba nimepeleka ombi hilo na ni muda umefika sasa, lakini pia anafahamu kwamba wafadhili wamenipa muda na ukweli ni kwamba nashukuru majibu yake ya kwanza, anasema anatafuta huo mwanya, lakini muda umefika sasa wafadhili wanaondoka kwa sababu pesa zinaondoka na Serikali haijatupa pesa ya kujenga daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitoe hoja tujadili ili Serikali ije na mpango wa kudumu na siyo mpango wa haraka ambao hautaweza kupelekea wafadhili wakatuelewa. Naomba kutoa hoja.

MWENYEKITI: Ahsante. Waheshimiwa tunaingia kwenye *guillotine*. Katibu.

Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango

Kif. 1001 – <i>Administration &HR Mg'nt</i>	Sh. 7,371,377,000
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 1,229,030,000
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i>	Sh. 31,767,929,000
Kif. 1004 – <i>Legal Service</i>	Sh. 1,447,780,000
Kif. 1005 – <i>Government Comm. Unit</i>	Sh. 380,243,000
Kif. 1006 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 545,213,000
Kif. 1007 – <i>MCC Tanzania</i>	Sh. 0
Kif. 1008 – <i>Procurement Mg'nt Unit</i>	Sh. 749,648,000
Kif. 1009 – <i>Public Procurement Policy Unit</i>	Sh. 0
Kif. 1010 – <i>Information & Comm. Techn</i>	Sh. 961,747,000
Kif. 3001 – <i>Internal Audit General</i>	Sh. 3,204,496,000
Kif. 5001 – <i>Government Asset mg'nt Div</i>	Sh. 4,589,111,000
Kif. 6001 – <i>Financial Mgt. Inform. Syst. Div</i>	Sh. 2,793,069,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 7 – Msajili wa Hazina

Kif. 1001 – <i>Administration &HR Mgt</i>	Sh. 1,618,779,750
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 258,956,349
Kif. 1003 – <i>Planning Unit</i>	Sh. 198,811,623
Kif. 1004 – <i>Legal Services Unit</i>	Sh. 210,907,800
Kif. 1005 – <i>Procurement Mg'nt Unit</i>	Sh. 123,928,800
Kif. 1006 – <i>Information Comm. Techn</i>	Sh. 327,008,600
Kif. 1007 – <i>Inform. Educ. & Comm. Unit</i>	Sh. 145,671,826
Kif. 1008 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 211,152,374
Kif. 2001 – <i>Public Investment Mgt. Div</i>	Sh. 100,640,334,300
Kif. 3001 – <i>Privatization and Monitoring</i>	Sh. 563,275,789
Kif. 4001 – <i>Management Service Div</i>	Sh. 618,660,789

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha

Kif. 1001 – <i>Administration & HR Mgt.</i>	Sh. 1,174,377,511
Kif. 1002 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 42,600,000
Kif. 2001 – <i>Technical Department</i>	Sh. 99,340,000
Kif. 2002 – <i>Zanzibar Office</i>	Sh. 70,500,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu

Kif. 1001 – <i>Administration & HR Mg'nt Unit</i>	Sh. 966,580,000
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh. 34,520,443
Kif. 1003 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh. 5,850,000
Kif. 1004 – <i>Monitoring Unit</i>	Sh. 63,000,000
Kif. 1005 – <i>Inspect Unit</i>	Sh. 193,450,000
Kif. 1006 – <i>Procurement Mg'nt Unit</i>	Sh. 7,050,000
Kif. 1007 – <i>Legal Service Unit</i>	Sh. 56,780,000
Kif. 1008 – <i>Mg'nt Inform. Syst.Unit</i>	Sh. 188,355,557

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 21 – Hazina

Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 809,301,000
---	-----------------

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)

Kif. 1009 – <i>Public Procurement Policy Unit</i>	Sh. 967,435,000
Kif. 2001 – <i>Government Budget Div</i>	Sh. 238,844,003,000
Kif. 2002 – <i>Policy Analysisi Division</i>	Sh. 297,249,987,000
Kif. 4001 – <i>External Finance Division</i>	Sh. 40,408,747,000
Kif. 4002 – <i>Public Private Partnership Unit</i>	Sh. 836,072,000
Kif. 7001 – <i>Proverty Eradication and Empowerment</i>	Sh. 1,213,703,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 22 – Deni la Taifa

Kif. 1001 – Admin. & HR Mgt.....Sh. 9,472,122,300,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiiliko yoyote)

Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali

Kif. 3001 – *Public Debt Management*.....Sh. 144,000,000
Kif. 3002 – *Expenditure Management*Sh. 4,489,767,500
Kif. 3003 – *Financial Management*.....Sh. 35,519,968,644
Kif. 3004 – *Financial Systems*Sh. 3,150,000,000
Kif. 3005 – *Sub Treasury Arusha*Sh. 82,275,379
Kif. 3006 – *Sub Treasury Coast*.....Sh. 84,595,535
Kif. 3007 – *Sub Treasury Dodoma*.....Sh. 187,954,900
Kif. 3008 – *Sub Treasury Iringa*.....Sh. 83,142,786
Kif. 3009 – *Sub Treasury Kagera*.....Sh. 81,943,928
Kif. 3010 – *Sub Treasury Kigoma*.....Sh. 82,639,634
Kif. 3011 – *Sub Treasury Kilimanjaro*.....Sh. 83,138,311
Kif. 3012 – *Sub Treasury Lindi*.....Sh. 83,221,671
Kif. 3013 – *Sub Treasury Mara*.....Sh. 82,757,640
Kif. 3014 – *Sub Treasury Mbeya*.....Sh. 82,938,280
Kif. 3015 – *Sub Treasury Morogoro*.....Sh. 87,081,416
Kif. 3016 – *Sub Treasury Mtwara*.....Sh. 82,938,280
Kif. 3017 – *Sub Treasury Mwanza*.....Sh. 87,578,592
Kif. 3018 – *Sub Treasury Rukwa*.....Sh. 83,932,633
Kif. 3019 – *Sub Treasury Ruvuma*.....Sh. 87,412,866
Kif. 3020 – *Sub Treasury Shinyanga*.....Sh. 82,689,692
Kif. 3021 – *Sub Treasury Singida*.....Sh. 85,080,116
Kif. 3022 – *Sub Treasury Tabora*.....Sh. 84,787,279
Kif. 3023 – *Sub Treasury Tanga*.....Sh. 85,921,338
Kif. 3024 – *Sub Treasury Manyara*.....Sh. 88,016,107
Kif. 3025 – *Sub Treasury Njombe*.....Sh. 107,308,103
Kif. 3026 – *Sub Treasury Geita*.....Sh. 87,412,868
Kif. 3027 – *Sub Treasury Katavi*.....Sh. 87,131,134
Kif. 3028 – *Sub Treasury Simiyu*.....Sh. 87,081,416
Kif. 3029 – *Sub Treasury Songwe*.....Sh. 82,966,587
Kif. 4001 – *Local Government Finances*.....Sh. 130,102,400
Kif. 7001 – *Pension and Gratuity*.....Sh. 285,052,956

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 45 – Mkaguzi Mkuu wa Serikali

Kif. 1001 – *Administ. & HR Mg'nt Div.*..... Sh. 14,956,609,250

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)

Kif. 1002 – *Finance and Accounts Unit*Sh. 1,246,693,249

Kif. 1003 – *Internal Audit Unit* Sh. 294,181,080

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1004 – *Ministerial Audit Division*Sh. 7,821,164,017

Kif. 1005 – *Local Govn't Authorities Div.*.....Sh. 12,050,422,292

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)

Kif. 1006 – *Performance Audits Division*.....Sh. 2,390,457,892

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kif. 1007 – *National Account Division*Sh. 11,837,191,025

Kif. 1008 – *Techn. Support Service Unit*.....Sh. 4,283,139,000

Kif. 1009 – *Public Authorities Audit Div.*.....Sh. 3,117,510,804

Kif. 1010 – *Planning, Monitoring & Evaluation*Sh. 709,951,864

Kif. 1011 – *Procurement Mg'nt Unit*..... Sh. 397,740,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na marekebisho yake)

Kif. 1012 – *Inform. & Comm. Techn. Unit*Sh. 1,510,481,401

Kif. 1013 – *Forensic Audit Unit*Sh. 334,608,000

Kif. 1014 – *Quality Assurance Unit*Sh. 614,400,000

Kif. 1015 – <i>Government Comm. Unit</i>Sh.	55,000,000
Kif. 1016 – <i>Risk Mg'nt & Compliance Unit</i>Sh.	19,000,000
Kif. 1017 – <i>Legal Service Unit</i>Sh.	99,400,000
Kif. 1018 – <i>Parliamentary Coordination Unit</i>Sh.	94,998,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 66 – Tume ya Mipango

Kif. 1001 – <i>Administration & HR Mg'nt</i>	Sh. 1,625,804,631
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i>	Sh. 169,372,000
Kif. 1003 – <i>Planning and Monitoring Div</i>Sh.	245,586,369
Kif. 1004 – <i>Government Comm. Unit</i>Sh.	158,565,000
Kif. 1005 – <i>Internal Audit Unit</i>Sh.	214,796,000
Kif. 1006 – <i>Procurement Mg'nt Unit</i>Sh.	164,290,000
Kif. 1007 – <i>Library and Doc. Unit</i>	Sh. 132,096,000
Kif. 1008 – <i>Management Inform. Syst</i>Sh.	191,598,000
Kif. 2001 – <i>Macro Economy Cluster</i>Sh.	800,587,000
Kif. 2002 – <i>Productive Sector Cluster</i>Sh.	312,556,000
Kif. 2003 – <i>Infrastructure and Service Cluster</i>	Sh. 295,396,000
Kif. 2004 – <i>Social Service and Demographics Cluster</i>	Sh. 329,581,000
Kif. 2005 – <i>International Trade and Econ. Relation</i>	Sh. 296,136,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MATUMIZI YA MAENDELEO

Fungu 7 – Msajili wa Hazina

Kif. 1003 – <i>Planning Unit</i>	Sh. 375,000,000
Kif. 1004 – <i>Legal Service Unit</i>	Sh. 100,000,000
Kif. 1006 – <i>Information and Comm. Technology</i>	Sh. 700,000,000
Kif. 1007 – <i>Information, Education and Comm. Unit</i>	Sh. 0

Kif. 2001 – *Public Investment Mgt Div*..... Sh. 480,000,000
Kif. 3001 – *Privatization and Monitoring* Sh. 85,000,000
Kif. 4001 – *Management Service Division*Sh. 260,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 21 – Hazina

Kif. 1009 – *Public Procurement Policy Unit*..... Sh. 0
Kif. 2001 – *Government Budget Div*..... Sh. 1,356,335,354,000
Kif. 2002 – *Policy Analysis Division*..... Sh. 29,613,324,337
Kif. 4001 – *External Finance Division*.....Sh. 4,488,023,404
Kif. 4002 – *Public Private Partnership Unit* Sh. 5,000,000,000
Kif. 7001 – *Poverty Eradication and Empowerment* Sh. 200,000,000
(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali

Kif. 3002 – *Expenditure Management* Sh. 68,000,000
Kif. 3003 – *Financial Management*Sh. 3,127,000,000
Kif. 3004 – *Financial System*Sh. 305,000,000
Kif. 4001 – *Local Government Finances*Sh. 100,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 45 – Mhasibu Mkuu wa Serikali

Kif. 1001 – *Administ. & HR Mg'nt Div*..... Sh. 6,400,000,000
Kif. 1010 – *Planning, Monitoring and Evaluation Div*Sh. 5,400,948,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango

Kif. 1001 – *Administration and HR Mgt*..... Sh. 0
Kif. 1003 – *Policy and Planning* Sh. 6,260,000,000

Kif. 1004 – *Legal Service*Sh. 1,000,000,000
Kif. 1005 – *Government Comm. Unit*Sh. 0
Kif. 3001 – *Internal Audit General*.....Sh. 1,500,000,000
Kif. 5001 – *Government Asset mgt Div*.....Sh. 1,000,000,000
Kif. 6001 – *Financial Mgt. Inform.*
Systems DivisionSh. 1,810,500,000

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 66 – Tume ya Mipango

Kif. 2001 – *Macro Economy Cluster*Sh. 0
Kif. 2002 – *Productive Sector Cluster*Sh. 579,000,000
Kif. 2004 – *Social Service & Demographics Cluster*Sh. 3,896,800,000

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarudia.

(Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tuketi. Mtoa hoja, taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi zake, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 – Wizara ya Fedha na Mipango, yalipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Nitamke kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2017/2018 yamepitishwa na Bunge.

Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu wake lakini pia na timu ya wataalamu, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu pamoja na *machinery* yote iliyofanikisha hili pamoja na Tume ya Mipango. Siyo kazi nyepesi, lakini tunawapongezeni. Katika kuwapongeza tunaamini fedha hizi katika mwaka ujao zitaweza kupatikana kwa wakati kwa kutegemea makusanyo ya Serikali ili tuweze kutekeleza majukumu yetu kwa wananchi.

Baada ya kusema hayo, sina matangazo na muda wetu ndiyo huo. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho, siku ya Alhamisi, tarehe 1Juni, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 2.12 usiku Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 1 Juni, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*